# Nipashe

Jumatano Novemba 27, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580086

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Mbunge anayetaka uenyekiti Chadema aanika sera zake

UKURASA 3




UKURASA 13


## YALIYOMO

**UKURASA WA 3**

**NHC YAPEWA SIKU 90 KUHAKIKI WAPANGAJI**
SERIKALI imelipa miezi mitatu Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kufanya uhakiki wa miradi ya ubia waliyoingia na watu binafsi pamoja na nyumba zake...

**UKURASA WA 4**

**ONGEZEKO LA WATU LAIWEKA SEKTA UHIFADHI NJIA PANDA-3**
KATIKA sehemu ya ripoti hii jana, ilielezwa nafasi ya utalii na uhifadhi katika uchumi wa taifa. Endelea na sehemu...

**UKURASA WA 5**


**WB, SERIKALI WAJITOSA MAPINDUZI ELIMU UFUNDI**
SERIKALI kwa kushirikiana na Benki ya Dunia, wanatekeleza mradi wa kuleta mapinduzi kwenye elimu ya ufundi Afrika Mashariki (EASTRIP)...


# Tahadhari walaji nyama kitimoto

**YADAIWA** kuwa na minyoo ya kifafa, mikoa vinara kwa waathirika yawekwa bayana...*Endelea ukurasa wa 2*

## MADUDU USHIRIKA YAFIKISHWA TAKUKURU

UKURASA 3




## VIFURUSHI VIPYA BIMA AFYA SASA HADHARANI

UKURASA 2






**MICHEZO** SIMBA, YANGA ZAPEWA MBINU MAFANIKIO CAF UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA

# Tahadhari walaji nyama ya nguruwe

**Na Woinde Shizza, ARUSHA**

MINYOO aina ya tegu inayotoka kwenye nyama ya nguruwe (cysticercodis) imedaiwa kuwa tishio kwa walaji wa nyama hiyo na kusababisha kifafa kwa binadamu.

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, alitoa tahadhari hiyo wakati akifungua mkutano wa kwanza wa kimataifa jana wa kujadili minyoo ya tegu wa nguruwe, jijini hapa.

Dk. Ndugulile, alisema serikali haijapata chanjo ya kumzuia mnyoo huyo wa nguruwe na ipo katika utafiti wakuangalia namna ya kumdhibiti.

Alisema walaji wa nguruwe wafahamu kuwa kuna minyoo inayopatikana kwenye nyama hiyo kupitia mayai na inaweza kumuathiri binadamu endapo atakula nyama isiyopikwa vizuri na mboga ambazo hazijaoshwa na kupikwa vizuri.

Dk. Ndugulile alisema athari zinazotokana na kula nyama hiyo ni kubwa ikiwamo kupata ugonjwa wa kifafa, tatizo ambalo limeshaingia nchini na limeanza kuathiri zaidi mikoa ya Manyara, Njombe, Mbeya, Sogwe na Arusha, huku asilimia 16 ya wananchi wanaoishi mikoa hiyo wakiathirika kwa ugonjwa huo.

"Jinsi ya kutokomeza ugonjwa huu wa minyoo wa tegu wa nguruwe, ni wafugaji kufuga kisasa na kuacha wanyama wao kuzurura ovyo kwa sababu huacha kinyesi chenye mnyoo huyo katika mboga," alisema.

Pia, aliwataka wafugaji kupata ushauri kitalaamu wa mifugo na wachinjaji wasichinje bila kizingatia utaalamu unaosimamia wanyama hao.

Aliwataka wanaokula nyama hiyo kuhakikisha inapikwa vizuri na kuiva.

Hata hivyo, alisema wafugaji wanaweza kuzuia kwa mifugo yao kuzagaa na kupima mnyama kabla ya kuchinja.

Mkurugenzi mkuu wa Taasisi ya magonjwa ya binadamu (NIMR), Prof. Yunus Mgaya, alisema wanatekeleza mradi huo kwa kukusanya taarifa za mnyoo huyo mbaye anapatikana kwa kula mboga zilizobeba mayai yaliotokana na vinyesi vya nguruwe au kinyesi cha binadamu.

"Mradi huu unatekelezwa na nchi zingine mbili Afrika Msumbiji na Zambia na tunashirikiana na wadau wetu wa utafiti wa Ujerumani kutoka Chuo Kikuu cha Munchen," alisema.

Kaimu Mkuu wa idara ya tiba ya mifugo na afya ya jamii ambaye pia ni Mkurugenzi wa mtandao wa utafiti wa kisayansi Prof. Helena Ngowi, alisema mnyoo huyo ni hatari kwa sababu anaweza kuleta adhari katika utumbo na ubongo wa binadamu.

# Vifurushi vipya bima ya afya bayana

**Na Romana Mallya**

MFUKO wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), umetangaza vifurushi vipya vitatu vya bima ya afya, vinavyoonyesha matibabu kwa kila umri na kundi.

Aidha, vifurushi hivyo ambavyo vinatarajia kuzinduliwa kesho na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu (pichani), vimegawanyika katika umri wa miaka 18 hadi 35, miaka 36 hadi 59 na miaka 60 kuendelea.

Kwa mujibu wa taarifa iliyopatikana jana jijini Dar es Salaam na kuthibitishwa na NHIF, vifurushi hivyo ni Ninajali Afya, Wekeza Afya na Timiza Afya.

Vifurushi hivyo vimeonyesha ukubwa wa familia ikiwa ni mtu binafsi, wenza na mtoto mmoja hadi wanne pamoja na wazee wa miaka 60 kuendelea.



**MTU BINAFSI**

Taarifa hiyo imeonyesha kuwa mtu binafsi mwenye umri wa miaka 18 hadi 35 katika kifurushi cha Ninajali Afya ni Sh. 192,000, Wekeza Afya Sh. 384,000 na Timiza Afya Sh. 516,000.

Kwa mtu binafsi wenye umri wa miaka 35 hadi 59, Najali Afya ni Sh. 240,000, Wekeza Afya Sh. 444,000 na Timiza Afya Sh. 612,000.

Pia, imebainisha kuwa mtu binafsi mwenye umri wa miaka 60 kuendelea kwa kifurushi cha Najali Afya Sh. 360,000, Wekeza Afya Sh. 660,000 na Timiza Afya Sh. 984,000.

WENZA BILA WATOTO

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, wenza wasio na watoto wenye umri wa miaka 18 hadi 35 kifurushi cha Ninajali Afya ni Sh. 384,000, Wekeza Afya Sh. 732,000 na Timiza Afya Sh. 996,000.

Kwa wenza wenye umri wa miaka 36 hadi 59 kifurushi cha Ninajali Afya ni Sh. 456,000, Wekeza Afya Sh. 864,000 na Timiza Afya Sh. 1,188,000.

**MTU MWENYE WATOTO**

Taarifa hiyo imeonyesha kuwa mtu binafsi na mtoto mmoja hadi wanne wanaweza kugharamia vifurushi hivyo kwa gharama zifuatazo:

Wenye umri wa miaka 18 hadi 35 mwenye mtoto mmoja hadi wanne kifurushi cha chini katika eneo la Ninajali Afya ni Sh. 540,000 na cha juu ni Sh. 816,000.

Kwa eneo la Wekeza Afya mwenye idadi hiyo ya watoto kifurushi cha chini ni Sh. 924,000 hadi Sh. 1,452,000 na kifurushi cha Timiza Afya kiwango cha chini ni Sh. 1,272,000 na cha juu ni Sh. 2,028,000.

Kwa umri wa miaka 36 hadi 59 eneo la Ninajali Afya kifurushi cha chini ni Sh. 576,000 na cha juu ni Sh. 900,000.

Aidha, eneo la Nawekeza Afya, kifurushi cha chini ni Sh. 1,068,000 na cha juu ni Sh. 1,584,000. Kwa eneo la Timiza Afya kima cha chini ni Sh. 1,464,000 na cha juu ni Sh. 2,220,000.

Taarifa hiyo inaonyesha kuwa mtu binafsi mwenye mtoto mmoja hadi wanne mwenye umri wa miaka 18 hadi 35, kifurushi cha Ninajali Afya kiwango cha chini Sh. 312,000 na cha juu Sh. 636,000 na kifurushi cha Timiza Afya kiwango cha chini ni Sh. 792,000 na cha juu Sh. 1,648,000.

Pia, katika kifurushi cha Wekeza Afya kwa kundi hilo, kiwango cha chini Sh. 576,000 na cha juu ni Sh. 1,092,000.

Taarifa hiyo imeonyesha wenye umri wa miaka 36 hadi 59 ambao wana watoto umri huo kwa kifurushi cha Ninajali Afya kiwango cha chini ni Sh. 360,000 na cha juu ni Sh. 672,000 huku kwenye Wekeza Afya kiwango cha chini Sh. 648,000 na cha juu Sh. 1,164,000.

Aidha, kifurushi cha Timiza Afya kiwango cha chini ni Sh. 888,000 na cha juu ni Sh. 1,644,000.

**JUU YA MIAKA 60**

Kwa wenye umri wa miaka 60 kuendelea eneo la Ninajali Afya kiwango cha chini ni Sh. 360,000 na cha juu 684,000.

Aidha, eneo la Nawekeza Afya wa umri huo kiwango cha chini ni Sh. 660,000 na cha juu ni Sh. 1,284,000.

Katika kifurushi cha Timiza Afya kiwango cha chini ni Sh. 684,000 na kiwango cha juu ni Sh. 1,800,000 na kwamba umri huo umehesabiwa kwa mtu mmoja na wenza.

HUDUMA ZITOLEWAZO

Vifurushi hivyo vinahusisha kwenye huduma za kumuona daktari, kulazwa Chumba cha Uangalizi Maalum (ICU), uchunguzi, X-Ray na rufani mbalimbali kutoka zahanati hadi hospitali za mkoa na dawa.

Aidha, Najali Afya na Wekeza Afya havitakuwa huduma ya vipimo vya MRI huku kifurushi cha Timiza Afya huduma hiyo ikitolewa mara moja na mgonjwa atachangia asilimia 50.

Huduma ya CT- Scan kwenye kifurushi cha Ninajali Afya haitakuwapo lakini kwenye Wekeza Afya kitatolewa kwa mwaka mmoja na baada ya hapo mgonjwa atatakiwa kuchangia asilimia 50.

Kwa upande wa kifurushi cha Timiza Afya mgonjwa atachangia asilimia 25. Kifurushi cha Najali Afya na Wekeza Afya hakitahusika na huduma za ICU.

# Mbowe adaiwa kuugua dengue

**Na Hellen Mwango**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe, anayekabiliwa na wenzake katika kesi ya uchochezi amedai mahakamani bado anasumbuliwa na maradhi ya dengue, malaria na shinikizo la damu.

Kadhalika, Mbowe kupitia wakili wa utetezi Peter Kibatala, amedai afya yake haijaimarika na kwamba hatamudu kuendelea kutoa ushahidi.

Maombi hayo yaliwasilishwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba anayesikiliza kesi hiyo katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam.

Upande wa Jamhuri ukiongozwa na Mkurugenzi Msaidizi wa Mashtaka, Faraja Nchimbi, ulidai kuwa kesi hiyo imepangwa kwa ajili ya kuendelea na ushahidi wa utetezi ikiwamo mshtakiwa kuhojiwa na upande wao na kwamba wako tayari kuendelea.

Hata hivyo, Kibatala alidai kuwa kama mawakili wako tayari kuendelea lakini shahidi (Mbowe) hali ya afya yake si nzuri hivyo anaiomba muda mahakama mteje wake apumzike.

Alidai kuwa kwa sababu kesi hiyo ni ya jinai, lakini mshtakiwa anasumbuliwa na maradhi ya homa ya dengue, malaria na shinikizo la damu ameona ni muhimu kutii mahakama na kuja kusikiliza kesi hiyo.

"Wiki iliyopita mshtakiwa alilazwa Novemba 22, na aliruhusiwa kutoka Hospitali ya Aga Khan kutokana na afya yake kuwa haijaimarika anaomba muda wa kupumzika kwa sababu hali yake si nzuri ili aje kuendelea na ushahidi kwa kujibu maswali ya Jamhuri," alidai Kibatala.

Upande wa Jamhuri ulipinga ombi hilo kwa madai kuwa wiki iliyopita walipokea taarifa ya kuumwa kwa Mbowe iliyoambatanishwa na vyeti vya matibabu.

INAENDELEA UK 26

## HABARI KITAIFA

## Madudu ya ushirika yatua Takukuru

Na Augusta Njoji, DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga, amekabidhi ripoti ya ukaguzi wa vyama vya ushirika kwa mwaka 2018/19 kwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) ambayo imebaini ubadhirifu wa zaidi ya Sh. bilioni 124.05.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini hapa, Hasunga alisema katika mwaka wa fedha wa 2018/19, Serikali ilitoa maagizo kwa Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (Coasco) kukagua vyama vya ushirika vyote 11,410 vyenye usajili hadi Juni, mwaka huu.

"Kati ya vyama hivyo, hai ni 6,463, vyama sinzia ni 2,844 na vyama ambavyo havipatikani ni 2,103. Hadi kufikia Juni 30, Coasco ilikagua vyama vipatavyo 4,413 sawa na asilimia 102.63 ya lengo la serikali la kukagua vyama 4,300," alisema.

INAENDELEA UK 8

## NHC yapewa siku 90 kuhakiki wapangaji

Na Romana Mallya

SERIKALI imelipa miezi mitatu Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kufanya uhakiki wa miradi ya ubia waliyoingia na watu binafsi pamoja na nyumba zake baada ya kubainika kuwapo kwa wajanja wanaojinufaisha nazo.

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wiliam Lukuvi, alitoa agizo hilo jana jijini Dar es Salaam baada ya juzi kutembelea miradi ya shirika na kutaka ifikapo Machi 30, mwakani, uhakiki huo uwe umekamilika.

"Ninajua kuna baadhi ya wapangaji wameanzisha vishirika vya nyumba ndani yenu, kuna watu

INAENDELEA UK 8



Mbunge wa Ndanda mkoani Mtwara, Cecil Mwambe (Chadema), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati akitangaza dhamira yake ya kugombea nafasi ya Mwenyekiti wa Taifa wa chama hicho. 3. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mbunge anayetaka uenyekiti Chadema aanika sera zake

Na Mary Geofrey

MBUNGE wa Ndanda, Cecil Mwambe, ametaja kilichomsukuma kutaka kuchukua mikoba ya Freeman Mbowe kukiongoza Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema).

Mwambe amekuwa mwanachama wa kwanza wa chama hicho kikuu cha upinzani nchini kutangaza kuchuana na Mbowe katika kinyang'anyiro cha nafasi ya mwenyekiti wa chama hicho wakati wa uchaguzi wa chama uliopangwa kufanyika Desemba 18, mwaka huu.

Hata hivyo, Mbowe bado hajatangaza kama ana nia ya kuendelea kuwania nafasi hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mwambe ambaye pia ni mjumbe wa Kamati Kuu ya Chadema, alisema endapo akishinda katika uchaguzi huo, atawaunganisha viongozi wote wa vyama vya upinzani ili wakae meza moja na serikali kuondoa tofauti za kisiasa zilizomea nchini.

Alisema Tanzania inahitajika siasa safi ili wananchi wapate maendeleo ya kweli, akisisitiza kuwa siasa chafu zinavuruga amani ya taifa.

"Nikipata nafasi hii, nitawakusanya viongozi wenzangu wote wa vyama vya upinzani, tutengeneze ajenda ya pamoja, tutawaona viongozi wa chama tawala ili kuona namna ya kuondoa tofauti zetu.

"Si kweli kuwa nchi yetu haihitaji upinzani na kama hawataki watatueleze kwa sababu sijawahi kuona kuwapo kwa mazungumzo ya pamoja," Mwambe alisema.

Mwenyekiti huyo wa Chadema Kanda ya Kusini alisema endapo akichaguliwa kushika nafasi hiyo, atahakikisha anaondokana na adui namba moja aliyemwita mtambuko wa kisiasa.

"Kama mtakumbuka, hivi karibuni sisi vyama vyetu vya upinzani tumesusia kushiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Lazima jambo hili lifike mwisho na mwisho wa hili jambo ni kukaa meza ya mazungumzo ili kusema mahitaji yetu. Kwanini tulisusia na nini mahitaji yetu ya msingi?

"Mwisho wa siku, siasa ni maisha, na kama ni hivyo, basi tuangalie ni namna gani watu wanaweza kutoka mbele kwa sababu siasa ndiyo inapanga bei ya unga, bei ya sukari na inapanga bei ya chumvi," Mwambe alisema.

Aliongeza kuwa chama hicho kina wenyeviti 10 wa mikoa na wajumbe wa kamati kuu, hivyo kiongozi yeyote anaweza kushika nafasi hiyo kumsaidia mwenyekiti kama ingetokea kutakiwa kufanya hivyo.

"Nimejipima nikajiona ninafaa kuwania nafasi hii kwa sababu chama chetu ni cha kidemokrasia iliyo wazi, hivyo nikaona basi naweza kugombea nafasi ya mwenyekiti wa chama chetu," Mwambe alisema.

Mbunge huyo wa Ndanda mkoani Mtwara alikiri kuwa Mbowe amefanya mambo makubwa wakati wote wa uongozi wake, lakini hakumpi tiketi ya kuendelea kuongoza kwa sababu kila binadamu ana ukomo wa uvumilivu wa maisha na ndiyo sababu ya kuamua kuchuana naye katika uchaguzi huo.

Alisema wanahitaji kumpokea kijiti mwenyekiti wao huyo ili kuboresha yale aliyofanya na kukifanya chama hicho kuwa imara zaidi ili kishike dola.

Mwambe alisema chama hicho kwa sasa kinahitaji mwenyekiti mwanaharakati atakayefanya kazi kimkakati ili kukisaidia kutimiza lengo lake la kushika dola.

Mwambe aliwaomba wajumbe wa kamati kuu kuondokana na makundi ya ushabiki ili kuchagua kiogozi atakayekisaidia chama kusonga mbele na kufikia malengo yao.

Alisema alichukua fomu mtandaoni Desemba 26, mwaka huu, akaijaza na kuilipia ada ya Sh. milioni moja na aliirudisha Ofisi ya Chadema.

Uchukuaji wa fomu za kuwania nafasi mbalimbali za juu za uongozi ndani ya Chadema unaendelea katika ofisi za chama hicho zilizoko maeneo mbalimbali nchini hadi Novemba 30 mwaka huu saa 10:00 jioni utakapofungwa.


MASETO AUCTIONEER & DEBT COLLECTOR LTD

### NOTISI/TANGAZO LA MNADA

Kwa idhini tuliyopewa na **FIRST NATIONA BANK (FNB), MASETO AUCTIONEER & DEBT COLLECTOR LTD** tunatangaza kuuza dhamana za wadaiwa sugu walioshindwa kulipa mikopo yao katika Benki tajwa hapo juu kama watashindwa kulipa madeni yao ndani ya siku 14 tangu kutolewa kwa tangazo hili. Minada hii itafanyika kama inavyoonesha hapa chini;

| S/N | JINA LA MTEJA | UMILIKI WA DHAMANA | AINA YA DHAMANA NA MAHALI ILIKO | TAREHE NA MUDA WA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| 001 | JOHN ELISHA ABEL | JOHN ELISHA ABEL | NYUMBA YENYE HATI MILIKI NO. 159221 ILIYOKO KIWANJA NO. 41, BLOCK J, KIZINGA AREA– WILAYA YA ILALA | 11/12/2019 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 002 | DENIS KASHAIJA MUSHEMA | DENIS KASHAIJA MUSHENA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI NO. 5387, ILIYOKO KIWANJA NO. 159, BLOCK I, TUANGOMA – WILAYA YA TEMEKE | 13/12/2019 SAA 04:00 ASUBUHI |

Masharti ya mnada

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku hiyo hiyo ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14) kukamilisha malipo yote, ukishindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25% na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama za kuona, kukaguwa, kuhamisha umiliki, na zingine zinazoambatana na hili ni juu ya mnunuzi.

KWA TAARIFA ZAID WASILIANA NASI KUPITIA ANUANI HIZI:
MKURUGENZI MTENDAJI,
MASETO AUCTIONEER,
P.O BOX 75087,
DAR ES SALA
+255 765 999 000 AU +255 787 288 442 AU +255 762 260 787

215533602



## KUMBUKUMBU



Faustin S. Chale
17 Oktoba 1936 – 26 Novemba 2018

***Mume, baba, babu na rafiki mpendwa.***

Misa ya Kumbukumbu itafanyika **Jumamosi 7 Desemba 2019,** saa 4 asubuhi katika Kanisa la Mtakatifu Petro, Oysterbay, DSM ikifuatiwa na sala fupi ya kubariki kaburi la marehemu katika Makaburi ya Kinondoni.

Familia inatoa shukrani za dhati kwa ndugu, jamaa na marafiki kwa upendo na ukarimu mkubwa mlioionyesha toka kifo cha mpendwa wetu hadi sasa. Mwenyezi Mungu awabariki na kuwazidishia vyote mlivyo toa.

***Bwana ni nuru yangu na wokovu wangu, ni mwogope nani?***

***Bwana ni ngome ya uzima wangu, nimhofu nani? – Zaburi 27:1***

115534402

RIPOTI MAALUM - 3



Baadhi ya wakazi wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro wakiwa kwenye mkutano na viongozi wa Wizara ya Maliasili na Utalii (hawapo pichani) hivi karibuni. Idadi ya wakazi ndani ya mamlaka hiyo iliongezeka kutoka 8,000 mwaka 1959 hadi 90,000 mwaka 2016.

# ONGEZEKO LA WATU LINAVYOIWEKA SEKTA UHIFADHI, UTALII NJIA PANDA

## ■Hali hifadhini yashtua wataalamu

**Na Sanula Athanas**

KATIKA sehemu ya pili ya ripoti hii jana, ilielezwa nafasi ya utalii na uhifadhi katika uchumi wa taifa. Pia ikaelezwa hatari inayolikabili taifa dhidi ya usimamizi wenye mwelekeo unaokinzana na ustawi wa sekta hiyo. Endelea na sehemu ya mwisho kupata ushuhuda wa mustakabali wake:

---Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu ya Mwaka 1992 inagusa moja kwa moja uhifadhi na utalii. Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, anakiri kasi ya ongezeko la watu nchini imekuwa kikwazo katika harakati za taifa kupunguza umaskini na kuimarisha utoaji wa huduma.

Katika wasilisho lake bungeni mwaka juzi kuhusu Taarifa ya Hali ya Uchumi Mwaka 2016 na Mpango wa Maendeleo ya Taifa Mwaka 2017/18, alisema Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, waziri huyo ilionesha wastani wa ongezeko la watu kitaifa ni la asilimia 2.7 kwa mwaka, hivyo kufikia mwaka 2016, nchi ilikadiriwa kuwa na watu milioni 48.7.

Mchumi huyo alisema kwa makadirio hayo, Tanzania ni nchi ya tano kwa idadi kubwa ya watu Afrika, ikitanguliwa na Nigeria, Ethiopia, Misri na DRC.

"Idadi kubwa ya watu na kasi ya ongezeko imekuwa tatizo kubwa katika harakati za kupunguza umaskini na kuimarisha utoaji wa huduma," Dk. Mpango alisema na kuongeza kuwa serikali imeendelea kuongeza na kuimarisha upatikanaji wa elimu ya msingi, hususani kwa wasichana.

Pia mwaka huo huo, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, akaliambia Bunge kuwa kasi ya ongezeko la watu nchini ni zao la elimu duni katika masuala ya uzazi.

"Utafiti unaonesha kinamama wenye elimu ya sekondari na kuendelea, huzaa watoto wachache zaidi ikilinganishwa na wanawake wasiokuwa na elimu," Dk. Kijaji alifafanua.

Alisema Tanzania ina Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu iliyoridhiwa mwaka 1992, kwa lengo la kupunguza kasi ya ongezeko la watu ili iendane na huduma za jamii zilizopo, dhana inayosisitizwa na Rais mstaafu Mkapa.

"Mambo yaliyobainishwa katika sera hiyo ni namna serikali ilivyojipanga kutoa elimu ya msingi na sekondari, usawa kijinsia, umri wa kuolewa, matumizi ya njia za kisasa za uzazi na wajibu wa kila mdau tukiwamo sisi (wabunge)," alisema.

Akirejea Utafiti wa Afya ya Mama na Mtoto wa mwaka 2015/2016, Dk. Kijaji alisema msichana anapokaa shuleni kwa muda mrefu, vivyo hivyo uwezekano wa kuzaa watoto wengi unapungua, kwa sababu anakuwa amejitambua na kiuchumi anaboreka.

**KINACHOJIRI HIFADHINI**

Wizara ya Maliasili na Utalii, pia Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), wanabainisha ongezeko la wakazi ndani ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ni chanzo cha magonjwa mapya yatokanayo na mwingiliano kati ya binadamu, wanyamapori na mifugo.

Hifadhi hiyo ilianzishwa mwaka 1959 baada ya wakoloni wa Kiingereza kumega eneo la Hifadhi ya Taifa ya Serengeti ili kupata eneo la kuwahamishia wafugaji wa Kimaasai waliokuwa Serengeti na ikaundiwa mamlaka rasmi ya kuisimamia.

Miaka 20 baadaye (1979), Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (Unesco) liliitangaza Ngorongoro kuwa sehemu ya linachokiita 'Urithi wa Dunia'.

Aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Prof. Jumanne Maghembe, katika wasilisho la makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka 2017/18 mjini Dodoma, alisema idadi ya watu ndani ya hifadhi hiyo iliongezeka kutoka 8,000 mwaka 1959 hadi 90,000 mwaka 2016.

Ripoti ya CAG kuhusu mashirika ya umma kwa mwaka 2015/16, inabainisha kuwa mwaka 1959 wakati Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro inapoanzishwa, wakazi asili ndani ya mamlaka hiyo walikuwa hawazidi 20,000 wakiwa na mifugo yao na hapakuwapo nyumba za kudumu.

Kwa mujibu wa Prof. Maghembe, hadi kufikia mwaka 2016, tayari kuliwapo makazi mengi ya kudumu, lakini eneo halisi la mamlaka likibaki kuwa kilometa za mraba 8,292.

Pia Ripoti ya CAG inabainisha Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 ilionesha hifadhi kuwa na wakazi 80,000, wanaongezeka kwa wastani wa asilimia nne kila mwaka, ambayo ni tishio kwa mfumo wa ikolojia hifadhini.

Shirika la Umoja wa Mataifa Linaloshughulikia Idadi ya Watu (UNFPA), kupitia ripoti yake ya Septemba mwaka huu, lilionesha tafsiri ya uwiano nchini, kwamba kuna wastani wa vizazi 37 na vifo saba katika kila watu 1,000.

Hiyo inatoa tafsiri kwamba Ngorongoro iliyokadiriwa kuwa na wakazi 90,000 mwaka 2016, itakuwa na wakazi 136,620 ifikapo mwaka 2030.

Katika ripoti yake, CAG anabainisha kwamba hifadhi hiyo ina makazi ya kudumu yaliyoandikishwa yenye nyumba za kisasa na baadhi ya vijiji vina hadhi ya miji.

Mkaguzi anarejea mwaka 1976, Kata ya Ngorongoro iliyokuwa na vijiji vinne lakini hadi kufikia mwaka 2016, ilishakuwa na vijiji 36 vilivyounda kata 13. Ina maana kuna ongezeko la kata 12 ndani ya miaka 40.

"Makazi haya yanahitaji miundombinu na huduma zote za kijamii kama vile shule na vituo vya afya," CAG anasema kupitia ripoti yake hiyo.

Anautaja mtihani mwingine uliopo kupitia hamasa ya kiuchumi anayoeleza: "Hakuna vigezo vilivyowekwa ili mtu kujiunga na jamii ya ufugaji. Hali hii inahamasisha watu wengi kuhamia katika eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, hivyo mamlaka inaweza kupokea watu wengi zaidi na hatimaye kusababisha migogoro mingi ya ardhi.

"Pia hali hii inaweka ugumu wa jinsi ya kufanya shughuli za kuhifadhi maliasili iliyopo katika hifadhi, kulinda maslahi ya wakazi wa asili na kukuza utalii."

Ushauri wa CAG kwa menejimenti ya hifadhi ni kuwa na mpango wa matumizi ya ardhi yanayohakikisha hatua zinachukuliwa dhidi ya ongezeko la makazi na shughuli za kibinadamu, ambazo kimsingi ni sumu kwa maendeleo ya hifadhi.

Kwenye Hifadhi ya Taifa Serengeti iliyoanzishwa mwaka 1951, ikiwa na ukubwa wa kilomita za mraba 14,763, nako kumebainika tatizo la watu kuvamia mapori yanayoizunguka ambayo ni Loliondo, Grumeti na Maswa.

Hifadhi hiyo pia inazungukwa na maeneo ya wazi ya Ikona na Makao, ambayo sasa yamevamiwa na kuathiri mapito ya wanyamapori.

Kwa mujibu wa Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori (Tawiri), uvamizi wa maeneo hayo umesababisha wanyamapori kuuawa, kuongezeka kwa uwindaji haramu na kusambaa kwa magonjwa ya wanyamapori kwenda kwa wanyama wa kufugwa na kinyume chake.

**SHIDA KUU ILIKO**

Kamishna Msaidizi Mwandamizi Masuala ya Elimu kwa Umma wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (Tawa), Twaha Twaibu, anasema Pori la Akiba Maswa liko katika hali mbaya kutokana na uvamizi.

Anasema hali hiyo pia imeyakumba maeneo mengine ya hifadhi, akilitaja Pori la Akiba Selous kuwa ni miongoni mwa maeneo ya hifadhi ambayo watu wanazidi kuweka makazi.

"Watu wanapokuwa wengi karibu na maeneo ya hifadhi, ujangili unaongezeka kwa sababu wanapokosa kitoweo, matokeo yake ni kuwinda wanyamapori.

"Watu wanapoongezeka, ardhi haiwezi kuwatosheleza kwa makazi na shughuli za maendeleo. Wanapokosa maeneo ya malisho ya mifugo yao, wanaingiza mifugo hifadhini kinyume cha Sheria ya Wanyamapori.

"Kwa kifupi, ongezeko la watu lina faida katika kupata nguvu kazi na soko la bidhaa, lakini sisi wahifadhi tunaliona ni tatizo kwa uhifadhi," Kamishna Twaibu anasema.

Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Mawasiliano wa Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa), Pascal Shelutete, anataja mkakati wao ni shirika kushirikiana na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, kusimamia matumizi bora ya ardhi nchini.

**KAULI YA WAZIRI**

Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamis Kigwangalla, anasema serikali imeshachukua tahadhari ya ongezeko la watu na anataja mikakati iliyopo kwa hifadhi za taifa na maeneo tengefu kuwekwa ulinzi maalum.

Anakiri kuwapo kwa hatari dhidi ya ustawi wa uhifadhi na utalii kutokana na tishio la ongezeko la watu, akidokeza wastani wa makadirio ya sasa ni kati ya milioni 50 na 60.

"Sasa, kwa kuzingatia hilo, ni lazima tulinde hifadhi zetu ili ziendelee kuchangia uchumi wa nchi kwa kuingiza fedha za kigeni, hifadhi zetu pia ni chanzo cha hewa muhimu kwa maana ya oksijeni, maji na hata mbao.

"Tuhakikishe usalama wa taifa letu unakuwapo na jambo hili sharti tuliwekee mikakati leo maana Tanzania bila hifadhi, haiwezi kuwa na hadhi iliyonayo kwa sasa kiuchumi.

"Tusiangalie maslahi yetu tu sisi tuliopo kwa sasa, tuache ubinafsi, tuchukue hatua kwa pamoja kuhakikisha hifadhi zetu zinaendelea kuwapo kwa maslahi ya kizazi cha sasa na kijacho," Dk. Kigwangalla anasema.

# WB, serikali wajitosa mapinduzi vyuo ufundi

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI kwa kushirikiana na Benki ya Dunia, wanatekeleza mradi wa kuleta mapinduzi kwenye elimu ya ufundi Afrika Mashariki (EASTRIP).

Akizungumzia mradi huo Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Ufundi, Dk. Leornad Akwilapo, alisema benki hiyo imetoa Dola za Marekani milioni 75 (sawa na Sh. bilioni 172.4) kwa ajili ya kutekeleza mradi huo katika vyuo vinne nchini ambavyo ni Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam (DIT) kampasi ya Dar es Salaam na Mwanza na Chuo cha Ufundi Arusha (ATC).

"Fedha hizi zinatolewa na Benki ya Dunia kwa ajili ya kuvijengea vyuo vya hivyo uwezo ili kutoa wanafunzi wenye ujuzi stahiki wa kuwawezesha kujiajiri ama kuajiriwa na pamoja na kuvijengea vitu vya umahiri," alisema Dk. Akwilapo aliyemwakilisha Waziri wa wizara hiyo, Prof. Joyce Ndalichako.

**"Fedha hizi zinatolewa na Benki ya Dunia kwa ajili ya kuvijengea vyuo vya hivyo uwezo ili kutoa wanafunzi wenye ujuzi stahiki wa kuwawezesha kujiajiri ama kuajiriwa na pamoja na kuvijengea vitu vya umahiri," alisema Dk. Akwilapo aliyemwakilisha Waziri wa wizara hiyo, Prof. Joyce Ndalichako.**

Kwa mujibu wa Katibu Mkuu huyo, mradi huo utawezesha kujenga miundombinu bora na kuweka vifaa pamoja na kuwajengea uwezo wakufunzi.

Aidha, Dk. Akwilapo aliwataka Watanzania kufahamu kuwa elimu ya ufundi ni muhimu kwa maendeleo ya nchi hasa katika uchumi wa viwanda, na kwamba vyuo vya ufundi visiwe chaguo la mwisho kwa mtu anayefeli.

"Tunaishukuru Benki ya Dunia kwa maana fedha hizo zitatumika katika kuhakikisha wanawajengea uwezo wanafunzi na wanapohitimu inakuwa rahisi kuajiriwa viwandani na hasa ikizingatiwa Tanzania inaelekea katika uchumi wa viwanda kwa sasa."

Naye, Mratibu wa Mradi huo kutoka Wizara hiyo, Dk. Noel Mbonde, alisema vyuo hivyo vinne vimejikita katika masuala ya Teknolojia ya Habari (Tehama), gesi asilia, ngozi na masuala ya anga, na mradi huo unakwenda kuongeza udahili wa wanafunzi katika fani hizo NIT pamoja na ununuzi wa ndege ya mafunzo.

Naye, Mhadhiri wa DIT kampasi ya Dar es Salaam, Dk. Joseph Matiko, alisema fedha hizo ni kwa ajili ya kujenga miundombinu itakayoendana na kasi ya ukuaji wa TEHAMA chuoni hapo.

Alisema baada ya kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu, chuo kitakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 3,500 kutoka Afrika Mashariki.

Mwakilishi kutoka Kenya, Nelson Gitau, alisema mradi huo kwao utahakikisha elimu ya ufundi inakua, na kwamba kijana akitoka chuoni aweze kuingia moja kwa moja na kufanya kazi viwandani na hata kujiajiri mwenyewe.

Naye, Mkuu wa kitengo cha Elimu kutoka Benki ya Dunia, Dk. Xiaoyan Liang, alisema lengo la kufadhili mradi huo ni kuhakikisha unawajengea uwezo vijana na kuzifanya nchi zinazotekeleza mradi huo zinakuwa na uchumi imara kupitia viwanda.

Mkutano huo wa siku nne unahusisha washiriki kutoka Kenya, Tanzania na Ethiopia ambazo zinatekeleza awamu ya kwanza ya mradi na unaratibiwa na Shirikisho la Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki, Benki ya Dunia na Wizara ya Elimu.

# Karani wa mahakama kizimbani madai ya rushwa

**Na Hellen Mwango**

**Hakimu Mbando alisema mshtakiwa anatakiwa kuwa na mdhamini mmoja mwenye vitambulisho vinavyotambulika na atasaini hati ya dhamana ya Sh. milioni tano.**

KARANI wa Mahakama ya Wilaya ya Temeke, Itialy Omary, amefikishwa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam kwa madai ya kuomba rushwa ya Sh. 200,000.

Mshtakiwa huyo alisomewa mashtaka yake mbele ya Hakimu Mkazi Agustina Mmbando.

Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Odessa Horombe, alidai kuwa mshtakiwa huyo anakabiliwa na shtaka la kupokea rushwa kinyume cha sheria.

Horombe alidai kuwa Aprili 27, 2018 katika viunga vya Mahakama ya Wilaya ya Temeke, mshtakiwa aliomba rushwa ya Sh. 200,000 kutoka kwa Musa Abdallah, ikiwa ni kishawishi cha kumsaidia kukwepa hatia dhidi ya shtaka lililokuwa linamkabili kesi namba 211/2018 ya usalama barabarani iliyopo mahakamani hapo.

Mshtakiwa huyo alikana mashtaka hayo. Horombe alidai kuwa upelelezi umekamilika na kuiomba mahakama ipange tarehe nyingine kwa ajili ya kumsomea maelezo ya awali.

Hakimu Mbando alisema mshtakiwa anatakiwa kuwa na mdhamini mmoja mwenye vitambulisho vinavyotambulika na atasaini hati ya dhamana ya Sh. milioni tano.

Alisema kesi hiyo itasikilizwa maelezo ya awali Novemba 28, mwaka huu.

Mshtakiwa alitimiza masharti hayo na yupo nje kwa dhamana.


NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO LTD

N A M

Property Management, General Auction Services, Debt Collection, Court Broker, Advertising & Commission Agency

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa Idhini tuliyopewa na **EFC TANZANIA MICROFINANCE BANK LTD, MAKAO MAKUU – DAR ES SALAAM,** tunatoa notisi ya siku kumi na nne (14) kuanzia Tarehe ya tangazo hili kwa wadaiwa wanaotajwa hapa chini walipe madeni wanayodaiwa.

Kushindwa kulipa kwa muda huo, tutalazimika kuuza dhamana (mali) zao kwa mnada wa hadhara.

| sn | Name of Client | Collateral Details |
|---|---|---|
| 1 | Matilda Japhet Zellah | Mortgage Over Residential License No. TMK006424, Parcel No. TMK/CHB/KIM2/213 Located at Charambe, Kimbangulile Temeke in the Name of Rashid Abdalah Amuri<br>Transfer Ownership House located at Tabata Segerea Ilala Owned by Matilda Japhet Zellah |
| 2 | Catherine Albert Mshatta | Transfer Ownership of the House Located at Mwembe Bamia, Occupied by Catherine Albert Mshatta. |
| 3 | Regina B Itala | Mortgage Residential License No. ILA012456, Parcel No. ILA/UKG/MZZ37/63, Located at Ukonga, Occupied by Joseph Asuke Kasera and Regina Boniface Joseph. |
| 4 | Halima Hamza Omary | Transfer Ownership House Located at Temboni Mbezi in Ubungo Municipality in the name of Halima Hamza Omari. |
| 5 | Athumani H Mahimbo | Mortgage Over Residential License No. KND013438, Parcel No. KND/KWE/KMZ39/163, Located at Kawe Mzimuni, Kinondoni in the name of Athumani Hassan Mahimbo, of Dar es salaam. |
| 6 | Sunrise Communications Company Limited | Mortgage over Residential License No. ILA028656, Parcel No. ILA/UKG/MBK33/14, Located at Ukonga markazi Ilala, in the name of Consolata Thomas Makoba. |
| 7 | Mwema Khamis Mwamvura | Legal Mortgage Over Certificate of Title No. 142739 L. O No. 628720 on Plot No. 94 Block "H", Chekeni Mwasonga Area, Temeke Municipality in the name of Mwema Khamis Mwavura of P.O.Box No. 15785, Dar es salaam.<br>Legal Mortgage over Certificate of Title No. 153949, L.O. No717349, Located On Plot No, 179, Block "K", Mbutu Area in Temeke Municipality in the name of Ally Yussuf Marsha of P.O. Box No . 4843, Dar es salaam. |
| 8 | Akida Ramadhan Mwaimu | Legal Mortgage Over Residential License No. KND024459, Parcel No. KND/KWE/MG115/98 located at Makongo Juu, Kawe in Kinondoni Municipality in the name of Akida Ramadhani Mwaimu Of Dar es salaam. |
| 9 | Everada M Ndugumchana | Transfer Ownership of the House Located at Njeteni Street, Mbezi Luis, Ubungo Municipality, in the name of Evarada Mathew Ndugumchan of P.O. Box 90426 Dar es salaam. |
| 10 | Joshua M Kiyeyeu | Transfer of Ownership House Located at Kibaga, Kinyerezi – Ilala Municipality Owned by Joshua Mei Kiyeyeu. |
| 11 | Rahel Stephano Mjengi | Transfer Ownership House Located at Mzinga, Mzinga Ward Ilala Municipality in the name of Godfrey Emanuel Shilla and Rahel Stephano Mjengi. |
| 12 | Kitwana Twalib Jongo | Mortgage Tittle No. 140995, Plot No. 49, Block 10 at Mabwepande Occupied by Kitwana Twalib Jongo.<br>Chattels Mortgage on DAF T513CUR, Model No,FIAT CF75.310 Body Type Tractor Colour Blue, Year of Manufacture 2001, Chassis No.XLRTE75PCOE561567,Engine No.S10877 Owned By Twalib Transport<br>Chattels Mortgage on TOYOTA NOAH T667 DCU, Model No. E-SR40G,Colour White, Year Of Manufacture 1998,Chasis No.SR400118746,Engine No.3S5041591 Owned By Kitwana Twalib Jongo. |
| 13 | Fatuma Abdul Chimu | Mortgage Residential Licence No. ILA029169, Parcel No. ILA/KTD/KTK53/65A, Occupied by Chimu Hassan Chimu |
| 14 | Emmanuel J Tesha | Legal Mortgage over Certificate of Title No 145135, L.O No 279596, Located on Plot No. 214, Block 21, Buyuni in Ilala Municipality in the name of Emmanuel Jorginder and Rosemary Jorginder of P. O Box 12057, Dar es salaam. |
| 15 | Augustine Mark Macheye | Transfer Ownership of House Located at Zavara, Chanika Buyuni in Ilala Municipality in the name of Augustine M Macheye. |
| 16 | Prisca Ernet Byekwaso | Mortgage Residential Licence No. TMK041003, Parcel No. TMK/CHB/NZSA16/243, Located at Charambe, Occupied by Prisca Ernest Byekweso. |
| 17 | Rehema M Mwaruka | Tranfer Ownership of the House located at Kivule Majohe, Occupied by Muharami Athuman Seseme. |
| 18 | Swisy Investment Limited | Vehicle Mitsubish Fuso with registration No T952 ASM with chassis no FK617J510111 in the name of Swisy Investment Limited<br>Legal Mortgage Over Certificate of Title No. 60757, L.O No. 214100, located on Plot No. 140, Block 9, Tuangoma Area in Temeke Municipality, In the name of Pembe Chuma Pembe of P.O. Box 45085, Dar es salaam. |
| 19 | Michael C Kemege | Transfer Ownership House located at Viwege Majohe, Occupied by Michael Chacha Kemege. |
| 20 | Boniface Pius Rugakingira | Legal Mortgage over Residential Licence No. TMK018605, Parcel No. TMK/TDK/KLH1/211 Located at Kilimahewa Street, Tandika , Temeke Municipality, In the name of Boniface Pius Rugakingira. |
| 21 | Yusuf Salum Kalyanye | MortgageCertificate Of Occupancy Title No. 79948, Plot No . 1141, Block C, Situated at Kizza Occupied By Yusuf Salum Kalyanye. |
| 22 | Nuru J Kidunda | Mortgage Residential Licence no KND028986,Parcel No KND/KWE/MGJ13/14, Situated at Kawe, Occupied by Oswald Kupelwa Nshiku. |
| 23 | Flora Mkway | Transfer Ownership Of House Located at Kipawa Uwanja Wa Ndege, Occupied By Flora Anderson Mkway. |
| 24 | Benedict Chengula | Transfer Ownership House Located at Goba, Matosa - Kinondoni Owned by Benedict Chengula |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hiyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

**Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:**
**Mkurugezi Mtendaji**
**NUTMEG Auctioneers**
**Mkwepu Street**
**Ami Buliding, 3rd Floor.**
**P.O. BOX 6201**
**DAR ES SALAAM**
**MOBILE + 255 -754 497396/0752000695**

**AU**

**Mkurugezi Mtendaji**
**EFC Microfinance Bank**
**Tanzanite Park,**
**38 New Bagamoyo Road,**
**P.O. BOX 11735**
**DAR ES SALAAM**
**Tel: +255-22 2760211/12**

215533101

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Mradi huu utawakomboa wahitimu wa elimu ufundi*

**KUNA** taarifa njema zinazoeleza kuwa setikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Benki ya Dunia, wanatekeleza mradi wa kuleta mapinduzi kwenye elimu ya ufundi Afrika Mashariki (EASTRIP).

Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Ufundi, Dk. Leornad Akwilapo, alisema katika utekelezaji wa mpango huo, benki hiyo imetoa Dola za Marekani milioni 75 (Sh. bilioni 172.4) katika vyuo vinne ambavyo ni Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam (DIT) kampasi ya Dar es Salaam na Mwanza pamoja na Chuo cha Ufundi Arusha (ATC).

Kwa mujibu wa Akwilapo, fedha hizo zinatolewa na Benki ya Dunia kwa ajili ya kuvijengea vyuo hivyo uwezo ili kutoa wanafunzi wenye ujuzi stahiki wa kuwawezesha kujiajiri ama kuajiriwa na pamoja na kuvijengea vitu vya umahiri.

Katibu Mkuu huyo, aliyemwakilisha Waziri wa wizara hiyo, Prof. Joyce Ndalichako, alisema mradi huo utawezesha kujenga miundombinu bora na kuweka vifaa pamoja na kuwajengea uwezo wakufunzi.

Aliwataka Watanzania kufahamu kuwa elimu ya ufundi ni muhimu kwa maendeleo ya nchi hasa katika uchumi wa viwanda, na kwamba vyuo vya ufundi visiwe chaguo la mwisho kwa mtu anayefeli.

Kwamba fedha hizo zitatumika katika kuhakikisha wanawajengea uwezo wanafunzi na wanapohitimu inakuwa rahisi kuajiriwa viwandani na hasa ikizingatiwa Tanzania inaelekea katika uchumi wa viwanda.

Mpango huo tunaona ni mzuri na utakuwa na manufaa kwa nchi yetu ambayo ajira kwa vijana imekuwa moja ya changamoto kubwa kutokana na serikali kutokuwa na uwezo wa kuajiri wahitimu wengi wanaotoka kwenye vyi vikuu na vya kati.

Hatua ya kuwezesha vyuo vya elimu ya ufundi bila shaka itajaribu kupunguza mahaki ya ajira, kwa sababu vyuo hivyo vitasaidia kuzalisha vijana ambao wakishahitimu hawatahangaika kutegemea kuajiriwa na serikali bali watajiongeza kwa kujiajiri wenyewe.

Ni wakati mwafaka sasa kwa vijana wetu wanaosoma elimu ya ufundi kwenye vyuo tajwa kuuchukulia mradi huu kama fursa adhimu ya kujiletea maendeleo.

Fursa nyingi zipo kwenye kozi wanazochukua kwa sababu kwa mujibu wa Mratibu wa Mradi huo kutoka Wizara hiyo, Dk. Noel Mbonde, vyuo hivyo vinne vimejikita katika masuala ya Teknolojia ya Habari (Tehama), gesi asilia, ngozi na masuala ya anga.

Jambo la msingi ni kuwa wahusika; kwa maana ya watekelezaji wa mradi wahakikishe kuwa fedha zinazotolewa na Benki ya Dunia zinatumika kwa mujibu wa malengo, na kwa kufanya hivyo kutawajengea imani ya kuendelea kusaidia.

Lakini pia serikali yetu iendelee kubuni na kutekeleza miradi mingine ya kuvipatia uwezo zaidi vyuo vya ufundi hususan na ufundi stadi vilivyoko chini ya Mamlaka ya Ufundi Stadi (VETA) ili wahitimu wake wamudu ushindani katika soko la ajira na wakati huohuo kujiajiri wenyewe.

Ikumbukwe kwamba wakati huu ambao Tanzania imepania kuingia katika uchumi wa kati kupitia ujenzi wa viwanda ifikapo mwaka 2025, viwanda vitakavyoanzishwa vitawahitaji wataalamu hao na wengine wanakuwa na fursa ya kuanzisha viwanda vyao vidogo.

Hatua ya msingi kwa wizara husika ni kubuni mikakati ya kuzalisha wahitimu bora katika vyuo vya ufundi ngazi zote, Pia serikali itenge fedha zaidi kwa ajili ya kuviwezesha vyuo hivyo.

Bila kufanya jitihada hizi, tunaweza kujikuta bila kuwa na hata mafundi mchundo kwenye viwanda vitakavyojengwa, hivyo kutegemea wa kutoka nje ya nchi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Elizabeth Zaya

# Uchaguzi mitaa wananchi wanahitaji kuujua ukweli

**UCHAGUZI** wa serikali za mitaa umemalizika huku Chama Cha Mapinduzi(CCM) kikishinda vijiji 12,260 sawa na asilimia 99.9.

Chama hicho pia kimeshinda katika mitaa 4,263 sawa na asilimia 100 katika matokeo ya jumla na katika nafasi ya mwenyekiti kimeshinda vitongoji 63,970 sawa na asilimia 99.4, kwa mujibu wa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa (Tamesemi), Selemani Jafo, ambaye wizara yake ndiyo yenye dhamana ya kusimamia uchaguzi.

Baadhi ya vyama vya upinzani ambavyo vilikuwa vimetangaza kutokushiriki katika uchaguzi huo navyo vilipigiwa kura kikiwamo chama kikuu cha upinzani, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Chama cha Wananchi(CUF) na ACT-Wazalendo.

Japokuwa vilitangaza kujiondoa lakini nembo za vyama vyao vilionekana katika karatasi za kupigia kura na hivyo wananchi wakatekeleza wajibu wao kwa kuwapa kura.

Vyama hivyo vilitangaza kujiweka pembeni katika uchaguzi huo kwa madai ya kutoridhishwa na mchakato mzima wa kukubalika kwa uteuzi wa wagombea wake, vikilalamika kutokuteuliwa kwa wagombea wake bila kuwapo na sababu za msingi.

Kwa mujibu wa matokeo yaliyotangazwa juzi na Waziri Jafo, vyama hivyo navyo vilipigiwa kura, ambapo Chadema na CUF vilipata ushindi katika kijiji kimoja kimoja na katika nafasi ya wenyekiti ACT-Wazalendo nacho kilishinda kitongoji kimoja.

Jafo alisema jumla ya nafasi zilizogombaniwa ni 332,160 ambazo zote zilihusisha katika uchaguzi wa vijiji 12,262, mitaa 4,263, vitongoji 63,992, wajumbe kundi la wanawake 106,622 na wajumbe kundi la mchanganyiko 145,021.

Katika nafasi ya wenyeviti, Chadema ilishinda nafasi moja ya wenyeviti wa vitongoji(19), kundi la wanawake(39), wajumbe kundi la mchanganyiko (71), huku CUF nayo ikipata nafasi moja ya kijiji, vitongoji viwili, wajumbe kundi la wanawake nafasi tatu na wajumbe kundi la mchanganyiko nafasi 14.

Baada ya matokeo hayo kutangazwa, baadhi ya vyama hivyo ambavyo vilikuwa vimetangaza kujitoa katika uchaguzi huo vilikuja juu kwa nembo yao kutumika katika uchaguzi.

Miongoni mwa vyama vilivyolalamika ni pamoja na CUF, Chadema, na ACT-Wazalendo.

Mkurugenzi wa Habari na Mawasiliano wa CUF, Abdul Kambaya, anasema wanashangaa nembo ya chama chao kutumika katika uchaguzi huo wakati walijitoa na kwamba msimamo wa chama hicho bado uko pale pale kwamba hawakushiriki katika uchaguzi huo.

Chama cha ACT-Wazalendo nacho kupitia Katibu Mwenezi, Ado Shaibu, kinasema msimamo wa chama hicho haujabadilika na kwamba walisikitishwa na nembo ya chama chao kutumika katika uchaguzi huo

Mkurugenzi wa Itikadi, Uenezi na Mambo ya Nje wa Chadema, John Mrema, anasema wanakusanya vielelezo na watatoa ushahidi kwa halmashauri zote zilizokiuka agizo la chama hicho.

Kwa yote haya yaliyotokea katika uchaguzi huu wa serikali za mitaa uliomalizika juzi, kuna jambo la kujifunza ili kuhakikisha kwamba katika uchaguzi ujao kusitokee tena kama yalivyojiri safari hii.

Funzo hilo linapaswa liwe kwa makundi mbalimbali ikiwamo kwa vyama vya siasa vyenyewe, mamlaka husika zinazohusika na masuala ya uchaguzi, viongozi wanaosimamia mchakato mzima wa uchaguzi huo.

Wahusika wajiulize kama kuna mahali wasimamizi au mamlaka na uchaguzi zilifanya makosa na kusababisha kutokea upungufu wajirekebishe, wakae chini na kuzitafutia ufumbuzi changamoto zilizojitokeza na kutoa maelezo kwa wananchi.

Kabla ya baadhi ya vyama hivyo kujitoa katika uchaguzi huo, yapo maandalizi ambayo wagombea wa vyama hivyo walikuwa wamejipanga kabla ya kutangaziwa kwamba wasishiriki kutoka kwa viongozi wao wakuu.

Na kwa kuwa ilikuwa ni agizo au amri kutoka kwa viongozi wao, kwa kupenda au kutokupenda walikubali kutoshiriki, lakini je, waliridhika na uamuzi huo?

Ni vema mambo haya yakatazamwa kwa undani na kuyatenda kwa haki bila kuathiri upande wowote au kuumiza mtu hasa katika uchaguzi mwingine unaokuja viongozi wawashirikishe wananchi wasiamue kufanya kila wanachoona kinawafurahisha.

MAKALA MAALUM

# Miaka mitatu Benki Kilimo 'kifua mbele'

**Na Mwandishi Wetu**

UNAIJUA Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB), sababu ya kuanzishwa kwake na inafanya nini hadi sasa? Japhet Justine, Mkurugenzi Mtendaji wa asasi hiyo ana ufafanuzi uliojitosheleza kupitia mazungumzo yake, alipohojiwa na kituo cha televisheni cha ITV jana.

Anaanza na historia kwamba ilianzishwa mwaka 2015 kama 'benki ya kisera' lengo ni kuboresha, kuendeleza kilimo na kuhamasisha taasisi nyingine za fedha kutoa mikopo inayochangia ukuaji sekta ya kilimo na ustawi wa wakulima. Hata hivyo, ilianza kutoa mikopo mwaka juzi.

Mtazamo mkuu kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, ni kusaidia usalama wa chakula endelevu nchini, ikihamasisha mapinduzi ya sekta ya kilimo, kutoka ulimaji wa kujikimu hadi kibiashara, inayoishia kukweza uchumi wa nchi na kupunguza umasikini.

Justine anafafanua msamiati wa jina la asasi hiyo 'Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania' na sio 'Benki ya Kilimo' pekee, akimaaminisha: "Jina lake linaakisi upana wa wigo wa shughuli zake. TADB haitoi tu mikopo, inawekeza pia katika stadi na tafiti zenye malengo ya kuendeleza minyororo ya thamani ya mazao ya kilimo,"

Anafafanua kwamba, benki hiyo inashauri maendeleo ya kisera katika kilimo na masharti yake kifedha, tofauti na benki nyinginezo, kwa manaa imeanzishwa kimkakati kutimiza malengo, ikiwamo kutoa mikopo ya muda mrefu na kati.

"TADB inatoa mikopo hadi miaka 15. Hii inatuwezesha kutoa mikopo ya miradi mikubwa na endelevu," anasema Justine na kuongeza haipokei wala kuweka amana na mtaji wake haupungui Sh. bilioni 50, ikitoa riba ndogo kwa wakopaji .

Anasema, mkopaji hupewa muda kuanza kurejesha hadi miaka mwili. Ni miradi inayotakiwa kuigusa jamii jirani kwa matokeo chanya kwao,

"Iwapo tutakutengenezea mfumo wa umwagiliaji, utuonyeshe ni namna gani wakulima wanaokuzunguka watafaidika na huo mradi wa umwagiliaji. Kama una kiwanda cha kuchinja ng'ombe, basi wafugaji wanaokuzunguka wafaidike na kiwanda chako," anaeleza Justine.

**MAGEUZI & WATEJA**

Justine anawataja wateja wake, akirejea tafsiri kutoka Shirika la Chakula Duniani (FAO), kwamba inagusa mazao, uvuvi, kilimo, maziwa na misitu.

"Kwa sasa, TADB tumejikita katika maeneo ya kwanza matatu Kilimo cha mazao, Uvuvi na Ufugaji. Misitu itakuwa sehemu ya wateja wetu siku za mbeleni," anasema na anafafanua:

"Unaweza kusema walengwa wakulima wa Tanzania wanaojihusisha na shughuli halali za kiuchumi zitokanazo na sekta ndogo ya kilimo, mifugo, uvuvi na misitu."

Kuhusu hatua za mafanikio tangu kuanzishwa, anazitaja ni kusaidia kubadilisha mtazamo kutoka kilimo kuwa shughuli ya kubahatisha na kimasikini, hadi kuonekana kazi kamili.

Pia, anasema TADB imefanikiwa kushawishi benki nyingine na wadau wa sekta ya fedha kuvutiwa kukipa kilimo umuhimu na kuelekezea fedha zaidi.

Anasema, hadi mwezi uliopita kuna mikopo ya Sh. bilioni 147.02, ikiwa ongezeko la Sh. bilioni 62.46 katika kipindi cha miezi tisa tangu Desemba mwaka jana.

PROGRAMU KILIMO

Justine anasema, TADB katika utekelezaji wa Program ya Pili ya maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDPII), ina nafasi gani inafanya kazi ya kuchochea kupitia mikopo na kufadhili stadi na miradi, ikiwamo ushiriki wa sekta binafsi.

"Pia tunafanya uchechemuzi (advocacy) kwa watunga sera na wafanya uamuzi juu ya fursa zilizopo na umuhimu wa kuondoa vikwazo ili kuwezesha malengo ya programu kufikiwa," anaeleza.

Anataja mikakati ya mikopo ni kuendeleza miundombinu ya umwagiliaji ya Sh. bilioni 17; upatikanaji pembejeo na zana za kilimo Sh. bilioni nne mwaka huu, Mwaka jana kuliwekezwa Sh. bilioni 6.6.

Katika uanzishaji viwanda vidogo vya wakulima na mtandao wa masoko ya mazao yao, inagusa wakulima 1190 kwa thamani Sh. bilioni 35.



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania, Japhet Justine (kushoto), alipozungumza jana. **PICHA: ITV.**

**UCHUMI VIWANDA**

Justine anasema, hadi sasa wameshatengeneza viwanda 12 katika kutekeleza sera ya Uchumi wa Viwanda, ikitolewa mikopo ya sh. bilioni 105.7, inagusa miradi ya uchakataji na usindikaji mazao ya mahindi, zabibu, mawese, alizeti, mpunga, maziwa na nyama.

Pia, anasema kuna mikopo ya Sh. bilioni 41 kwa ajili ya kununua na kuongeza thamani ya kahawa, mpunga na karafuu, kama ifuatavyo: Kiwanda cha kusindika mafuta alizeti iliyoko Kahama (imekamilika); mafuta ya alizeti Manyoni (kinajengwa); mafuta michikichi Kigoma; vifungashio Kahama; maziwa Njombe; na nyama Mwanza.

Vingine ni usindikaji mahindi; Arusha, Pwani, Njombe, Songwe, na Songea (Ruvuma); pia ukoboaji mpunga, Mombo (Tanga).

Katika ushirikiano wa kibenki, wameviunga mkono viwanda vinane kwa kuvifungamanisha na wakulima wanaotoa malighafi za viwanda kama soseji, mkoani Mwanza, maziwa Njombe, wakiegemea sera ya viwanda kuwezesha kuajiri wengi.

**UFANIKISHAJI MAJUKUMU**

Justine anasema, kupitia kongani na minyororo ya thamani, mikoa yote nchini imeunganishwa katika kongani nane na TADB inahudumia kupitia mawasiliano ya simu yasiyo na gharama kupitia namba maalum ya benki washirika.

"Ili kufikisha huduma karibu zaidi na wateja wake, TADB imeanzisha utaratibu wa kukopesha wa kupitia kongani na minyororo ya thamani," anasema. Mikoa nane imeunganishwa kupitia kanda zinazoendana kiikolojia, kwa kuoanisha mazao ya kipaumbele kupatiwa mikopo.

**MAFANIKIO MIAKA MINNE**

Justine anasema katika miaka mine, TADB imefufua kahawa, kupitia uwekezaji zaidi ya Sh. bilioni 39 msimu uliopita, akitoa mfano wa Kagera wakulima takribani 148,000 wamefaidika, wengine 5000 wameajiriwa, kati kinamama 1000.

Anataja siri ya kielelezo cha mfanikio ni kutolewa mkopo wa Sh. bilioni 147 na hadi sasa Sh. bilioni 43.25, zimeshaanza kurejeshwa. Anafafanua kiashiria kingine: "Kuongezeka takwimu za mikopo inayokwenda katika kilimo, mfano kwa mwaka huu kumekuwa na ongezeko la asilimia 73.86."

Mkurugenzi wa TADB, anasema hadi sasa wana ushirikiano na benki 17 za biashara, pia wakulima ili kilimo chao kiwe na tija zaidi na wadau katika kuchochea ukopeshaji katika kilimo, ikiwamo kuwa na Mfuko wa Dhamana kwa Wakulima wadogo (SCGS).

"Kwa ushirikiano huu, benki hizi zimetoa mikopo yenye jumla ya Sh. bilioni 30 kwa wanufaika zaidi ya 31,508 kwa kipindi cha mwaka moja hadi leo hii. Hizi ni pesa ambazo kama sio udhamini wa Benki ya Kilimo, benki za biashara zingeshindwa kutoa kwa kuwa wakulima wengi hawana dhamana," anasema.

"Tofauti na benki ya biashara, TADB inatoa mikopo na mazingatio mahsusi ya sekta ya kilimo na hali halisi za wakulima, ikiwamo misimu, riba na mahitaji mahsusi ya kila zao ikizingatiwa kuwa kila zao lina utofauti wake.

"Benki za biashara yanakitazama kilimo kama shughuli nyingine yoyote na hivyo masharti na huduma zake havikipi kilimo na mkulima upekee unaostahili," anasema Mkuu wa TADB, akidai benki za biashara zinaogopa athari za miradi ya kilimo

**MBINU ZA USHIRIKIANO**

Justine anataja ni kuwasaidia wakulima kupitia mafunzo ya ujasiriamali kwa katika kilimo; mfumo jumuishi unaomuingiza mkulima mdogo katika mfumo rasmi wa kifedha (financial inclusion), kujengewa uwezo pamoja na mafunzo ya utunzaji fedha.

Anataja matokeo chanya katika hilo ni kwamba wanufaika ni wakulima milioni 1.7, kati yao asilimia 30 ni wanawake.

| Na. | Kongani | Mikoa | Mazao |
|---|---|---|---|
| 1 | Kanda ya Kati | Dodoma, Manyara na Singida | Alizeti; Mahindi; Ng'ombe wa Nyama na Maziwa; Shayiri; Zabibu |
| 2 | Kanda ya Ziwa | Mwanza, Kagera, Mara, Shinyanga, Geita na Simiyu | Mihogo; Mpunga; Mikunde; Ng'ombe wa Nyama na Maziwa; Pamba; Miwa; Samaki |
| 3 | Kanda ya Kaskazini | Arusha na Kilimanjaro | Mahindi; Mbogamboga; Mikunde; Ng'ombe wa Nyama na Maziwa |
| 4 | Kanda ya Mashariki | Dar es Salaam Tanga, Pwani na Morogoro | Mihogo; Mpunga;Viungo; Mahindi; Ng'ombe wa Nyama na Maziwa; Korosho; Miwa; Samaki |
| 5 | Kanda ya Magharibi | Rukwa, Katavi, Kigoma na Tabora | Mahindi; Mpunga; Alizeti; Mikunde; Mafuta ya mawese; Ng'ombe wa Nyama; Samaki; Asali |
| 6 | Kanda ya Nyanda za Juu Kusini | Mbeya, Songwe, Iringa, Njombe, na Ruvuma | Mahindi; Mpunga; Alizeti; Mikunde; Shayiri; Ng'ombe wa Nyama na Maziwa |
| 7 | Kanda ya Kusini | Lindi na Mtwara | Mihogo; futa; Mikunde; Korosho; Samaki |
| 8 | Kanda ya Zanzibar | Unguja na Pemba | Matunda na mboga mboga; Viungo; Ng'ombe na Maziwa; Samaki |

# Madudu ya ushirika yatua Takukuru

INATOKA UK 3

Hasunga alibainisha kuwa katika vyama hivyo, 303 sawa na asilimia 6.87 vilipata hati inayoridhisha, 2,378 sawa na asilimia 53.89 vilipata hati yenye shaka.

Pia vyama 879 sawa na asilimia 19.92 vilipata hati isiyoridhisha na vyama 853 sawa na asilimia 19.32 vilipata hati mbaya.

"Ninayo orodha ya vyama vyote vyenye viashiria vya ubadhirifu, namkabidhi Mkurugenzi wa Takukuru akashughulike nao na bodi zao, akatusaidie kufuatilia fedha hizi. Tunataka fedha zao zipatikane na zirudi kwa wanachama," alisema.

**UBADHIRIFU**

Akitoa mchanganuo wa ubadhirifu huo, Waziri alisema kati ya vyama vikuu 38, vinne vilipata hati safi, vyama 22 vilipata hati yenye shaka, tisa vilipata hati isiyoridhisha na vitatu vilipata hati mbaya.

"Vyama hivyo vikuu vitatu vilivyopata hati mbaya inayohusisha hoja zenye viashiria vya ubadhirifu wenye jumla ya Sh. milioni 856.3 ni kwa Chama Kikuu cha Ushirika cha Ruangwa, Nachingwea na Liwale (Runali).

Viashiria vingine ni katika Muungano wa Vyama vya Akiba vya Kuweka na Kukopa (SCCULT) Sh. milioni 4.87 na Kyecu (Kyela) kwa kukosekana kwa hati za kuhesabu mali za kudumu mwisho wa mwaka," alisema.

Pia alisema Shirikisho la Vyama vya Ushirika (TFC) limepata hati isiyoridhisha ambayo inajumuisha fedha benki zisizofanyiwa malinganisho na pia kutooneshwa katika taarifa za Sh. bilioni 1.53.

**VYAMA VYA MSINGI**

Kuhusu vyama vya ushirika wa mazao (Amcos), Hasunga alisema kati ya vyama 2,710 vilivyokaguliwa, 15 vilipata hati safi, 1,347 hati zenye shaka, 599 hati zisizoridhisha na vyama 749 vilipata hati mbaya.

"Matatizo makuu katika vyama hivyo vya Amcos ni kushindwa kuandika vitabu vya hesabu, malipo mengi kutokuwa na vielelezo vya malipo, mifumo dhaifu ya udhibiti wa makusanyo na mauzo ya mazao, kukosekana kwa daftari la mali za vyama na watendaji wa vyama kutokuwa na weledi wa kuandika vitabu na taarifa za fedha za vyama," alisema.

**VYAMA VYA AKIBA NA MIKOPO**

Hasunga alisema kati ya vyama vya akiba na mikopo (Saccos) 1,448, Saccos 261 zilipata hati safi, 887 yenye shaka, 218 isiyoridhisha na 82 hati mbaya.

"Matatizo makuu ya Saccos nyingi ni kushindwa kuandika vitabu ipasavyo, marejesho ya mikopo ya wanachama kutofanyika kwa wakati, baadhi ya waajiri kuchelewesha kuwasilisha makato ya wanachama kwa Saccos,"alisema.

Aliongeza kuwa: "Madeni makubwa yanayothiri utendaji wa Saccos, miamala ya benki kutofanyiwa malinganisho na baadhi ya miamala kuwa na ubadhirifu."

**UBADHIRIFU WENYEWE**

Alisema katika ukaguzi wa kawaida uliofanyika kwa mwaka huo, fedha zenye mashaka ni Sh. bilioni 87.6, hasara iliyotengenezwa kwa uzembe ni Sh. bilioni 22.8 na wizi ni Sh. bilioni 2.8.

> **"Vyama hivyo vikuu vitatu vilivyopata hati mbaya inayohusisha hoja zenye viashiria vya ubadhirifu wenye jumla ya Sh. milioni 856.3 ni kwa Chama Kikuu cha Ushirika cha Ruangwa, Nachingwea na Liwale (Runali).**

Aidha alisema katika ukaguzi maalum uliofanyika fedha zenye shaka ni Sh. Bilioni 6.2, hasara iliyotengenezwa kwa uzembe ni Sh. bilioni 2.6 na wizi ni Sh. bilioni 1.7, hivyo jumla kuu ya viashiria vya ubadhirifu kuwa Sh. Bilioni 124.05.

Pia alisema vyama 682 vilikataa kuwasilisha vitabu kwa ajili ya ukaguzi na kati ya vyama 853 vyenye hati mbaya, vipo vyama vyenye viashiria vya ubadhirifu wa fedha na mali 130 na vyama vyenye matatizo mbalimbali ya uongozi na utendaji ni 723.

**KAULI YA TAKUKURU**

Akizungumza baada ya kupokea ripoti hiyo, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Takukuru, Brigedia Jenerali John Mbung'o, alisema taasisi hiyo ina mamlaka ya kushughulika na ubadhirifu wote na kuwataka wale wote waliohusika kuanza kurejesha fedha hizo kuanzia jana na hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

"Tutawachunguza na hatutaacha jiwe lolote ambalo halijageuzwa kwenye suala hili la ushirika, wachukue tahadhali mapema kuanza kurejesha fedha hizo mapema sana," alisema.

Alisema wataanza uchunguzi mara moja na pale kwenye ushahidi watapelekwa mahakamani, watashtakiwa na hata kabla ya kushtakiwa kushirikiana na Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali watapeleka maombi ya kutaifisha mali zao.

"Iwe nyumba, biashara, mifugo itataifishwa. Waanze wenyewe kurejesha fedha kabla hatua za kufuatiliwa hazijachukuliwa," alisema.

Mwenyekiti wa TFC, Dk. Titus Kamani, alisema tume itatoa ushirikiano unaostahili ili kuhakikisha hatua stahiki zinachukuliwa kwa wahusika.




# NHC yapewa siku 90

INATOKA UK 3

wana nyumba mbili au tatu kwa ujanja wao na wao wanakodisha. Tutawaondoa wapangaji hewa na tutawatambua wamiliki hewa wa nyumba zilizotaifishwa.

"Kuna watu wakihama kwenye nyumba wanaziuza kwa gharama kubwa wanachukua fedha juu ya mgongo wa shirika hili kwa sababu inaelekea hatuna utunzaji wa kisasa wa takwimu za wapangaji na nyumba."

Pia, alilitaka shirika hilo liingie kwenye utaratibu wa kidijitali kwa kuanzisha nyaraka za kieletroniki ili kutunza kumbukumbu za wapangaji.

"Taarifa hizi ziingie kwenye mfumo wa Mamlaka ya Vitambulisho Vya Taifa (Nida), wapangaji wote lazima wafanyiwe uhakiki taarifa zao zifanane na taarifa za Nida.

"Kila mpangaji anapohamia kwenye nyumba tumjue anafanya kazi wapi, jina lake kamili kama alivyojiandikisha Nida."

Alisema anawajua baadhi ya watu wanaomiliki zaidi ya nyumba moja kwa majina tofauti na wengine wanazitumia kuzikodisha huku wakiwa kwenye majengo mengine.

"Wote watambuliwe, najua kuna vishoka ambao wanaowatumia kuzikodisha, mfanye uhakiki upya wa kielektroniki. Wakati wa uhakiki hakikisheni maofisa na mameneja wa Mkoa wa Dar es Salaam wanaondolewa na kuwekwa watu wengine," alisema.

Waziri Lukuvi aliwaeleza wananchi kuwa nyumba za shirika hazitolewi kwa familia kama urithi baada ya aliyepangishwa kufariki, bali waliobaki hutakiwa kwenda NHC kwa ajili ya upangaji upya.

Akizungumzia changamoto nyingine ya muda mrefu, alisema ni ya kufanya miradi kwa ubia na watu binafsi ambayo imesababisha shirika linufaike kwa asilimia 25 pekee.

"Ipo miradi ipatayo 192 ambayo imeingia ubia kati ya NHC na watu binafsi, hapa kuna tatizo ambalo ninataka kutoa maagizo kwa bodi mpya ya shirika ipitie upya mikataba hii kwa sababu mingi haina tija ya moja kwa moja kwa shirika," alisema.

Alisema sehemu kubwa ya mikataba hiyo, shirika ilitoa ardhi yenye thamani kubwa na wajenzi wengine wametoa fedha.

"Ninajua bodi ya shirika ilisimamisha miradi michache kama 45, iliyobaki tumieni wataalam wa ndani na nje wanaoweza kukaa pamoja na wabia ili angalau serikali lipate faida. Pande zote zinufaike."

Waziri Lukuvi alisema haiwezekani shirika litoe viwanja Masaki na maeneo mengine vyenye thamani kubwa halafu liambulie asilimia 25 maisha yote.

Aliwataka wote walionunua nyumba zilizotaifishwa kuwa wamenunua mabomu na serikali itawafikia kila mmoja.

Alilitaka shirika hilo lifanye uhakiki wa majengo yote yaliyotaifishwa kwa sababu juzi walipoitembelea nyumba namba 43 iliyopo Kinondoni wameona ina mashaka.

"Nyumba hii ilitaifishwa na mwenye nyumba akarudishiwa kwa mkataba kwamba aishi hadi atakapokufa, lakini hati ibaki kwa msajili, tulipofuatilia kwa aliyeishi sasa ni raia wa Ghana na siyo wa raia wa Kihindi."

Akizungumzia wapangaji waliongia kwenye nyumba kwa kutozwa fedha na mtu wa kati au matapeli, aliwataka wamfuate na atazirejesha fedha hizo hata kama ni Sh. milioni 100 kwa sababu hawapangishi kwa fedha.

Alilitaka shirika hilo kuhakikisha hadi ifikapo mwishoni mwa Januari deni la Sh. milioni 400 ambalo serikali inalidai la kodi ya ardhi liwe limelipwa.

Pia alilitaka shirika liwape hati pacha wote walionunua vipande vya nyumba walizokuwa wanaziuza ili walipe kodi.

HABARI KITAIFA

## Mwamko wanawake kujiunga elimu ya juu wapaa

Na Idda Mushi, MOROGORO

MWAMKO wa wanawake kujiendeleza na masomo ya elimu ya juu umeendelea kushika kasi katika vyuo kikuu mbalimbali nchini, kikiwamo cha Mzumbe kwa wanawake wengi zaidi kuhitimu kozi mbalimbali mwaka huu ikilinganishwa na wanaume.

Kwenye mahafali ya 18 ya chuo hicho kampasi kuu ya Morogoro, kati ya wahitimu 2,523 wanaohitimu, 1,314 sawa na asilimia 52.1 ni wanawake, ikilinganishwa na asilimia 45.9, sawa na wahitimu 1,209.

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Mzumbe, Prof. Lughano Kusiluka, alikiri hali hiyo kuwa ya ki historia ikilinganishwa na miaka mingine idadi ya wanaohitimu kuwa ni wanaume.

Aliwapongeza wanawake wote waliojenga uthubutu na kuamua kujiendeleza na masomo ya elimu ya juu kwa kuonyesha wanaweza, tofauti na miaka ya zamani idadi ya wahitimu wanawake ilikuwa ni ndogo na vyuo mbalimbali kulazimika kuwahimiza kutumia fursa ya kujiendeleza.

Prof. Lugano alisema Chuo cha Mzumbe kina kampasi tatu za Morogoro, Dar es Salaam na Mbeya na kwamba katika mwaka wa masomo wa 2019/2020 wameshasajili jumla ya wanafunzi 4,994 wakiwamo 414 wanaochukua Astashahada, 566 Stashahada na 3,436 Shahada ya kwanza huku wanafunzi 578 wakisajiliwa kuanza masomo katika shahada za umahiri.

Hata hivyo, alisema idadi ya waliodahiliwa kwa mwaka huu ni ndogo ikilinganishwa na vijana wanaofaulu na kukidhi vigezo vya kusomea fani mbalimbali chuoni hapo na kwamba nia yao ni kuona idadi ya wadahiliwa inaongezeka mara dufu ili Watanzania wengi wapate fursa ya kujiendeleza kwa kupata elimu bora na kulisaidia taifa.

Prof. Kusiluka alisema kilichowakwamisha kuchukua wanafunzi wengi ni upungufu wa miundombinu muhimu ya kitaaluma, ingawa serikali imeendelea kufanya uwekezaji mkubwa katika kampasi zake zote ikiwamo ujenzi wa mabweni ya wanafunzi, madarasa, kumbi za mihadhara na ofisi kusaidia utoaji wa taaluma.

Kaimu Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu Mzumbe, Pius Maneno, alisema pamoja na mafanikio mbalimbali bado kuna changamoto zinazowakabili ikiwamo ukosefu wa ajira kwa vijana wanaohitimu elimu ya juu.

Maneno alishauri kuwapo kwa utafiti utakaosaidia kupata majibu ya tatizo hilo ikiwamo idadi ya ajira zinazohitajika ikilinganishwa na wahitimu katika vyuo vilivyopo, uwezo wa wahitimu kujiajiri, matumuzi ya teknolojia katika kuongeza fursa za ajira na maandalizi ya wataalamu kutoka vyuo vikuu vilivyopo nchini.

Mwaka huu, Mkuu wa Chuo Kikuu Mzumbe, Jaji mstaafu Barnabas Samatta, aliwatunuku wahitimu wa kozi mbalimbali chuoni hapo.

# Maambukizi ya ukimwi Mwanza yapanda kwa kasi

Na Elizabeth Faustine, MWANZA

MAAMBUKIZI ya virusi vya Ukimwi kwa Mkoa wa Mwanza yamepanda kutoka asilimia 4.2 mwaka 2012 hadi 7.2 mwaka 2017.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, alisema hayo wakati akifungua maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani yaliyofanyika katika Uwanja wa Rock City Mall jijini Mwanza, jana.

"Kiwango cha maambukizi kwa sasa kimekua kwa kasi sana kutoka asilimia 4.2 hadi 7.2, si jambo jema," alisema.

Alisema taarifa zinaonyesha kundi la vijana wenye umri wa miaka 15 hadi 24 ndiyo liko kwenye hatari zaidi.

Mongella alisema maeneo ya visiwani ni hatarishi kutokana na asili na shughuli inayofanyika na kuwataka Watanzania kuungana kupiga vita kwa kuchangia mfuko wa udhamini wa kudhibiti Ukimwi.

"Ukimwi sio mwisho wa maisha, hakuna sababu ya wewe kujinyanyapaa, kwanza wewe mwenyewe na pili jamii, tuondokane na huu ushamba, tuende kwenye hatua inayofuata," alisema Mongella.

Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti Ukimwi, Dk. Leornad Maboko, alisema mfuko huo umewezesha kupatikana kwa Sh. bilioni 12 kwa ajili ya shughuli ya kudhibiti Ukimwi kwa mikoa ya Kanda ya Ziwa kazi ambayo inatarajiwa kuanza mwanzoni mwa mwaka ujao.

Alitaja namba ya kuchangia mfuko huo kwa ajili ya shughuli ya kusaidia kupunguza maabukizi ya virusi vya Ukimwi kwa mtu yeyote mwenye moyo wa kuchangia kuwa ni 0684909090.

Amewasihi wananchi wa Mkoa wa Mwanza kufika kwenye mabanda kwa ajili ya kupima saratani ya shingo ya kizazi, ya matiti, na kisukari.

Alisema maambukizi ya virusi vya Ukimwi kitaifa yanazidi kupungua kwa mwaka kutoka zaidi ya watu 100,000 miaka 10 iliyopita na kufikia maambukizi 72,000 kwa mwaka.

Mwenyekiti wa Baraza la watu wanaoishi na virusi vya Ukimwi nchini (NACOPHA), Letisia Morris, aliiomba serikali kuelekeza mapambano dhidi ya ununuzi wa vifaa tiba, na utoaji wa elimu ya matumizi ya dawa za kufubaza virusi hivyo (ARV) na wanaume kujitokeza kupima kujua kama wanaishi na virusi hivyo.

"Unyanyapaa ni tishio kubwa kuliko hata VVU na Ukimwi, tupige vita unyanyapaa, hakuna sababu ya kumnyanyapaa mtu anayeishi na virusi vya Ukimwi... kwa jamii tupige vita unyanyapaa dhidi ya watu wanaoishi na virusi vya Ukimwi na utakapopima ukaonekana una maambukizi anza tiba mapema, sisi huwa tunasema 'ongeza salio ili mawasiliano yawepo'," alisema Letisia.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Kivulini, Yasin Ally, alisema hofu ya vijana wa sasa sio Ukimwi wala magonjwa ya zinaa bali ni mimba.

"Wengi wamediriki kujifungia njiti shuleni kwa ajili ya kukwepa mimba kuliko Ukimwi na magonjwa ya zinaa, takwimu inaonyesha maambukizi mapya kwa vijana wa miaka 15 hadi 24 ni asilimia 40, hapa wadau wa ukatili na Ukimwi ni lazima tutafakari tunabadilishaje mbinu kwanini hofu ya vijana hawa ambayo ni waathirika wakubwa ni mimba na sio Ukimwi na sio magonjwa ya zinaa," alihoji Ally.

Kaulimbiu ya maadhimisho hayo ni 'Jamii ni chachu ya mabadiliko tuungane kupunguza maambukizi mapya ya VVU'.



Mafundi wakiendelea na ujenzi wa barabara za mpishano (Ubungo Interchange), katika makutano ya Barabara za Morogoro, Mandela na Sam Nujoma, eneo la Ubungo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Ukosefu wa maji wasababisha magonjwa ya kuhara kwa 90%

Na Enock Charles

ASILIMIA 90 ya magonjwa ya kuhara yanayoongoza kwa vifo vya watoto yanahusishwa moja kwa moja na uchafu unaotokana na ukosefu na upungufu mkubwa wa maji katika nchi za Afrika.

Hayo yameelezwa na Mkurugenzi wa Maendeleo ya Maji na Usafi wa Mazingira kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB), Wambui Gichuri, wakati wa mkutano wa mawaziri wa maji barani Afrika unaofanyika jijini Dar es Salaam.

"Magonjwa ya kuharisha ambayo yamekuwa yakiwaathiri zaidi watoto kwa kiasi kikubwa ni kutokana na ukosefu wa maji katika maeneo mengi barani Afrika," alisema Wambui.

Akirejea ripoti ya Umoja wa Mataifa kuhusu haki za wanawake, alisema wanawake wanapoteza saa milioni sita kwa siku kwa ajili ya kutafuta maji na hivyo kupunguza uwajibikaji katika sekta nyingine za maendeleo.

Akizungumza katika mkutano huo, Waziri wa Maji, Profesa Makame Mbarawa, alisema lengo la mkutano huo ni kuunganisha nguvu ili kutafuta suluhisho la tatizo la maji katika maeneo mbalimbali barani Afrika na kuimarisha ustawi wa jamii.

"Tuko hapa kuangalia jinsi gani ya kuongeza fedha zitakazosaidia kuendeleza miradi mbalimbali ya sekta ya maji katika nchi zetu za Afrika," alisema.

Alisema changamoto za upatikanaji wa maji katika nchi mbalimbali za Afrika zinafanana na hivyo ni muhimu kwa nchi hizo kuunganisha nguvu ya pamoja katika kutatua changamoto hizo ili kuboresha maisha ya wananchi wao.

# Wakulima wapewa pembejeo bure

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

HALMASHAURI ya mji wa Kahama mkoani Shinyanga, imetoa pembejeo za kilimo kwa wakulima vijana wenye shamba la kuanzia hekari tano na kuendelea yenye thamani ya Sh. milioni 17.9 ikiwa ni njia kutatua changamoto za kilimo kwa vijana.

Samson Sumuni ambaye ni Ofisa Kilimo wa Halmashauri hiyo, aliliambia gazeti kuwa kila mwaka halmashauri inatenga fedha kupitia mapato yake ya ndani kwa ajili ya kununua pembejeo za kilimo kwa wakulima vijana.

Alisema, wakulima waliokuwa wakinufaika na pembejeo hizo ni wenye umri wa kuanzia miaka 18 hadi 35 na zaidi ya wakulima 39 kwa mwaka huu wa fedha wa 2019/20 wamenufaika na kulima hekari 195.

Sumuni alisema, mwaka huu wa fedha halmashauri ilitenga Sh. milioni 17.9 kwa ajili ya kununua mbolea za kupandia (NPK) kilo 195, mahindi kilo 550, mbegu za alizeti kilo 90 pamoja na sumu ya kuua wadudu wanaoshambulia zao la pamba, chupa 90 na kuzigawa kwa wakulima.

Vile vile, mwaka jana 2018/19 halmashauri ilitenga Sh. milioni 54 na kutumika Sh. milioni 14.19 kutokana na mwitikio wa wakulima vijana kuwa chini na kusababisha mwaka huu bajeti kupungua.

Pia, mwaka huo walinunua mbolea za kupandia (NPK) kilo 139 kwa Sh. milioni 9.03, mbegu za mahindi kilo 360 kwa Sh. milioni 2.16 na mbegu za alizeti kilo 75 kwa Sh. milioni tatu na kuwagawia wakulima 27 kwa hekari 139.

"Kuna vijana wengi wako mitaani hawana shughuli ya kufanya na kwa kuliona hili tulianzisha mpango wa kutoa pembejeo za kilimo bure kwa vijana wenye umri kuanzia miaka 18 hadi 35 na wenye uwezo wa kulima kuanzia hekari tano na kuendelea, na kila mwaka wanazidi kuongeza," alisema Sumuni.

Hata hivyo, alisema, wanawapatia elimu ya namna ya kulima kisasa na kuhifadhi chakula katika mazingira mazuri na mbinu ya kutafuta masoko.

Kadhalika, alisema kulingana na vijana wengi kuwa na mwitikio wa kujikita katika kilimo, mwaka wa fedha ujao wataongeza bajeti ya kununua pembejeo hizo ili kila kijana mwenye uwezo wa kulima hekari tano za kilimo cha mahindi, alizeti au pamba aweze kupata.



Mmoja wa wanachama wa Klabu ya Lions Dar es Salaam Mzizima, Ragib Hassanali, akipima shinikizo la damu, wakati wa kambi ya upimaji bure wa ugonjwa wa kisukari na shinikizo la damu, iliyofanyika katika Hospitali ya TMJ, tawi la Temeke juzi, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Ugonjwa wa Kisukari Duniani. Zaidi ya wakazi 300 kutoka Temeke, Ilala na maeneo ya jirani walinufaika na huduma hiyo, iliyoandaliwa na klabu hiyo, kwa kushirikiana na hospitali hiyo na duka la usambaji dawa la Samiro. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vitendo vya ukatili kwa watoto vyaitia doa Tanga

**Na Mwandishi Wetu, TANGA**

MKUU wa Mkoa wa Tanga, Martine Shigella, amekemea tabia ya wazazi, walezi na jamii mkoani humo kukumbatia vitendo vya ukatili dhidi ya watoto na kusababisha kuwa na takwimu za juu za vitendo vya ukatili.

Mkoa huo kwa mujibu wa takwimu za Jeshi la Polisi, unaongoza kwa vitendo vya ukatili nchini dhidi ya watoto.

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imeamua kuweka kongamano la vitendo vya ukatili dhidi ya watoto mkoani humo ili kujadiliana namna bora ya kuondokana na changamoto hiyo.

Mkuu wa Mkoa huo katika hotuba yake kwa wadau wa kongomano hilo alisema vitendo hivyo ni aibu kwa wakazi wa mkoa huo na kuwataka wadau wa kongamano hilo kuja na mkakati utakaowezesha kuweka mikakati ya kupambana na hatimaye kutokomeza ukatili dhidi ya watoto.

Mkurugenzi wa Watoto, Wizara ya Afya Idara Kuu Maendeleo ya Jamii, Mwajuma Magwiza, alisema kongamano hilo linafanyika mkoani Tanga kutokana na kuongoza kwa vitendo vya ukatili nchini na linahusisha watoto, viongozi wa dini na wazee mashuhuri wa mkoa huo ili kwa pamoja kutafuta namna bora ya kutokomeza vitendo hivyo.

Magwiza aliwaambia waandishi wa habari kuwa kongamano hilo linaangazia changamoto ya ukatili dhidi ya watoto kama janga kubwa ambalo kimsingi halinabudi kuangaliwa upya kwa mustakabali wa ustawi wa maisha ya baadaye ya mtoto. Aliyataja maeneo manne ambayo wizara yake na wadau watatoa kwa ajili kuelimisha eneo la ukatili, wajibu wazazi na walezi katika makuzi ya mtoto, ukatili wa watoto mtandaoni pamoja na umuhimu wa malezi na makuzi kwa ajili ya maendeleo ya mtoto.

Wakati huo huo Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Watoto kutoka Wizara ya Afya Idara Kuu Maendeleo ya Jamii, Sebastian Kitiku, akifafanua kuhusu ukatili wa watoto mitandaoni, amewataka wazazi na walezi kuwa makini na watoto kwenye matumizi ya vifaa vya kielektroniki kwa kuwa vinatumika kuendeleza vitendo vya ukatili dhidi ya watoto.

Kitiku alisema watoto wanatumia muda mwingi katika vifaa hivyo akizitaja simu kuwa tishio kwa watoto kwa kupata ukatili wa kingono mtandaoni kupitia mawasiliano hayo na kompyuta na kusababisha wengine kujiua baada ya kukosa usaidizi baada ya kufanyiwa ukatili huo na watu wasio wajua.

Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto ulipitishwa rasmi na nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa, Novemba 20, 1989 na uanzishwaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto (Child Rights Convention) na hadi sasa nchi 190 wanachama wa Umoja wa Mataifa ambazo zimetia saini na kuridhia mkataba huo.

## Kanisa Anglikana kusomesha watoto maskini

**Na Jumbe Ismailly, MANYONI**

KANISA la Anglikana Dayosisi ya Rift Valey, linatarajia kuanzisha kituo cha huduma kwa mtoto katika Wilaya ya Ikungi, mkoani Singida kitakachopokea watoto 250 wenye sifa ya kuwa maskini wa hali ya juu.

Askofu wa Kanisa hilo, John Lupaa, alisema kituo hicho kitakachofunguliwa mwezi Desemba, mwaka huu kitapokea watoto wa madhehebu yote bila ubaguzi na watapatiwa msaada wa nyanja kuu nne.

Kwa mujibu wa kiongozi huyo, misaada itakayotolewa katika nyanja hizo kwa watoto wenye umri wa kuanzia miaka sifuri hadi miaka 22 ni pamoja na kiroho, kielimu, kiuchumi, kijamii na kimwili.

"Nyanja ya kiroho maana yake masomo ya kidini na maadili mema (mafunzo ya Biblia), wanafunzi wanaosoma watalipiwa ada kuanzia chekechea hadi chuo kikuu kwa kupatiwa madaftari, kalamu, sare," alisema.

Nyanja nyingine ni pamoja na kumwandaa mtoto kuwa na uhusiano mzuri na jamii inayomzunguka, matatibu, michezo na lishe, lengo likiwa kumwondoa mtoto kwenye umaskini wa hali ya juu.

Askofu Lupaa alisema mpango huo utafadhiliwa na shirika lisilokuwa la kiserikali la Compasion International Tanzania kwa kushirikiana na Kanisa la Anglikana.

Pia, alisema kituo hicho kitatoa mafunzo ya cherehani na ufundi seremala kwa ajili ya kuwaandaa watoto hao kwenda kujiajiri katika shughuli za ujasiriamali wakati wakisubiri ajira toka serikalini.

Watoto watakaochaguliwa kujiunga na kituo hicho watagharamiwa kuanzia darasa la chekechea hadi chuo kikuu.

**"Nyanja ya kiroho maana yake masomo ya kidini na maadili mema (mafunzo ya Biblia), wanafunzi wanaosoma watalipiwa ada kuanzia chekechea hadi chuo kikuu kwa kupatiwa madaftari, kalamu, sare," alisema.**

# Madiwani Mbulu wamfagilia JPM

**Na Allan Isack, MBULU**

BARAZA la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu mkoani Manyara, limempongeza Rais John Magufuli, kwa kufanikisha ujenzi wa miradi ya maendeleo ya Hospitali ya Wilaya pamoja na jengo la utawala la makao makuu ya halmashauri hiyo.

Akizungumza katika kikao cha Baraza la Madiwani, Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Joseph Mandoo, alisema wanampongeza Rais Magufuli kwa kufanikisha ujenzi wa miradi hiyo.

Mandoo alisema Halmashauri ya Mbulu imepiga hatua ya kimaendeleo kwenye sekta ya elimu, afya, utawala, miundombinu, kilimo na ufugaji.

Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Hudson Kamoga, alisema kutokana na kutengwa kwa fedha hizo, halmashauri imezidi kupiga hatua za kimaendeleo kupitia miradi inayoendelea kutekelezwa.

"Jengo la utawala la makao makuu linaendelea vizuri na hospitali inaendelea kujengwa katika Kata ya Dongobesh, natarajia ujenzi huu utakamilika baada ya miaka mitano," alisema Kamoga.

Alisema wanatarajia kutenga eneo la kumbukumbu ambalo litaandikwa majina ya madiwani waliokuwapo madarakani kipindi cha utekelezaji wa miradi hiyo, wakiongozwa na mwenyekiti wa halmashauri hiyo na mkurugenzi mtendaji.

Mkuu wa Wilaya ya Mbulu, Chelestino Mofuga, alisema Rais Magufuli amefanya maendeleo mengi kwenye wilaya hiyo na taifa, ikiwamo ujenzi wa miradi ya kimkakati ya muda mfupi kwa kipindi cha miaka minne aliyoiongoza nchi.

"Tumeona barabara za ghorofa, elimu bila malipo, ujenzi wa reli ya kisasa, umeme, ujenzi wa hospitali mpya za wilaya na vimejengwa vituo vya afya," alisema Mofuga.

**"Jengo la utawala la makao makuu linaendelea vizuri na hospitali inaendelea kujengwa katika Kata ya Dongobesh, natarajia ujenzi huu utakamilika baada ya miaka mitano," alisema Kamoga.**

# NEC yaahidi wanahabari ushirikiano kuelekea 2020

**Na Allan Isack, ARUSHA**

MKURUGENZI wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Dk. Wilson Mahera, amesema Tume itatoa ushirikiano wa kutosha kwa vyombo vya habari nchini kuelekea uchaguzi mkuu mwaka 2020.

Akizungumza wakati wa hafla fupi ya kukabidhiwa cheti cha kutambua ushirikiano wake na waandishi wa habari alipokuwa Mkurugezi wa Halmashauri ya Arusha, Dk. Mahera aliwashukuru wanahabari kwa kutangaza na kuandika habari za mambo yaliyofanywa na serikali kwenye halmashauri hiyo.

Hafla ya kumkabidhi cheti cha shukrani ilifanyika jana katika Ofisi za Chama cha Waandishi wa Habari Mkoa wa Arusha (APC).

Alisema Rais Magufuli alipowateua aliwaambia wakajenge uhusiano mzuri na waandishi wa habari, viongozi wa dini, viongozi wa kimila na wananchi.

"Tume ya uchaguzi ipo tayari kutoa ushirikiano wa jambo lolote la uchaguzi kwa waandishi na vyombo vya habari," alisema Mahera.

Alisema walishirikiana vyema na waandishi wa habari kuandika habari na kuripoti taarifa za miradi mikubwa ya maendeleo iliyotekelezwa na serikali.

"Awali viongozi hawakuwa wanatoa taarifa za mambo yaliyofanywa na serikali, lakini Rais Magufuli alituagiza tutoe taarifa ya miradi inayotekelezwa na serikali," aliongeza Dk. Mahera.

"Tumejitahidi sana kadiri tulivyoweza kujenga mahusiano na kufanya kazi na waandishi wa habari," alisema.

Pia aliwashukuru waandishi wa magazeti ya Nipashe na The Gurdian pamoja na kwa kuandika na kuripoti habari za miradi ya maendeleo iliyotekelezwa na serikali kwenye kituo chake cha kazi cha awali.

"Kwa kweli magazeti ya Nipashe na The Guardian yametubeba katika kuhabarisha umma mambo ya kimaendeleo yaliyofanywa na serikali kwenye Halmashauri ya Arusha, nawapongeza sana kwa ushirikiano wenu kwa maslahi ya kulijenga taifa letu," alisema Mahera.

"Katika Halmashauri ya Arusha DC, tulikuwa na kata 26, na vijiji 68, maeneo yote haya tulifika na waandishi wa magazeti haya na stori zetu zilitoka, pia tulikutana na changamoto mbalimbali kama kunyeshewa na mvua na kupigwa na jua, lakini hatukukata tamaa kwani yote tulifanya kwa maslahi ya wananchi na taifa letu," aliongeza.

Alisema agizo la Rais lilitokana na kukutana na malalamiko mbalimbali akiwa katika kampeni za uchaguzi za mwaka 2015.

Alisema Julai 12, mwaka 2016 aliripoti katika kituo chake cha kazi na ilikuwa kwa mara ya kwanza kufanya kazi katika ngazi ya serikali za mitaa.

"Huku kwenye serikali za mitaa kunahitaji wasomi, kwa sababu ndio kiungo muhimu cha kupeleka maendeleo kwa wananchi," aliongeza Mahera.

Mwenyekiti wa APC, Claud Gwandu, alimpongeza kwa kuteuliwa kuwa Mkurugenzi wa NEC, na kuwa waandishi wataendelea kutoa ushirikiano kwake.

"Tunafuraha sana kwani ulifanya kazi kwa karibu na waandishi wa habari bila ya kuwa na ubaguzi, na chama kinatambua mchango wako kwani ulitusaidia kupata hatimiliki ya eneo letu la ujenzi kwenye halmashauri ambayo awali ulikuwa Mkurugenzi.

"Katika wakurugenzi wote wa Mkoa wa Arusha, wewe ulikuwa na mahusiano mazuri na waandishi wa habari, hivyo tunakutakia heri kwenye majukumu mengine ya sasa," alisema Gwandu.



Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Arusha, Dk. Maulid Madeni, akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jijini humo juzi, kuhusu kuwasimamisha kazi Mkuu wa Idara ya Mipango Miji na Ardhi, Dickley Nyato na Ofisa Mipango Takwimu na Ufuatiliaji (Mchumi wa Jiji ), Anna Mwambene, ili kupisha uchunguzi wa eneo lenye ukubwa wa ekari 30 la ujenzi kituo cha mabasi Bondeni City. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Gambo atoa neno kwa Takukuru

**Na Allan Isack, ARUSHA**

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, ameitaka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoani hapa, kuchukua hatua za kisheria mapema badala ya kusubiri kukamilika kwa miradi ya maendeleo ndipo waibuke na matatizo yaliyojitokeza.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa ziara yake ya kutembelea mradi mkubwa wa maji wenye thamani ya Sh. bilioni 520 unaotekelezwa katika Jiji la Arusha.

"Kumekuwa na tatizo la miradi mingi ikishakamilika ndio Takukuru wanaibua malalamiko ya kuwa kuna hela zimeliwa kwenye miradi, jambo hili siyo sawa," alisema Gambo.

Gambo aliitaka Takukuru iache tabia ya kuvizia watu kula fedha za umma ndipo wachukue hatua badala yake hatua stahiki zichuliwe mapema.

"Tunafahamu kuwa Takukuru ina utaratibu wa kufuatilia ujenzi wa miradi ya maendeleo hatua kwa hatua, hivyo naomba wasisubiri hadi tatizo litokee ndio watafute ufumbuzi," aliongeza Gambo.

Aidha, aliwataka wataalamu wa miradi kila wanapoandika ripoti nakala nyingine zipelekwe Takukuru kwa ajili ya kufuatilia kwa karibu mradi husika.

"Kila mnapoandika ripoti zenu nakala nyingine mzipeleke Takukuru ili waweze kutusaidia kufuatilia mradi huu kwa karibu na kama kuna tatizo litatokea hatua zichukuliwe mapema, na siyo msubiri mpaka mradi ukamilike," alisema Gambo.

"Imani yangu kwa Takukuru kama mlivyokuwa mkifanya kwenye miradi mingine katika Mkoa wa Arusha mtaendelea kuutupia jicho mradi huu," alisema Gambo.

# DC apiga marufuku wanafunzi kutumwa baa

**Na Mary Mosha, ROMBO**

MKUU wa Wilaya ya Rombo, Agnes Hokorogoro, amepiga marufuku wanafunzi kutumwa na wazazi au walezi kwenye nyumba za starehe (Baa) kwa ajili ya manunuzi ya vileo au vitu vingine vinavyopatikana maeneo hayo.

Aidha, alisema lengo likiwa kuepusha madhara yanayoweza kutokea wawapo kwenye maeneo hayo.

Aliyasema hayo jana wakati akipokea mifuko 200 ya saruji kutoka kampuni Saruji ya Moshi, kwa ajili ya ujenzi wa bweni la wasichana katika Shule ya Sekondari Maida iliyopo wilayani Rombo mkoani Kilimanjaro.

Alisema katika wilaya hii tumejikita katika kutokomeza pombe, lakini wapo baadhi ya wazazi na walezi wanawatuma wanafunzi kwenye maeneo hao, jambo ambalo linawapelekea kujifunza lugha sizo na staa na wakati mwingine kudhalilisha.

"Nimepiga marufuku mwanafunzi kutokutumwa baa, kwenda kununua pombe au kileo chochote na kwa yoyote atakayekaidi hatua kali za kisheria zitachukuliwa ikiwa ni pamoja na kifungo jela," alisema na kuongeza:

Alisema inatulazimu kupiga marufuku walimu, wazazi na jamii kuwatuma wanafunzi katika maeneo yenye vilevi kwani humo watu ambao hawana maadili wanaweza wakasababisha kuvunjwa kwa sheria ya mtoto ya mwaka 2009.

"Tumeanza na ujenzi wa bweni la wasichana ili watoto wetu wa kike waache kutembea umbali mrefu hii ikiwa ni njia ya kutokomeza mimba za utotoni na tutakapomaliza tutanza na mabweni ya wavulana lengo likiwa kuhakikisha elimu wilayani rombo inakuwa na kushika nafasi ya kwanza kitaifa,"alisema.

"Wapo wazazi wengine wanawatumia watoto hao kutoka kuuza au kusimamia maeneo wanapouza Vileo jambo ambalo wakati wengine hudhalilishwa na kudhihakiwa au kudanganywa na watu wasio na nia njema na kuharibu maisha yao," alisema.

**"Tumeanza na ujenzi wa bweni la wasichana ili watoto wetu wa kike waache kutembea umbali mrefu hii ikiwa ni njia ya kutokomeza mimba za utotoni na tutakapomaliza tutanza na mabweni ya wavulana lengo likiwa kuhakikisha elimu wilayani rombo ...**

# Vanila kuleta mabadiliko kiuchumi

**Na Mary Mosha, KILIMANJARO**

MKOA wa Kilimanjaro umeleta mabadiliko ya kiuchumi kwa kusajili Umoja wa Wakulima wa Vanila chini ya kanuni namba 14(2) kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Namba 6 ya Mwaka 2013.

Hayo yamebainishwa kwenye kikao cha ushauri cha mkoa wa Kilimanjaro, chini ya uongozi wa Dk. Anna Mghwira.

Alisema licha ya kuwapo kwa changamoto katika vyama vya ushirika lakini uwekezaji huo utaleta mabadiliko ya kiuchumi ikiwamo kukuza uchumi wa nchi.

"Tumeamua kuanzisha umoja wa Vanilla kutokana na kubaini kuwa zao hilo ni moja asili yake ni Afrika ya Kusini, India na nchi nyingine za Amerika ya kati...ambapo mkoani hapa liliingia 2000, ambapo tumepata wadau wawili waliosaidia kuhamasisha zao hili katika kutoa ajira kwa vijana na kulipa mapato ya serikali," alisema.

Alisema lengo la kusajili umoja huo ni kuwaimiza wakulima kujikita katika kulimo cha Vanilla, kwani hutumika kwenye kutengeneza harufu mbalimbali pamoja na kwenye viwanda vya kutengeneza dawa za matibabu ya binadamu.

"Hadi sasa tumefika katika halmashauri za Moshi, Hai na Siha, tutaendelea kuhamasisha halmashauri zote za mkoa huu, soko la uhakika lipo kuanzia Sh. 4,000 hadi 30,000/- kwa vanila mbichi na kutoka Sh. 300,000 hadi Sh. 800,000 kwa kilo moja ya vanila," alisema.

Naye Mrajisi wa Ushirika Mkoa, John Henjewele, alisema uanzishwaji wa ushirika huo utaweza kuleta mabadiliko ya kiuchumi katika mkoa na taifa kwa ujumla.

"Tumeanza jitiada za kuhamasisha kila halmashauri kuhakikisha wanalima zao hili ambalo linaonekana kuwa na bei kubwa na linatumika nchi mbalimbali duniani," alisema.



Mkurugenzi wa Shule ya Sekondari Mgutwa wilayani Simanjiro, Mkoa wa Manyara, Shedrack Mlemeta, akisoma taarifa kwenye mahafali ya tano ya kidato cha nne ya shule hiyo, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Same, Mwanga zaongoza uharibifu mazingira

**Na Mary Mosha, MOSHI**

BALOZI wa mazingira nchini, Padri Msafiri Aidan, amesema wilaya za Same na Mwanga zinakabiliwa na uharibifu wa mazingira unaotokana na ukataji miti ovyo na uchomaji wa mkaa hali inayochangia kuongezeka kwa ukame kwenye wilaya hizo.

Akizungumza na Nipashe jana ofisini kwake, alisema kuwa kuna haja ya serikali kubadilisha sheria ya mazingira kutokana na iliyopo imepitwa na wakati kwenye baadhi ya vipengele.

Alisema kuwa asilimia 80 ya uoto wa asili umepotea wilayani humo kutokana na uvunaji miti usioendelevu kwa ajili ya mkaa na kuni.

"Ukiangalia hizi ndizo zinaongoza kwa tatizo la ukame na hali hiyo inatokana na wakazi wa maeneo hayo kukata miti ovyo, kwani shughuli yao kubwa ni uchomaji wa mkaa unaosafirishwa kwenda mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Dar es Salaam," alisema.

Balozi huyo alisema kuwa serikali pamoja na wadau mbalimbali wa mazingira wanatakiwa kuwapatia wananchi wa wilaya husika nishati mbadala ili waweze kuachana na shughuli hizo haramu.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Mwanga, Thomas Apson, amesema kuwa msitu wa Kileo umevamiwa na watu wasiopenda mazingira wamesababisha uharibifu wa mazingira.

"Nimeshuhudia eneo kubwa la hifadhi ya msitu huo, ambao ni sehemu ya chanzo cha maji, likiwa limekatwa miti huku kukiwa na zaidi ya matanuru 12, mengine yakiwa yanafuka moshi na mengine yakiwa kwenye hatua za kuwashwa moto kwa ajili ya kupata mkaa," alisema.

Naye Ofisa Mazingira Mkoa wa Kilimanjaro, Emanueli Kiyengi, anasema changamoto ya uharibifu wa mazingira katika maeneo mbalimbali mkoani hapa ni kutokana na ukosefu wa elimu juu ya utunzaji.

"Sisi kama mkoa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali tunajikita katika kuhakikisha tunatoa elimu juu ya madhara yanayotokana na uharibifu wa mazingira ili kuweza kutokomeza tatizo hilo, alisema Kiyengi.



Ukurasa 14

**Uchaguzi Serikali Mitaa ulivyoandika historia**

Wanawake hawajaonekana kikamilifu kwenye uongozi



Ukurasa 18




Ukurasa 15

**Kutokujituma kikamilifu sababu utitiri mabango ziara za viongozi**

# siasa


JUMATANO NOVEMBA 27, 2019

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe




Ukurasa 20

**Ujasiriamali wa uasi,vita unavyochochea mauaji DRC**

# Uchaguzi Serikali Mitaa wapinzani waangalie mbele, kujipanga 2020

**Na Mwandishi Wetu**

**U**CHAGUZI wa serikali za mitaa umekamilika na wapinzani waliokuwa watazamaji badala ya washiriki wamenyakua viti kwenye baadhi ya maeneo. Ni ajabu lakini ni kweli kwa mujibu wa matokeo ya uchaguzi huo yaliyotangazwa jana.

Ni kitendawili ambacho Mwenyekiti wa Chadema Freeman Mbowe, alipohojiwa jana baadhi ya vyombo vya habari, anasema ushindi wa wapinzani wakiwamo wanachama wake ni udhaifu na aibu kwa taasisi zilizosimamia uchaguzi huo wa serikali mitaa.

Mbowe anasema kama upinzani ulijitoa rasmi inakuwaje tena wagombea walioondoa ushiriki wao washinde? Ni jambo ambalo linaipa sifa mbaya mamlaka ya kusimamia uchaguzi huo, CCM na mchakato wa kutangaza matokeo hayo umezidi kumshangaza.

Vyama vikuu vilivyojitoa ni pamoja na Chadema, CUF, ACT - Wazalendo na NCCR-Mageuzi.

Hata hivyo, katika baadhi ya maeneo kwa mujibu wa taarifa za viongozi wake, vyama vi-



**INAENDELEA UK.16**




Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe anashangaa chama chake kupata ushindi katika mitaa 69 kwenye uchaguzi ambao walijitoa. **PICHA: MTANDAO**

**Ethiopia na mchakato mamlaka za majimbo** Ukurasa 19

# Uchaguzi Serikali za Mitaa ulivyoandika historia



Viongozi wa vyama vya upinzani, Prof. Ibrahim Lipumba wa CUF (kulia), Freeman Mbowe (Chadema) na James Mbatia (NCCR Mageuzi), wakiwa kwenye moja ya harakati zao za kisiasa. **PICHA: MTANDAO**

**Na Sabato Kasika**

HATIMAYE uchaguzi wa serikali za mitaa na vijiji uliokumbwa na sintofahamu zilizosababisha vyama vikuu vya upinzani kuususia, umehitimishwa.

Ulimalizika baada ya kufanyika Jumapili iliyopita ukihusisha CCM na baadhi ya vyama vya upinzani.

Uchaguzi huo ulifanyika, huku kukiwa na mkanganyika wakati wa kupiga kura kutokana na baadhi ya wananchi kujitokeza kuwapigia kura wagombea wao kwa mujibu wa katiba, lakini vitongojini, mitaani na vijiji hakukuwa na uchaguzi na wakakuta baadhi ya vituo vimefungwa.

Vyama vikuu vya upinzani vya ACT-Wazalendo, Chadema, Chama cha Wananchi (CUF), NCCR Mageuzi, Chauma na UPDP vilisusia uchaguzi huo.

Pamoja na vyama hivyo kususia uchaguzi huo, Chama Cha Mapinduzi na vingine kadhaa vya upinzani vikiwamo vya Tanzania Labour Party (TLP), ADC na NLD vilishiriki katika uchaguzi huo.

Licha ya Waziri mwenye dhamana Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa iliyokuwa inasimamia uchaguzi huo, Seleman Jafo, kuviomba vyama hivyo kubadilisha msimamo na kurudi kwenye kinyang'anyiro hicho, viliendelea kugoma.

Msimamo huo wa upinzani haukubadilisha ratiba ya uchaguzi, na badala yake taratibu ziliendelea kama kawaida ikiwamo kufanya kampeni na hatimaye uchaguzi, ambao ulifanyika kwenye baadhi ya maeneo Jumapili Novemba 24.

> Serikali za mitaa zilirudishwa rasmi kisheria, ili kusogeza huduma zaidi za kimaamuzi, katika ngazi za wananchi kwa ajili ya kurahisisha shughuli za maendeleo.

## SABABU YA KUSUSA

Vyama vilivyosusia uchaguzi huo vilikuwa na sababu mbalimbali ingawa ni kama zilikuwa zinafanana, kwani sababu kubwa kwa ujumla ilikuwa ni kutoridhishwa na mchakato mzima kuanzia uchukuaji wa urejeshwaji wa fomu.

Kwamba wagombea wa vyama hivyo walikuwa wakinyimwa fomu, na wale waliobahatika kupata fomu hizo, walikwama kuzirejesha kutokana na kile walichodai kuwa ni kufungwa ofisi za serikali.

Kutokana na hayo na mengine kadhaa waliolalamikiwa bila kupatiwa ufumbuzi, wakaamua kujiweka pembeni kuliko kuendelea kushiriki katika uchaguzi, ambao waliamini usingekuwa wa huru na wa haki.

Wapo wapinzani wengine kama Mwenyekiti wa NCCR Mageuzi, James Mbatia, ambaye alitangaza chama chake kujitoa, lakini akashauri kufanyika kwa mazungumzo kwa ajili ya kuendelea kulinda amani ya nchi hii.

Hata hivyo, ushauri wake huo haukufanyiwa kazi badala yake maandalizi ya uchaguzi yaliendelea kama kawaida na hatimaye kufanyika kwenye baadhi ya maeneo ambayo wagombea hawakupita bila kupigwa.

Baada ya kufanyika kwa uchaguzi huo, baadhi ya wachambuzi na wadau wa siasa wamechambua na kutoa maoni yao kuhusu uchaguzi huo walipozungumza na gazeti hili jana.

Wadau hao ni Thomas Ngawaiya, ambaye ni Mkurugenzi wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo (CEGODETA) na Mjumbe wa Jukwaa la Katiba Tanzania (Jukata), Deus Kibamba.

## MSIMAMO WAO

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo, (Cegodeta), Thomas Ngawaiya, anasema uchaguzi huo uwe fundisho kwa baadhi ya wanasiasa kwa kushindwa kutimiza vigezo.

"Ninasema hivyo, kwa sababu nilisikia kuwa kulikuwa na wagombea ambao waliwekwa tu bila kuzingatia vigezo na mwisho wa siku wakaenguliwa na katika uchaguzi na kubaki wakilalamika," anasema Ngawaiya.

Mkurugenzi huyo anasema, suala la uchaguzi ni la kikatiba na kwamba kwa mtu ambaye alikuwa na malalamiko alipaswa kwenda mahakamani kama alibaini kudhulumiwa haki yake badala ya kususa.

"Lakini ajabu ni kwamba vyama havikufanya hivyo na badala yake vikasusia uchaguzi, labda nishauri kuwa viwe makini wakati wa mchakato wa uchaguzi ili kuepuka kukumbana na vigingi mbele ya safari," anasema.

## SAFARI NDEFU

Deus Kibamba ni mchambuzi wa siasa na pia mjumbe wa Jukwaa la Katiba Tanzania (Jukata), anasema bado kuna safari ndefu, ili kufikia demokraisa ya kweli nchini.

"Wazo ambalo kimsingi lilikuwa lifanikishe uchaguzi huu lilikuwa ni wadau kukaa pamoja badala kung'ang'ania kuufanya wakati tayari vyama vikuu vya upinzani vimejitoa," anasema Kibamba.

Anaeleza kuwa , matokeo yake baadhi ya maeneo vituo havikufunguliwa kwa wakati na kuwapo kwa wapigakura wachache, hali ambayo anaamini kwamba ulikuwa ni kama uchaguzi wa kituko.

"Yaani kile, ambacho nimejifunza ni kwamba tunakwenda pabaya katika kuimarisha demokrasia ya vyama vingi nchini, na nimemshangaa mtu mmoja anahojia halafu anasema umefanikiwa sana," anasema.

Mchambuzi huyo wa siasa anasema, tangu mchakato wa kuandikisha wapigakura watu hawakujitokeza kwa wingi hadi serikali ikaongeza siku, na kisha wakati wa kuchukua fomu yakajitokeza matatizo mengine.

"Hayo yote yalitosha kukaa pamoja na kwa ajili ya kupata muafaka, lakini mchakato wa uchaguzi ukaendelea na matokeo yake ndiyo hayo, ambayo Watanzania wameyaona," anasema.

Kibamba anasema, yote yaliyotokea tangu mchakato wa kuandikisha wapigakura, kuchukua fomu hadi uchaguzi, ni muhimu kujifunza kitu na kutorudia makosa uchaguzi mwingine baada ya miaka mitano ijayo.

Mdau huyo anasema, anamamini kwamba Tamisemi haina wataalam wa kusimamia uchaguzi, na kwamba tangu zamani walipendekeza uchaguzi wa serikali za Mitaa usimamiwe na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (Nec).

"Maana yangu ni kwamba Nec ina wataalama wa mambo ya uchaguzi ingawa sina uhakika kama inaweza kuwa huru kiasi cha kutangaza matokeo bila kupendelea, lakini ninaamini ina watalaam.

Anasema, iwapo uchaguzi wa serikali za mitaa utaunganishwa na uchaguzi mkuu, nchi inaweza kuokoa fedha nyingi badala ya kuacha zikipotea kwa kutenganisha uchaguzi huo.

Anakumbusha kuwa kwa mujibu wa Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tamisemi, Mwita Waitara, alikaririwa bungeni, akisema serikali ilipanga kutumia takriban Sh. bilioni 82 katika uchaguzi huo nchini kote.

"Serikali za mitaa zilirudishwa rasmi kisheria, ili kusogeza huduma zaidi za kimaamuzi, katika ngazi za wananchi kwa ajili ya kurahisisha shughuli za maendeleo," anasema.

Anasema, wananchi wamepewa mamlaka ya kuchagua viongozi wao, katika maeneo hayo na kusimamia rasilimali zao kama ardhi na nyinginezo, kukusanya mapato, kupanga matumizi.

"Kifupi ni kwamba serikali inaanzia kwenye kitongoji hadi serikali kuu, hivyo uchaguzi huu una umuhimu wake ingawa umekumbwa na hayo ambayo Watanzania wengi wameyashuhudia," anasema.

UCHAMBUZI

# Kutokujituma kikamilifu sababu utitiri mabango ziara za viongozi

Na Reubeni Lumbagala

ZIPO njia kadhaa za kuwasilisha ujumbe kwa mamlaka mbalimbali ili viongozi wapate taarifa na hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya wanaolalamikiwa au kukosolewa.

Uandishi wa ujumbe kwenye mabango ni njia mojawapo inayotumiwa na wale wanaotaka sauti zao sikike kutokana na ukweli kuwa hawajapata ufumbuzi wa kile wanachokitaka.

Mabango ya maelezo yanayoweza kulenga katika kuwasilisha kero, kupongeza au hata kubeza kama njia ya kuonyesha kutoridhika na uamuzi juu ya jambo au mambo Fulani ndani ya jamii, taifa.

Mabango hutumiwa popote duniani kwenye mikusanyiko ambayo wahusika wanalenga kuwafikishia ama viongozi wao kile wanachoona kinawaudhi , au wanakihitaji, wanakilalamikia na pia kuwapongeza.

Zama hizi ziara za viongozi wakuu hasa wanapotembelea mikoani au wanapokuwa kwenye shughuli za kijamii, uwasilishaji wa mabango yenye malalamiko umekuwa ni jambo la kawaida.

Ndiyo maana mjadala wangu leo napenda kujikita kwenye kuangalia chimbuko la mabango hayo kwa kuangalia iwapo viongozi wa maeneo yanayotoka mabango hayo wanahusika kwa kuwa pengine hawatimizi majukumu yao kikamilifu.

Naamini kuwa jukumu namba moja la kiongozi wa nafasi yeyote ile ni kuwatumikia wale anaowaongoza. Ni wajibu wa kiongozi aliyechaguliwa au kuteuliwa kuhakikisha anakuwa mtumishi wa wale anaowaongoza katika kuzitafutia ufumbuzi changamoto zinazowakabili.

Ni ili wanaoongozwa wafurahie kuongozwa na kiongozi huyo, kazi ya kiongozi ni kuwatumikia anaowaongoza, si hisani bali ni wajibu wa msingi ambao kama kiongozi atashindwa kulitimiza jukumu hilo, anakuwa katika hatari ya kutopata ushirikiano wa kutosha kutoka kwa wale anaowaongoza.

Makala hii inaungana na kauli za mara kwa mara ambazo Rais John Magufuli pamoja na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa wamekuwa wakisisitiza kuwa viongozi wanapaswa kuwatumikia wananchi waliopo katika maeneo yao ya kiutawala. Viongozi hawa mara kwa mara wanapatapo fursa za kuongea na viongozi wengine wamekuwa wakisisitiza viongozi kutenga muda kwa ajili ya kusikiliza kero za wananchi na kuzitafutia ufumbuzi.

Mkazo huu umetokana na baadhi ya viongozi kusahau wajibu wao wa kusikiliza kero za wananchi, hali inayosababisha zinapokuja ziara za viongozi wa juu kama Rais, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu katika maeneo mbalimbali kupokelewa na mabango mengi ambayo yanazungumzia kero nyingi zilizopo katika mabango hayo.

Kwa ujumla kero kwenye mabango zipo katika uwezo wa viongozi wa maeneo haya kuzitatua.



Mabango haya yanapeleka ujumbe wa aina mbalimbali kwa viongozi, lakini kama watendaji wangetimiza majukumu yao kikamilifu vilio vya shida ya maji vingetoweka. **PICHA: MTANDAO**

> Viongozi wa juu kama Rais, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu wanaweza kusaidia kutatua changamoto zile ambazo zinahitaji maamuzi kutoka ngazi za juu na si ngazi ndogo zilizopo katika idara za Halmashauri.




Hawa ni wakuu wa mikoa, wilaya, wakurugenzi na hata wakuu wa idara za halmashauri kama maofisa mipango, kilimo, ardhi na wahandishi.

Kutokana na baadhi ya viongozi kutokutenga siku za kusikiliza kero za wananchi kumesababisha uwepo wa kero nyingi zinazowakabili wananchi huku zikikosa suluhisho la kudumu kutoka kwa viongozi wao na hii kusababisha zinapokuwepo ziara za viongozi wa juu wa serikali, viongozi hao kupokelewa na mabango mengi ya wananchi.

Makala hii haipingani na uwepo wa mabango ya wananchi kwenye ziara za viongozi wa ngazi za juu, tatizo ni pale kero nyingi za wananchi za kwenye mabango zinazohitaji kuelezea masuala ambayo yalipaswa kutatuliwa na viongozi wao na si viongozi wa juu wa serikali.

Viongozi wa juu kama Rais, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu wanaweza kusaidia kutatua changamoto zile ambapo zinahitaji maamuzi kutoka ngazi za juu na si ngazi ndogo zilizopo katika idara za Halmashauri.

Mathalani, changamoto za wananchi wawili kuuziwa kiwanja kimoja, tatizo hili linaweza kumalizwa na Ofisa Ardhi wa Wilaya husika kwa kufuatilia mtiririko mzima wa suala la ununuzi wa kiwanja hicho na hatimaye mwenye haki kupewa haki yake.

Kero ya baadhi ya vijiji kutokuunganishiwa umeme, tatizo hili inaweza kumalizwa na Meneja wa Tanesco wa wilaya husika na si kusubiri ziara ya Waziri Mkuu kuelezwa na wananchi kwa njia ya mabango ili aweze kushughulikia tatizo hili.

Septemba 2, 2019, Rais Magufuli alipofanya kikao na maofisa kata wa nchi nzima Ikulu jijini Dar es Salaam aliwakumbusha wajibu wao wa kusikiliza na kuzitafutia ufumbuzi kero za wananchi na si kusubiri wananchi wabebe mabango wakati wa ziara za viongozi wa kitaifa.

Rais Magufuli alisema "ninyi ndiyo mko karibu na wananchi ili kuainisha na kutatua kero zao. Msisubiri watu wanyanyue mabango wakati wa ziara za viongozi wa kitaifa".

Vilevile, Rais Magufuli aliendelea kusisitiza "Bebeni kikamilifu dhamana zenu za uongozi. Endapo kuna kero zilizo juu ya uwezo wenu zibebeni kwa viongozi wa juu, wakiwamo wakurugenzi wa halmashauri an wakuu wa wilaya".

Mkazo wa Rais Magufuli umejikita katika msingi wa viongozi kuwa watumishi wa wale wanaowaongoza na kusimamia wajibu wao wa msingi wa kuwatumikia kwa kutatua kero zao kwa wakati.

Ni muhimu kila kiongozi kutenga siku na muda wa kuongea na wale anaowaongoza hasa kusikiliza hoja zao na kuzifanyia kazi.

Itakuwa ni jambo jema kwa viongozi wa kitaifa wanapofanya ziara katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu, wakakutana na mabango yenye kueleza kero kubwa nyingi ambazo zinahitaji uamuzi wa viongozi wa ngazi za juu ili kero hizo zipatiwe ufumbuzi wa kudumu.

Muda wa viongozi kukaa ofisini kusubiri ripoti umekwisha. Viongozi wawatembee wananchi wao na kuhakikisha kuwa kero zinatatuliwa kwa wakati ili wananchi wawafurahie kuongozwa na viongozi wachapakazi, waadilifu na wazalendo. Tafakari.

***Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.***

***Maoni: 0764- 66634***

# Uchaguzi Serikali za Mitaa wapinzani waangalie mbele, kujipanga 2020

INATOKA UK.13



Viongozi na wananchi wakijiandikisha kupiga kura kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

tatu vya CUF, ACT -Wazalendo na Chadema wagombea wake waliibuka washindi kwenye baadhi ya vijiji na mitaa na katika kundi la wajumbe mchanganyiko na hata la wanawake.

Eneo mojawapo ambalo CUF ilishinda ni Rubondo mkoani Kigoma ambako chama kilipata ushindi kwenye kijiji kimojawapo wilayani humo.

Mambo kama hayo ya wasioshiriki kushinda yanawaachia wananchi maswali kadhaa mojawapo ni hili itakuwaje kama waliojitoa wamechaguliwa? Ina maana nafasi zao zitaendelea kubakia au uchaguzi utafanyika tena kwenye sehemu hizo kwa vile kuwa wajumbe hao walishaandika na kutoa taarifa za kujiondoa ushiriki wao?

Iwapo mgombea ameshinda na chama chake kinasema hakimtambui kwa kuwa hakikushiriki kwenye kinyang'nyiro hicho hatma yake ni nini? Anaondoka kwa kuwa hana chama au anafutwa uanachama kwa kukiuka maelekezo ya chama?

Wapinzani walisema wanaamini kuwa uchaguzi si hisani wala suala la kubembelezewa bali ni mchakato wa kikatiba na kila mtu ana haki ya kushiriki, kukataa na pengine kulalamika mahakamani kama ikibidi kufanya hivyo.Ndiyo maana wakaamua kujitoa.

Kama wadau wa kisiasa, vyama vya upinzani havikufurahishwa na mchakato mzima wa uchaguzi wa serikali za mitaa na vijiji na kuamua kujiweka pembeni.

Hata hivyo, licha ya upinzani kususia uchaguzi na kukataa mapendekezo ya serikali ya kutaka wagombea walioondolewa kwenye kinyang'anyiro hicho kurudi kwenye uchaguzi, inaelekea kuwa hata huo ushindi wanaodaiwa kuupata pengine ni kura zenye utata.

Inawezekana ni hivyo kwa sababu hata hao waliokuwa wanasimamia uchaguzi waliofanya kazi ya kujumlisha na kuhesabu kura ilikuwaje wakawapa ushindi watu ambao hawajashiriki kwa kuwa wamejitoa? Maswali hayo yanazidi kuwafikirisha wapinzani ambao wanaweza kusema kuwa ni kiini macho kama Mbowe alivyosema hawakubaliani na ushindi huo.

Kama viongozi wamethibisha kuwa watu hawatashiriki kuna haja ya kuwachunguza walioshinda na kufahamu ilikuwaje wakachaguliwa kwenye sintofahamu hiyo, kama ambavyo baadhi ya viongozi wa vyama vitatu vikubwa ambao wagombea walitangazwa washindi walivyosema.

**KUANGALIA MBELE**

Hata hivyo, kwa kuwa uchaguzi wa viongozi wa vijiji, mitaa na vitongoji umekwisha na matokeo yametangazwa ni wakati wa kuangalia mbele na kujipanga kuendeleza siasa za kuchagiza maendeleo.

Kwa hiyo baada ya matokeo ya sasa wapinzani waanze kujiangalia

> Uhimilivu pia ni muhimu na kuanza kujipanga na si kujitoa kunapokuwa na misuko suko ndani ya uchaguzi.

kwani wameususia uchaguzi wa serikali za mitaa na sasa wajiandae kuingia kwenye uchaguzi mkuu wa 2020.

Ni wakati wa kujipima 'kimsuli' wanavyojiona zama hizi na kujiuliza je, wana uwezo wa kushawishi Watanzania na kujikusanyia wanachama na wakabaki nao kama walivyokuwa hapo awali?

Waendelee kujichunguza iwapo wana ubavu wa kupata kura nyingi kama ilivyokuwa siku za nyuma? Kuanzia hapo watakubaliana na mtizamo kuwa nguvu na ushawishi wao ipo ndiyo maana wakachaguliwa hata baada ya kujitoa au unapungua na kuanzia hapo watajipanga upya.

Wapinzani wasiendeleze malumbano bali wajiangalie pia kwenye kigezo cha umaarufu. Hivi zama hizi umaarufu upo au unaaanza kunyauka na wakati mwingine umepungua?

Wajitafakari kuona je suala la migogoro ndani ya vyama inayotokana na kuwa na udikteta au



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Seleman Jafo.



Profesa Ibrahimu Lipumba, Mwenyekiti wa CUF, chama chake kimeshinda uongozi katika kijiji cha Rubondo.

kukosa demokrasia jumuishi nalo likoje?

Kwa kasi gani ndani ya kambi ya upinzani kumekuwa na kasi ya kupungua kwa wanachama wengi wakihamia na kujiunga na chama tawala? Wanaoondoka ni pamoja na wabunge, madiwani na hata wanachama wa kawaida, hilo wanalitafiti na kulitolea maelezo gani?

Aidha, wapinzani watafakari pia kama wanao ushawishi kwa umma ama umepungua miongoni mwa raia . Yote hayo wayafanyie kazi kwa vile yanakuwa na taathiri kwenye ushindani wa kisiasa na uwajibikaji ndani ya vyama hivyo kwenye uchaguzi mkuu wa 2020.

**WANACHAMA**

Suala la kujua hali ya wanachama endapo wanapungua au wanaongezeka ni la kipaumbele na kufahamu iwapo kuna watu wapya wanaojiunga na vyama au hali inakuwaje. Ingefaa pia wakaangalia katika maeneo ambayo wamepata ushindi kwenye uchaguzi wa vijiji wana wanachama?

Suala jingine la kufuatilia ni hili, je vijana zama hizi wanapenda upinzani na wana mawazo mapya au kila mmoja anaangalia wapi atapata mkate wake au kama watu wanavyosema wanasaka tonge?

**UPIGAJI KURA**

Suala la wananchi kushiriki kupiga kura ni muhimu, wapinzani wajiulize vipi kasi ya upigaji kura wanaionaje? Inawapa fursa ya kujiingiza kwenye kupigiwa kura mwakani.

Pamoja na kupiga kura kuna masuala ya kuzijua kanuni na kushiriki kwenye uchaguzi, je wanachama wao wanazijua kanuni? Kama zipo kanuni mpya wanafanya jitihada gani kuzifuatilia ili zitokea mapema na kutumia wanasheria wa vyama vyao kuwafundisha wanachama wao kuzichambua na kuzijua?

> Hivi zama hizi umaarufu upo au unaaanza kunyauka na wakati mwingine umepungua?

**UHIMILIVU WA VYAMA**

Ni wakati pia wa kuchunguza na kujua uhimilivu wa vyama vyao 'party stability' hii itavisaidia kujijua na kujipanga namna ya kusimama na kushiriki uchaguzi mkuu badala ya kuamua kujitoa .

Uhimilivu pia ni muhimu na kuanza kujipanga na si kujitoa kunapokuwa na misuko suko ndani ya uchaguzi.

Kwa ujumla kujitoa si ufumbuzi wa malalamiko yanayotolewa cha msingi ni kushindana na kuona mwisho unawaletea nini. Si vyema kukimbia vita hata kabla ya kuvijadili na kujifunza nguvu ya adui unayemkabili.

## Ripoti ya BBI kutatua matatizo ya Wakenya?



Wahusika wakuu BBI, Rais Kenyatta na Raila (kulia). **PICHA: BBC**

**NAIROBI,** Kenya

JOPOKAZI la Maridhiano nchini Kenya maarufu kama Building Bridges Initiative (BBI) au handisheki, liliiloanzishwa Machi 9, mwaka2018 baada ya Rais Uhuru Kenyatta na mpinzani wake mkuu wa kisiasa, Raila Odinga , walipoamua kuzika tofauti zao za kisiasa na kusalimiana hadharani, linafanikiwa kuwaunganisha Wakenya?

Lengo kuu la BBI ni kuunganisha taifa ambalo nusura litumbukie kwenye vita kufuatia uhasama uliozuka baada ya kinyang'anyiro cha uchaguzi wa urais wa mwaka wa 2017.

Uhuru Kenyatta na Raila Odinga baadaye waliunda kamati ya watu 14 ambao waliandaa mikutano ya umma kwenye majimbo 47 kote nchini Kenya, ili kupokea maoni kuhusu mabadiliko wayatakayo wakenya hususani wakizingatia vigezo vifuatavyo;

Mosi ni jinsi ya kumaliza migawanyiko ya kikabila, kuwashirikisha watu wote kuhusu masuala ya utawala na kisiasa na mbinu za kushughulikia suala la kumaliza uhasama wa kisiasa unaotokea wakati wa uchaguzi mkuu.

Vigezo vingine ni namna ya kuimarisha amani na usalama, kukabiliana na janga la ufisadi, jinsi ya kukabiliana na ukosefu wa maadili ya kitaifa, masuala ya majukumu na haki za raia, masuala ya kuwajibika kwa pamoja

Jinsi ya kuendeleza serikali za ugatuzi.

Kamati hiyo ilikusanya maoni kutoka kwa Wakenya takribani 7,000 na imendaa ripoti ambayo iliwasilishwa kwa Rais Kenyatta na Raila Odinga.

Ripoti hiyo baadaye itatolewa hadhari na kuwasilishwa kwa umma ili ipigwe msasa.

Ikiwa Wakenya watakubaliana na yaliyomo kwenye ripoti hiyo, huenda kura ya maoni ikaitishwa na kurekebisha katiba ya mwaka wa 2010 ambayo itasababisha mabadiliko katika muundo wa serikali.

Mambo muhimu yaliyojitokeza katika jopo hilo maarufuku kama 'Handisheki' ni pamoja na mpasuko mkubwa wa kisiasa ulijitokeza nchini Kenya kuhusu maridhiano kati ya Rais Uhuru na kiongozi wa upinzani Raila Odinga.

Maridhiano hayo yameleta mgawanyiko ndani ya chama tawala cha Jubilee na Muungnao wa Upinzani unoongozwa na Raila Odinga wa NASA.

Aidha, Naibu Rais William Ruto, anaongoza mrengo wa kisiasa ujulikanao kama Tangatanga" unaoonekana kupinga handisheki kati ya Uhuru na Raila.

Kadhalika, Uhuru na Raila nao katika juhudi zao za kupigia debe maridiano yao ya kisiasa wana wafuasi wao wanaoegemea mrengo wa kisiasa wa 'Kieleweke.'

Miongoni mwa vigogo wa Muungano wa NASA wanaopinga 'handisheki' ni Musalia Mudavaidi, ambaye ni kinara wa chama cha Amani National Congress (ANC). **BBC**

# Wanawake hawajaonekana kikamilifu kwenye uongozi



Baadhi wa wabunge wanawake wakifuatilia vikao vya bunge . Watafiti na watetezi wa haki za kinamama wanataka ushirikishwaji zaidi wa wanawake kwenye masuala ya uongozi kwa kuwa bado hawajapewa nafasi kama inavyostahili. **PICHA: MTANDAO**

**Na Elizabeth Zaya**

WADAU wa utetezi wa haki za binadamu na za wanawake wanaiona serikali ya awamu ya tano kama imevunja rekodi kwa kumthamini mwanamke wa Tanzania jambo ambalo limedhihirika kwa kumteua Samia Suluhu Hassan, kuwa Makamu wa Rais.

Makamu wa Rais ni wa kwanza kushika nafasi hiyo tangu taifa lipate uhuru mwaka 1961, lakini licha ya uteuzi wake, wanawake wanasema pamoja na kuvunja rekodi hiyo kwa serikali ya awamu ya tano kumteua mwanamke katika nafasi hiyo nyeti kuna kusuasua .

Wanaona kuwa bado idadi ya uwakilishi wa kundi hilo katika nafasi mbalimbali za uongozi katika kipindi cha miaka minne ya serikali hiyo ni mdogo.

"2015 baada ya kuingia kwa serikali ya awamu ya tano, ilivunja rekodi ya kumteua Makamu wa Rais, tutaendelea kuipongeza kwa hatua hii, ambayo imeweka historia katika nchi yetu,"anasema, Deo Temba ambaye ni Ofisa Programu Mwandamizi kutoka Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP).

Wanayasema hayo katika mahojiano na Nipashe kwa nyakati tofauti, yaliyolenga namna wanawake wanavyochangia kwenye uongozi wa nchi katika awamu ya tano.

> Hii haijalishi ni katika uchaguzi wa serikali za mitaa, wala uchaguzi mkuu, idadi yao ya kugombea bado siyo ya kuridhisha kwa kuangalia mijini na vijijini.

Temba anaeleza kuwa katika miaka minne ya serikali ya awamu ya tano wanawake mawaziri ni asilimia 17 na makatibu wakuu ni asilimia 11 pekee, aidha, kwa upande wa wakuu wa mikoa ni asilimia 23 wakati wakuu wawilaya ni asilimia 28.

Akizungumzia nafasi za wanawake ndani ya vyama vya siasa, Ofisa Programu wa TGNP, anasema ndani ya vyama hivyo, idadi ya wanawake wanaoteuliwa na vyama vyao kuwania nafasi mbalimbali za uongozi wa juu nako bado hali hairidhishi.

"Katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 wanawake walioteuliwa ndani ya Chama Cha Mapinduzi ni asilimia tisa,Chadema ni asilimia sita, Chama cha Wananchi CUF, asilimia 11 wakati ACT-Wazalendo ni asilimia 15."

Temba anasema katika ngazi ya udiwani, kati ya wagombea 10,879, wanawake walikuwa 679 jambo ambalo halivutii sana masikioni kwa watetezi wa haki za uongozi.

## UWAKILISHI KUPUNGUA

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), cha Dar es Salaam, kinaona kwamba katika kipindi cha miaka minne ya serikali ya awamu ya tano, uwakilishi wa wanawake umepungua kidogo.

"Na hapa hatuwezi kulaumu kwa sababu hatuna sheria ambayo imeelekeza kwamba nafasi za wanawake katika uongozi na hasa wa kuteuliwa uweje. Nafasi hizi huwa zinatolewa kutokana na utashi wa kiongozi husika aliye madarakani kwa wakati huo,"anasema Anaemy Sillayo.

Sillayo Meneja Utafutaji Rasilimali wa LHRC, anaongeza:

" Kwa upande wa wabunge pekee, ndiyo katiba inazungumzia kwamba wanawake wasipungue chini ya asilimia 30, lakini katika maeneo mengine hasa ambayo yanahitaji uteuzi kama mawaziri, wakuu wa mikoa na wilaya,makatibu wakuu haizungumzi chochote isipokuwa utashi wa kiongozi mwenyewe aamue kuteua au kutoteua na ndiyo maana wakati mwingine wanaweza kuongezeka au kupungua zaidi."

"Mfano tunazo wizara takribani 20, lakini wanawake mawaziri ni wanne tu, ambaye ni Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako, Waziri wa uwekezaji, Angela Kairuki na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Ajira na Watu Wenye Ulemavu,Jenista Mhagama,"anasema Sillayo.

Anaeleza kuwa kwa ujumla kuna kurudi nyuma katika suala zima la uongozi kwa wanawake hususani uongozi wa juu, kwa sababu bado katika maeneo mengi, wanawake hawajapewa nafasi za kusimamia ofisi mbalimbali za serikali ikiwamo wizara na bodi mbalimbali.

Sillayo anasema kukosekana kwa idadi kubwa ya wanawake katika nafasi za juu za maamuzi kunachangia kuwapo kwa changamoto mbalimbali katika jamii hususani zinazolenga usawa wa kijinsia.

"Hali hii inachangia ule mchango wa wanawake katika kufanya maamuzi kuwa nyuma na ndiyo tunaona kwamba zinapotokea changamoto, kundi la wanawake wanarudi nyuma, japokuwa tunashukuru kwamba kitendo cha kumpatia mwanamke katika nafasi moja hiyo kubwa ya kuwa msaidizi wa Rais, kimetupa nguvu kubwa na tumeshuhudia mchango mkubwa, anaoutoa katika kutetea wanawake na kuwapa moyo kupambana katika nafasi mbalimbali za uongozi,"

## KUSHIRIKI UCHAGUZI

Sillayo anasema anaona bado wanawake wamekuwa hawajitokezi vya kutosha katika kugombea nafasi za uongozi katika nyanja mbalimbali zinazoanzia kwenye serikali za mitaa hadi ubunge.

Anasema wanawake ndilo kundi kubwa ambalo limekuwa likijitokeza kwa wingi kupiga kura kuchagua viongozi wao katika maeneo mbalimbali japo nao si wagombea.

"Tunafahamu mwitikio uliopo kwa wanawake katika kujitokeza kupiga kura kuchagua viongozi wao, lakini hatuwaoni kujitokeza kama kupiga kura, kugombea nafasi mbalimbali za uongozi hususani za kisiasa,"anasema Sillayo.

Anaongeza: "Hii haijalishi ni katika uchaguzi wa serikali za mitaa, wala uchaguzi mkuu, idadi yao ya kugombea bado siyo ya kuridhisha kwa kuangalia mijini na vijijini."

LHRC wanasema kuwapo wa wanawake wengi katika nyanja mbalimbali za uongozi kunasaidia kuchagia maendeleo.

## KINACHOWAKWAMISHA

LHRC inasema baadhi ya changamoto zinazochangia wanawake hao kushindwa kuwania nafasi mbalimbali katika siasa na uongozi ni kutokana na vikwazo mbalimbali ambavyo hukutana navyo.

Anataja baadhi ya vikwazo vinavyokwamisha wanawake wengi kushindwa kuwania nafasi mbalimbali za kisiasa kuwa ni pamoja na mfumo dume uliojengwa katika vyama vya siasa.

Sillayo anasema mfumo uliopo kwa vyama vilivyo vingi vya siasa, haumpi mwanamke kipaumbe kuwania nafasi mbalimbali za uongozi hata katika nafasi za juu za ndani za vyama vya siasa.

Aidha, ukosefu wa rasilimali hasa fedha na vitendea kazi vinavyohitajika kwenye kampeni nayo ni changamoto inayowakwamisha kina mama hao.




Wakazi wa Sidama katika moja ya kampeni za kupiga kura za kujipatia uhalali wa kuwa jimbo huru. **PICHA: MTANDAO**

# Ethiopia na mchakato mamlaka za majimbo

**Na Mashaka Mgeta**

WAKAZI wa Sidama nchini Ethiopia wamepiga kura ya maoni ya kutaka kuwa na mamlaka ya kuunda serikali ya jimbo lao, wakati ambapo jamii za kikabila zikihitaji mamlaka hayo kupitia mpango wa mageuzi ya Waziri Mkuu, Abiy Ahmed.

Mji wa Hawassa uliopo takribani kilomita 275 zikiwa ni sawa na maili 170, kusini mwa mji mkuu, Addis Ababa ndipo yatakapokuwa makao makuu ya Sidama.

Tume ya Uchaguzi ya nchi hiyo ilitangaza Jumamosi kuwa, matokeo ya awali ya kura hiyo yalionesha kwamba waliounga mkono walikuwa asilimia 98.5 ya wapiga kura waliojitokeza Jumatano ya wiki iliyopita wakiwa ni asilimia 99.7 ya waliojiandikisha.

Matokeo hayo yanaihakikishia Sidama yenye asilimia nne ya Waethiopia milioni 105, kuwa jimbo la 10 lenye mamlaka ya kudhibiti ushuru wa ndani, elimu, usalama na sheria ndogo nchini humo.

Katiba ya Ethiopia inatoa haki ya kutafuta mamlaka ya jimbo kujitegemea, kwa jamii za zaidi ya makabila 80, ikiwa ni kupitia mpango wa mageuzi ya kisiasa ya Waziri Mkuu Abiy Ahmed.

Nchi, ambayo ilikuwa moja ya mataifa yenye ukandamizaji wa haki za kiraia barani Afrika, imekuwa ikifanyika mageuzi makubwa ya haraka ikiwamo utekelezaji wa misingi ya uwazi, tangu Waziri Mkuu Abiy alipoteuliwa kushika wadhifa huo mwaka jana.

Lakini uhuru mkubwa uliopo umesababisha kuibuka mvutano wa kikabila ambao umekandamizwa kwa muda mrefu na kuwatia nguvu wakuu wa majimbo yenye nguvu kudai haki zaidi kwa watu wao.

Kwa mujibu wa taarifa ya vikundi vya waangalizi wa Umoja wa Mataifa, kwa kipindi cha mwaka jana, vurugu za kikabila ziliibuka na kusababisha zaidi ya watu milioni mbili kuyahama makazi yao huku mamia kadhaa wakiuawa.

> Ninaogopa jamii ya Sidama watakuja na kutupiga...watachukua ajira zetu na hata tukifungua mashtaka hatutatendewa haki kwa sababu tutakuwa tunalalamika kwa walio miongoni mwao.

Matokeo ya kura yaliyotolewa Jumamosi yanaweza kuhamasisha jamii za kabila nyinginezo zinazofikiria kuomba kura ya maoni kujitafutia mamlaka zaidi, hatua inayoweza kutishia mpango wa Waziri Mkuu Abiy kuimarisha umoja wa raia wa nchi hiyo kabla ya Uchaguzi Mkuu uliopangwa mwaka 2020.

Mamlaka mapya ya Sidama yatalitoa eneo hilo katika ukanda wa kusini (SNNP), sehemu 'iliyokubuhu' kwa ukabila, ikipakana na Kenya na Sudan Kusini.

Ofisa Mwandamizi wa Polisi mjini Hawassa, aliliambia Shirika la Habari la Reuters kuwa sherehe za kushangilia ushindi huo zilipigwa marufuku siku ya Jumamosi, lakini zingeweza kuruhusiwa baada ya matokeo rasmi kutangazwa.

Watu walishindwa kujitokeza hadharani kusherehekea, lakini madereva wengi walionekana wakiimba na kupiga miziki kwenye magari yao.

Muda mfupi baada ya matokeo kutangazwa, kundi la vijana waliokuwa wamekusanyika kwenye uwanja wa katikati ya mji wa Hawassa wakiimba na kucheza.

Hata hivyo, sherehe zao hazikudumu sana baada ya kutawanywa na askari polisi, miongoni mwao wakikamatwa na kuwekwa ndani.

Baada ya matokeo kutangazwa, mmoja wa wanaharakati wa Sidama, Unani Fikro (24), alikaririwa na Reuters akisema, "kuna marafiki waliouawa, kufungwa na wengine wameihama nchi kwa sababu ya suala hili.

Fikro akaongeza kusema, "kwangu, siku ya leo ni kama yenye ukombozi." Kisha akabubujikwa machozi.

Hata hivyo, matokeo hayo hayakuwafurahisha watu wa kabila nyingine wanaoamini kwamba mamlaka hayo yatawasababishia kutengwa na kubaguliwa.

"Ninaogopa jamii ya Sidama watakuja na kutupiga...watachukua ajira zetu na hata tukifungua mashtaka hatutatendewa haki kwa sababu tutakuwa tunalalamika kwa walio miongoni mwao," alisema kijana wa miaka 28, Tsion, ambaye hakutaka jina lake kamili litajwe kwa kuhofia usalama wake.

Kamishna wa Haki za Binadamu wa Ethiopia, Daniel Bekele, aliyetembelea zaidi ya vituo 100 vya kupigia kura kwenye miji mitano na maeneo 15 ya vijijini katika Sidama wakati wa upigaji kura Jumatano iliyopita, alisema kulikuwa na amani na hakukuwa na ukiukwaji mkubwa wa kanuni za upigaji kura hiyo.

Zaidi ya watu milioni mbili walisajiliwa na tume ya uchaguzi kushiriki katika upigaji kura huo.

Taarifa za vyombo mbalimbali vya habari zilieleza kuwa vituo vya kupiga kura vilifunguliwa mapema, yapata saa 12 asubuhi licha ya wapiga kura kuonekana wakiwa kwenye foleni kabla ya muda huo.

Hali hiyo inatajwa kusababisha ofisi nyingi za umma, shule na maeneo ya biashara kufungwa ili kupisha upigaji kura.

Ili kutoa mwanya kwa watu wengi zaidi kushiriki upigaji kura, taarifa zaidi zikaeleza kutoka vyanzo tofauti kwamba magari hasa ya abiria yalizuiliwa ikiwa ni sehemu ya hatua zilizochukuliwa na utawala, ili kuhakikisha upigaji kura unafanyika kwa amani.

Julai mwaka huu, palikuwapo taarifa zilizohusu watu kadhaa waliokuwa wakishiriki kampeni kutoka jamii za kikabila za Sidama, waliuawa katika ghasia wakati walipojitangazia mamlaka ya jimbo hilo kinyume na sheria.

Wachambuzi kadhaa wanasema mageuzi yanayofanywa na Waziri Mkuu Abiy, yanamuweka pia katika kukabiliwa na ugumu katika kuzuia ukabila ambao unatishia kuongeza mgawanyiko nchini humo.

Kwa hiyo, kura hiyo ya maoni inaonekana kama jaribio la kupata suluhu ya kadhia ya makabila yanayotaka kujitenga, ikiwa inaweza kutatuliwa kwa amani.

Tangu alipoingia madarakani, Aprili mwaka jana, Waziri Mkuu Ahmed, amesifiwa kwa kuleta mabadiliko ambayo hayakutarajiwa nchini humo.

Anadaiwa kuongoza mchakato wa amani na mataifa yaliyokuwa adui wa Ethiopia hasa Eritrea, tukio lililochangia akashinda tuzo ya amani ya Nobel mwaka huu.

Ingawa ni hivyo, kwa upande mwingine, Waziri Mkuu amezua hofu kwa hatua yake ya jinsi anavyoangazia mashirika na vyama vinavyopigania haki ya makabila tofauti nchini humo.

Katiba ya Ethiopia ya mwaka 1995, iliunda majimbo tisa ya kikabila yakiwamo ya Tigray linamilikiwa na watu wa kabila la Tigraya, Amhara - leyney jamii ya kabila la Amharic, wakati Sidama ilikuwa ndani ya SNNPR ambapo kuna makazi ya makabila 50.

Likiwa na asilimia nne ya idadi ya watu nchini humo, Sidama ni kabila la tano kwa ukubwa na kwamba wengi wanahisi kwamba wanahitaji utambulizi mkubwa kisiasa na serikalini.

***Makala hii imeandikwa kutoka vyanzo mbalimbali.***

# Ujasiriamali wa uasi,vita unavyochochea mauaji DRC



Wananchi wanaishi kwa wasiwasi muda wote kwa kuwa ndivyo waasi wanavyokuwa mitaani wakazunguka na silaha, hasa eneo la kaskazini mashariki mwa Congo. **PICHA: MTANDAO**

**Na Ani Jozeni**

HALI ya eneo la kaskazini-mashariki ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), imekuwa ya piga nikupige. Ni kwa sababu majeshi ya serikali ya Congo yanafanya msako na kulipua maskani au makambi ya jeshi la waasi la Allied Democratic Front (ADF) na kukimbia.

Jeshi hilo la waasi ambalo kwa miaka kadhaa lilikuwa linaonekana kuwa ni kundi la kivamizi kutoka Uganda au linalotumia eneo la Congo kushambulia Uganda linarudi, kufanya mashambulizi ya kulipa kiasi, na kuendeleza shughuli zake. Ndicho kinachotokea hivi sasa eneo hilo, ambako kwa wiki kadhaa watu wengi wameuawa.

Taarifa za awali kutoka Uganda miaka kadhaa iliyopita zilikuwa zinalitangaza kundi hilo kama la Kiislamu,kiongozi wake anaitwa Jamal Mukulu, lakini halionyeshi dalili zozote zile za kundi la aina hiyo. Halifahamiki kushambulia mahoteli ya kitalii au maduka makubwa ya supermarket kama Al Shabaab inavyofahamika kwa mashambulizi yake jijini Nairobi.

Watafiti wanasema kuwa kundi hilo hasa linasaka kudhibiti maeneo ili kufanya shughuli kama kununua vito maeneo hayo na kuviuza nje bila kusimamiwa na chombo chochote cha dola.

> Ilifika wakati wakazira kuendelea kuhusishwa na mauaji DRC kutokana na kupanuka kwa mkono wa sheria.

Inadaiwa maofisa wa jeshi wanahusika nalo pia ili kujinufaisha kiuwekezaji kwenye biashara isiyodhibitiwa.

Kwa upande mwingine mauaji ya raia yanayotokea kila wakati ni sehemu ya vitisho vya kundi hilo kwa wakazi wa maeneo hayo kulazimisha kulipatia kundi hilo nyenzo za aina tofauti, ikiwa ni pamoja na kuwasomba vijana wadogo kujiunga nalo.

Kwa upande mmoja kundi hilo tayari linaonekana kuchukua nafasi ya M23, ambayo viongozi wake walikamatwa na kufunguliwa mashtaka katika Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu wa Kivita huko Hague Uholanzi, na inaelekea likakosa kuungwa mkono na watawala nchini Rwanda.

Ilifika wakati wakazira kuendelea kuhusishwa na mauaji DRC kutokana na kupanuka kwa mkono wa sheria.

Yako makundi mengine ya kijeshi DRC kama lile la wakimbizi wa Rwanda waliohusika na mauaji ya kimbari mwaka 1994 ambao sasa wamekuwa kama kabila dogo la ziada DRC, sehemu ya Wanyarwanda waliokuwapo kabla. Wana mielekeo tofauti kuhusu utawala wa DRC na kwa jumla wanashiriki katika 'ujasiriamali wa kivita' unaoendelea nchini humo kama sehemu ya uporaji wa maliasili katika eneo la kaskazini mashariki.

Utawala wa sheria umesambaa kwa kiasi fulani maeneo mengine ya DRC tangu vita ya wenyewe kwa wenyewe kuanzia 1997. Ni wakati alipovurumishwa ugenini Rais Mobutu Seseseko na jeshi lililotokea Rwanda, ikiwa na Uganda.

Baadhi ya wachunguzi wanasema ADF inakutanisha wapiganaji kutoka makundi kadhaa mengine yaliyokuwa na nguvu awali, ikiwamo RCD (Rassemblement Congolais de la Democratie) Chama cha Kidemokrasia Congo.. uande wa Kisangani. Ni kundi lililotokana na umoja wa awali uliouondoa utawala wa Mobutu lakini ukafarakana wakati alipouawa Rais Laurent Kabila na walinzi vijana, hivyo ikaanza vita kati ya vipande vya umoja huo wa awali na wanaoiunga mkono Rwanda. Baadaye kundi hilo likaungana na wapiganaji wa Rwanda walioshiriki mauaji ya kimbari,likateketezwa wakati majeshi ya Rwanda yalipopenya hadi misitu iliyoko nyika kusini ya Kisangani, jiji muhimu zaidi la DRC upande wa kaskazini.

Wananchi katika eneo la kaskazini mashariki ya DRC wanaishi katika hofu ya mashambulio wakati wowote, na ziko taarifa kuwa maofisa wa jeshi la nchi hiyo wanaotoa fedha kwa makamanda wa ADF kwa kila mwananchi anayeuawa.

Wako maofisa wa Jeshi la Congo waliohojiwa na watafiti wakasema walipewa ahadi ya kulipwa Dola 250 kwa kila mtu atakayeuawa, lakini hawakusena nani aliwapa mchongo huo. Taarifa nyingine zinaainisha kuwa kuna wakati maofisa wa jeshi la serikali wanafika katika eneo fulani vijijini halafu baada ya siku mbili waasi wanakuja na kuua watu wengi, kuzuia serikali isifanye kazi.

Mara nyingine inatokea wakazi wa maeneo hayo wanawatambua wanaowashambulia, kwa mfano licha ya kuwa kundi hilo linasemekana kutokea Uganda, lina askari wengi wa eneo hilo kwani baadhi yao wanazungumza Kinyarwanda, lugha mojawapo ya Mashariki ya DRC Ndiyo maana wachambuzi wanasema kundi hilo lipo kwa takriban miongo miwili licha ya kuwa siku za nyuma yalikuwa yanasikika makundi mengine kama FDLR (la washiriki mauaji ya kimbari Rwanda), M23 (wasisi waliokuwa wanaonekana kutumiwa na utawala wa Rwanda), Mai Mai na mengine.

Halafu kuna wanaopata fedha nyingi za ndanii ya DRC au za nje kutokana na uhitaji wa ulinzi, hivyo ADF isipofanya mauaji maofisa wengi watakosa posho za kuwa nje ya vituo, safarini, n.k.

Vingozi wa serikali za mitaa eneo la |Beni wanasema kuwa kundi la ADF linafanana na Al Shabaab, hoja ambayo walinda amani wa Umoja wa Mataifa (MONUSC) hawaitilii maanani hisia hiyo.

Hawakubali kulinganisha ADF na Boko Haram kama meya wa Beni alivyoashiria, Ila MONUSC wanasema kundi hilo linashirikiana na makundi ya kijeshi katika nchi za jirani, na inaelekea wana washirika Uganda, ambako pia yamekuwepo mashambulio hata maeneo ya miji ya kati kusini ya nchi hiyo ambayo ndiyo maskani ya serikali, kwa miaka mingi tu.

Inaaminiwa kuwa sehemu ya jeshi la polisi nchini Uganda ilikuwa inashirikiana na waasi kufanya hujuma.

Jambo la kusikitisha ni kuwa kuna aina ya mashindano ya kufanya mashambulizi na kuua raia kwani kuna faida zinazopatikana hasa katika mustakabali mzima wa kulinda amani, halafu kupitisha magendo, kuendesha migodi bila bughudha ya kodi.

Kwa vile DRC bado iko katika mkwamo wa kisiasa ambako serikali iliyoko madarakani haina uwezo wa kubadili sura ya utawala uliowekwa na aliyekuwa rais, Joseph Kabila ambaye bado ana wingi wa viti bungeni, haitakuwa rahisi kubadili hali hiyo.

Kimsingi tatizo hapo ni ulimbikizaji mali kwa kufyeka miguu ya dola ili wenye migodi na biashara nyingine wasiingiliwe. Pengine kuua ni kuhakikisha kuwa kila kitu kinabaki kama kilivyo, hasa kwa upande wa maofisa wa juu wa jeshi la ulinzi la DRC.



HABARI MBEYA

# Waomba msaada mama mapacha 4

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

FAMILIA ya Emelia Joram (21), mkazi wa Mwakibete jijini Mbeya, mwenye watoto mapacha wanne, imeendelea kuwaomba Watanzania kuisaidia kwa hali na mali ili kuhakikisha watoto hao wanakuwa na afya njema.

Akizungumza na waandishi wa habari katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya ambako bado wamelazwa, mama mzazi wa binti huyo, Cecilia Mbaza alisema baada ya taarifa za mwanaye kusambaa kupitia vyombo vya habari wameanza kupokea misaada kutoka kwenye makundi mbalimbali.

Alisema kwa sasa wanahitaji msaada kutokana na kutokuwa na uwezo wa kuwanyonyesha watoto wote na hivyo wanahitaji maziwa mbadala kwa mujibu wa ushauri waliopewa na madaktari.

Alisema kwa sasa bado wanaendelea kuishi hospitalini hapo tangu mtoto wake alipojifungua Oktoba 31 mwaka huu kutokana na kwamba baadhi ya watoto walikuwa wapo kwenye chumba cha joto kutokana na kuzaliwa wakiwa na uzito pungufu.

Cecilia alisema vilevile madaktari wamewataka waendelee kubaki hospitalini hapo kwa ajili ya uangalizi zaidi wa mama pamoja na watoto wake na kwamba wataruhusiwa baada ya kujiridhisha.

"Kulea watoto hawa ni changamoto kubwa sana, mama yao amefanyiwa upasuaji hivyo hataruhusiwa kufanya kazi ngumu, lakini hata mimi siwezi kuwaacha nyumbani niende kutafuta, nitalazimika kuwa nao karibu mpaka watakapokua," alisema Cecilia.

Alisema kutokana na mazingira hayo anawaomba Watanzania wanaoendelea kuguswa waendelee kumsaidia ili awalee vizuri wajukuu zake hao ambao watatu ni wa kike na mmoja pekee ndio wa kiume.

Hata hivyo alisema historia ya familia zote mbili yaani upande wa mama na upande wa baba ni za mapacha lakini mapacha zaidi ya wawili imekuwa ni mara ya kwanza kutokea.

# TMA yahimiza tahadhari ya radi

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, imewataka wakazi wa mikoa hiyo kuchukua tahadhari ya kuuawa na radi kwa kuweka vifaa vya kukinga radi hiyo kwenye makazi yao pamoja na maeneo ya mikusanyiko.

Akizungumza na Nipashe, Meneja wa TMA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Issa Hamad, alisema radi ni mawimbi ya umeme yenye chaji za hasi (-ve charges), na kwamba inaleta madhara kwa binadamu na viumbe hai vingine kutokana na kwamba vina madini yenye chaji chanya (+ve charges).

Alisema inapotokea radi chaji hizo huwa zinavutana na kusababisha madhara, na kwamba miongoni mwa madini yenye chaji chanya zinazovutana na radi ni chuma, dhahabu na chumvi ambayo alidai kuwa baadhi yake yanapatikana kwenye miili ya binadamu na ndio maana huwa inaleta madhara.

Alisema ili kujikinga na madhara ya radi wananchi wanatakiwa kuepuka kukaa chini ya miti wakati mvua yenye radi inaponyesha, kuepuka kusimama sehemu ambayo mtu atakuwa mrefu kuliko vitu vyote.

"Lakini pia inashauriwa watu kuvaa viatu vikavu ili maji yasiweze kupitisha radi na ikitokea upo eneo la wazi ambalo hakuna vitu vingine virefu tunashauri upunguze kimo chako kwa kuchuchumaa ama kukaa ili angalau ikija itafute sehemu yenye miti," alisema Hamad.

Alisema radi huwa inapendelea eneo lenye mkusanyiko mkubwa wa chaji za chanya ikiwamo maeneo ya shule ambako wanafunzi huwa wanakusanyika, hivyo kutengeneza kundi kubwa la chaji hizo ambazo zinavutia radi.

Alisema maeneo hayo yanatakiwa kuwa na vikinga radi (Earth wire) ili kuzuia kutokea kwa radi hiyo ambayo inaweza ikasababisha madhara makubwa kwa watu.

Alisema mara nyingi radi imekuwa ikitokea katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kutokana na uwapo wa madini ya aina mbalimbali ambayo yanavutana na chaji za hasi.

Aliwatahadharisha wananchi kuepuka kuyahusisha matukio ya radi na imani za kishirikina kwa maelezo kuwa havina uhusiano na badala yake ni mambo ya sayansi ambayo wananchi wanahitaji kuelimishwa ili wayafahamu na wachukue tahadhari.

Hamad alisema taasisi hiyo inaendelea kutoa elimu kwa wananchi kwa njia mbalimbali, ikiwamo kutoa taarifa za utabiri wa hali ya hewa kila siku kupitia vyombo vya habari na mitandao ili wananchi wazitumie kufanya shughuli zao.

Alisema endapo wananchi watafuatilia na kuzielewa taarifa hizo na wakazingatia, wataepuka madhara ya radi pamoja na kufanya shughuli zao za uzalishaji mali kwa ufasaha.



Kijiko cha kampuni ya ukandarasi kikiendelea na ujenzi wa barabara ya kuanzia Mama John hadi Mwakibete, jijini Mbeya juzi. Ujenzi huo, ukikamilika utasaidia kupunguza msongamano wa magari kwenye barabara kuu ya Tanzania na Zambia. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# 11 mbaroni tuhuma gongo, mihadarati

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

WATU 11 wanashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani Mbeya wakiwamo wazee watatu kwa tuhuma za kukutwa na pombe haramu ya moshi (gongo) pamoja na dawa za kulevya aina ya bangi.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jana, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei alisema watu hao walikamatwa kupitia operesheni iliyofanyika Novemba 24 mwaka huu katika maeneo mbalimbali ya mkoa huo.

Alisema katika tukio la kwanza jeshi hilo lilimkamata mzee mmoja aliyetajwa kwa jina moja la Enny (65) Mkazi wa Airport ya zamani jijini Mbeya akiwa na lita tano za gongo nyumbani kwake na kwamba mzee huyo ni muuzaji na mtumiaji wa pombe hiyo.

Alimtaja mtuhumiwa mwingine kuwa ni Roida Ijande (60) mkazi wa Mtaa wa Mama John jijini Mbeya ambaye alikutwa na lita 20 za gongo na kwamba mtuhumiwa ni muuzaji na pia ni mtumiaji wa pombe hiyo.

Mtuhumiwa mwingine aliyenaswa ni mzee Lazack Mwakabungu (61) mkazi wa Uyole jijini Mbeya ambaye alikutwa na gongo lita 15 ambaye anadaiwa kuwa ni muuzaji na mtumiaji wa pombe hiyo haramu kwa mujibu wa sheria.


Kamanda Matei aliwataja watuhumiwa wengine waliokamatwa na gongo kuwa ni Janepha Cosmas (28) mkazi wa Kata ya Isyesye jijini Mbeya ambaye alikutwa na lita moja na nusu ya pombe hiyo akiwa ameigawanya kwenye chupa ndogo ndogo 15.

Alisema mtuhumiwa huyo pia alikutwa na bangi yenye uzito wa gramu 280 na kwamba mtuhumiwa ni mtumiaji na muuzaji wa pombe hiyo pamoja na bangi. Wengine waliokamatwa na pombe hiyo ni Amina Kabale (42) mkazi wa Mtaa wa Ilembo na Hassan Nasoro (25) mkazi wa Mji wa Tunduma mkoani Songwe wakiwa na gongo lita mbili pamoja na gramu 10 za bangi.

Wengine waliokamatwa na bangi ni Msafiri Jackson (30) Mkazi wa Nsalaga jijini Mbeya ambaye alikutwa na gramu 10, Agustino Mahinya (24) mkazi wa Nsalaga jijini Mbeya ambaye alikutwa na gramu 10, Paschal Uledi (31) ambaye ni kondakta wa daladala na mkazi wa Iwambi ambaye alikutwa amepanda miche minane nyumbani kwake.

Vilevile aliwataja Naomi Said (43) mkazi wa Uyole ya Kati jijini Mbeya ambaye alikutwa na lita 10 za gongo na Ramim Mbluki (18) mkazi wa Nsalaga jijini Mbeya ambaye pia alikutwa na bangi yenye uzito wa gramu 25.

Alisema watuhumiwa wote wamehifadhiwa katika kituo cha Polisi Kati wakati upelelezi unaendelea na kwamba baada ya upelelezi zitaanza taratibu za kuwafikisha mahakamani kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria.





# JPM aagiza kibano stika bandia za viza

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

RAIS John Magufuli ameagiza vyombo vya ulinzi na usalama kushughulikia haraka watu waliokamatwa kwa kuingiza stika bandia za viza zenye thamani ya Sh. bilioni 1.4.

Agizo hilo alilitoa juzi alipokuwa akiweka jiwe la msingi kwenye ujenzi wa makao makuu ya idara hiyo jijini hapa.

Alisema kuna watu wanatengeneza viza bandia na zimekuwa zikiikosesha serikali fedha, hivyo lazima mtandao huo umalizwe.

"Najua kuna suala linashughulikiwa na vyombo vya ulinzi na usalama, suala hili lishughulikiwe haraka la wale walioleta stika feki za viza za Sh. bilioni 1.4 washughulikiwe ili tumalize huu mtandao maana zimekuwa kila mara zikija zinachapishwa nchi jirani zinapitishwa uwanja wa ndege, "alisema.

Alimwagiza kamishna kufuatilia watendaji ambao wamekuwa wakitengeneza viza bandia na kuikosesha fedha serikali.

Pia alisema bado baadhi ya watendaji wake hawajamwelewa, huku akisema Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ni miongoni mwao.

Alisema amekuwa akizungumzia kuhusu kuwatumia wafungwa kwenye ujenzi wa miradi ya wizara hiyo, lakini bado halieleweki na hivyo kulazimika kutumia Jeshi la Wananchi kujenga nyumba za askari.

"Hapa kwenye hili jengo uwekaji wa Landscaping Sh. milioni 400 nilisikitika, kuna wafungwa 18,000 wangeletwa hata 200 na majembe wangelima lisingewazuia kupiga gwaride na kwata.

"Ndipo hapo huwa najiuliza sana inawezekana watendaji wangu hawajanielewa na miongoni mwa wasionielewa ni Wizara ya Mambo ya Ndani," alisema.

Alisema alipelekwa kwenye wizara hiyo Naibu Waziri ambaye ni mhandisi na amesajiliwa na bodi ya makandarasi na hata cheti cha usajili yeye ndio aliyemkabidhi kipindi akiwa waziri wa ujenzi.

Kuhusu ujenzi wa jengo la uhamiaji, Magufuli aliagiza kupitiwa upya gharama za ujenzi wa jengo la Idara ya Uhamiaji kutokana na kuwekwa vitu visivyo na umuhimu ikiwamo mfumo wa ulinzi (Security system) unaogharimu Sh. bilioni nane.

"Nilitoa Sh. bilioni 10 kwa ajili ya kuanza kujenga, baada ya kuomba kununua nyumba 113 za watumishi, nilikubali na pia ajira 400 nilikubali lakini hili la kutumia vifaa vya security system Sh. bilioni nane nakataa," alisema. Alisema hana wasiwasi na muundo wote unagharimu Sh. bilioni 12 kwa kuwa ni jengo la ghorofa nane na gharama za ukamilishaji Sh. bilioni 2.7.

"Ndio maana nazungumza haya mengine yananiumiza, shida za wananchi ni nyingi, Sh. bilioni nane ni kwa ajili ya CCTV kamera na milango ya kujifungua, kweli jengo ni zuri, lakini mmeweka vingine sio vya umuhimu," alisema. Rais alisema: "Angalau zingekuwa hela ndogo lakini si Sh. bilioni nane, sasa mkandarasi mwelekezi ambaye ni Chuo Kikuu cha Ardhi mnapaswa mtusaidie kupunguza gharama na sio kuongeza."

Alisema kipengele cha Sh. bilioni nane amekigomea na kuwataka kuangalia uwezekano wa kupunguza gharama.

"Badilisheni muundo wa milango yenu, CCTV kamera haichukui Sh. bilioni nane ni simple, mimi nilifunga wakati ule kwa Sh. nilioni tatu, sasa hii CCTV ya Sh. bilioni nane ipi? Unawapa watu wizara wakusaidie lakini hawakusaidii," alisema.

Aliagiza Kamishna wa Idara hiyo na wizara zinazohusika wakae na kupitia gharama wala zisifike Sh. bilioni 20.

"Inawezekana ziwe chini ya hapo, ningefanya mimi mabadiliko ingekomea Sh.b ilioni 14, unaweka milango ya kujifungua wenyewe kwani hamna mikono, mbona vitu vingine mnaweza kusukuma kwa mikono yenu?" Alihoji.

Awali, Kamshina Jenerali wa Uhamiaji, Dk. Anna Makakala, alisema Rais alitoa Sh. bilioni 10 kwa ajili ya ujenzi wa makao makuu ya Idara ya Uhamiaji Dodoma.

"Uliagiza kujengwa jengo zuri la kisasa linaloendana na hadhi ya uhamiaji, jengo hili litakuwa na hadhi ya kitaifa na kimataifa linatarajiwa kukamilika Novemba 27, mwaka 2020 na litakuwa la ghorofa nane na uwezo wa kuchukua watumishi 1,200," alisema.




Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango (wa pili kushoto), akipokea gawio la serikali kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Masanja Kadogosa (kulia), jijini Dodoma jana. Kushoto ni Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Doto James na Msajili Hazina, Athumani Mbuttuka. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Dodoma kunolewa uondoaji taka ngumu

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

WANANCHI wa Jiji la Dodoma watafundishwa namna ya kuondoa taka ngumu na za kawaida ili kulifanya jiji kuwa safi.

Mafunzo hayo yatatolewa na Shirika la Kimataifa la Uhifadhi wa Mazingira na Wanyamapori (WWF) kwa kushirikiana na kampuni ya simu ya mkononi Vodacom.

Hayo yalibainishwa jana na Mratibu miradi wa WWF, Savinus Kessy, baada ya kufanya usafi katika soko la Chang'ombe jijini hapa. Alisema mafunzo hayo ni sehemu ya utekelezaji wa mradi wa mwaka mmoja wa uhifadhi na utunzaji wa mazingira unaolenga kuifanya Dodoma kuwa ya kijani.

"Shirika limefanya jitihada hizi ili kuhakikisha tunaunga mkono jitihada za serikali za kufanya Dodoma kuwa ya kijani na mradi huu na mwaka mmoja una lengo la kuboredha mazingira ya Dodoma kupanda miti, kuhifadhi misitu na mazingira pamoja na kutengeneza bustani," alisema.

Alisema wamemua kufanya hivyo ili kuunga mkono jitihada za serikali za kuifanya Dodoma kuwa jiji la kijani ili liendane na hadhi ya jiji.

"Mradi huu tunashirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais tutafanya pia mafunzo kwa jamii ya kujifunza kutengeneza mifuko mbadala ya plastiki ili kuendeleza kampeni ya kutunza mazingira," alisema Kessy. Meneja wa Ruzuku na Mawasiliano Vodacom, Sandra Oswald, alisema wameanza kwenye jiji hilo ili wananchi watunze mazingira na kwamba wanatarajia kufikia miji mingine nchini.

"Tunahamasisha usafi wa mazingira kwa ujumla kwa kushirikiana na WWF na tumepanga kufanya katika mikoa mitatu tumeanza na Dodoma na baadaye mikoa mingine ambayo itapangwa," alisema.

Naye Ofisa Mazingira wa jiji, Ally Mfinanga, alisema usafi kwenye masoko ni muhimu kwa kuwa unasaidia kuepukana na magonjwa ya mlipuko hasa kipindi hiki cha mvua.

## CBE yashauriwa kufanya utafiti

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

SERIKALI imekiagiza Chuo cha Biashara nchini (CBE) kufanya utafiti mbalimbali kwa kina katika sekta ya biashara ili kuleta mabadiliko chanya ya sekta ya viwanda na biashara.

Agizo hilo lilitolewa na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, Anthony Mavunde, katika mahafali ya 54 ya chuo hicho tawi la Dodoma.

Mavunde alisema CBE inapaswa kujikita kufanya utafiti wenye mashiko katika sekta hizo ili matokeo yake yasaidie kuleta mabadiliko katika biashara nchini.

"Taifa linategemea wasomi katika sekta mbalimbali kwenda kufanya mabadiliko katika jamii inayotuzunguka, ikiwamo kusaidia wananchi kutatua changamoto zilizopo ndani ya sekta ya biashara ili iweze kusonga mbele," alisema.

Aidha, alisema serikali haitegemei kuona wasomi wanakuwa sehemu ya wanaolalamika.

"Mnapaswa kwenda kuwa sehemu ya watatuzi wa malalamiko katika sekta ya viwanda na biashara," alisema Mavunde.

Aliwataka kwenda kutumia vyema elimu waliyopata kwa kujikita kwenye tafiti maeneo tofauti na kuibua suluhisho la changamoto za sekta ya biashara.

"Mkifanya hivi ndani ya muda mchache Tanzania itafika mbali katika sekta ya viwanda na biashara ambayo ni muhimu katika kuongeza uchumi wa nchi," alisema.

Mavunde alisema serikali inafurahia kuona CBE inatoa wataalamu ambao inaamini wanakwenda kuwa msaada kwa wafanyabiashara wadogo na wakubwa kwa kuwapa ujuzi na maarifa ya ufanyaji biashara kitaalamu.

"Serikali itaendelea kuunga mkono jitihada zinazofanywa na CBE tunaomba wataalamu mnaohitimu katika chuo hiko mkawe chachu ya maendeleo ya taifa letu," alisema Mavunde.

Naibu Waziri huyo aliwahakikishia wahadhiri kuwa wataendelea kujiendeleza katika vyuo vya ndani na nje ya nchi ili kuboresha chuo hicho kiweze kutoa wataalamu walio bora kwenye sekta ya biashara.

**"Taifa linategemea wasomi katika sekta mbalimbali kwenda kufanya mabadiliko katika jamii inayotuzunguka, ikiwamo kusaidia wananchi kutatua changamoto zilizopo ndani ya sekta ya biashara ili iweze kusonga mbele," alisema.**



## HABARI ZANZIBAR

# Matatani tuhuma kuomba mgonjwa rushwa ya ngono

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MTUMISHI wa Hospitali ya Serikali ya Chakechake Kisiwani Pemba, Masoud Suleiman Abdallah, amesimamishwa kazi kwa tuhuma za kuomba rushwa ya ngono kwa mgonjwa.

Mgonjwa huyo alikwenda hospitalini hapo kutibiwa, hivyo hatua hiyo imechukuliwa ili kupisha uchunguzi wa tuhuma hizo.

Waziri wa Wizara hiyo, Hamad Rashid Mohammed, alisema pamoja wizara yake kumsimamisha kazi mtumishi huyo, wizara imeomba ripoti kamili kutoka Taasisi ya Kuzuia Rushwa Zanzibar (ZAECA) ambayo ilimtia mbaroni mtuhumiwa huyo ili kupata ukweli.

ZAECA ilimkamata mtumishi huyo wa kitengo cha Ultra Sound katika Hospitali hiyo Novemba 21, mwaka huu baada ya kudai rushwa ya ngono kwa mgonjwa kama malipo ya huduma hiyo.

Waziri Hamad alisema mtumishi huyo amesimamishwa kazi kwa mujibu wa kifungu namba 841 cha Sheria ya Utumishi Serikalini ya mwaka 2011 na kifungu cha 843 cha sheria hiyo.

Alisema wizara imekuwa ikijitahidi kuwaeleza watumishi wake juu ya uwajibikaji, heshima na kufuata maadili na miiko wakati wote wanapotekeleza majukumu yao kwani kazi hiyo inahitaji heshima na uaminifu mkubwa kwa jamii.

"Niwaombe watumishi kuhakikisha wanafuata maadili ya kazi zao kwa kuona wanaheshimu taratibu na kanuni za kazi," alisema.

Naye Mkurugenzi Uendeshaji na Utumishi wa wizara hiyo, Ramadhan Khamis Juma, alisema hivi sasa mtuhumiwa huyo atapatiwa nusu mshahara kwa kipindi cha miezi sita, na kama suala hilo halitakuwa limepatiwa ufumbuzi, mshahara wake utasimamishwa kabisa kwa mujibu wa sheria.

Pia alisema ikiwa mtuhumiwa huyo ikibainika hakutenda kosa, atarejeshewa haki zake zote, ikiwamo mshahara na haki nyingine muhimu.



Mafundi wa kampuni ya ujenzi ya Nyanza Road, wakichimba mtaro kwa ajili ya kutoa karavati za zamani ili waweke mpya katika Barabara ya Kitunda, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Bashiru ajigamba ushindi S/Mitaa

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ally, amesema ushindi wa CCM katika uchaguzi wa serikali za mitaa uliopatikana kwa upande wa Tanzania Bara ni kielelezo tosha cha ushindi wa mwaka 2020.

Aliyasema hayo alipowasili Zanzibar kwa ajili ya ziara ya kichama ya wiki moja ambayo itamalizika Desemba 4, mwaka huu.

Hata hivyo katika uchaguzi huo wa Novemba 24, vyama vikubwa viliususia kwa madai kuwa usingekuwa huru na haki kutokana na ukiukwaji wa taratibu, ikiwamo kuenguliwa kwa wagombea wao.

Lengo la ziara hiyo ni kuimarisha Chama Cha Mapinduzi visiwani Zanzibar, ambapo atashiriki shughuli mbalimbali za kichama kwa kuzungumza na viongozi wa ngazi mbalimbali sambamba na kuzindua miradi ya maendeleo.

Dk. Bashiru alisema ushindi huo wa asilimia 99 umepatikana kutokana na kukubalika kwa CCM kwa wananchi wanaonufaika na utekelezaji wa Ilani ya CCM mijini na vijijini.

Aidha, Dk. Bashiru alifafanua zaidi kwamba lengo la ziara hiyo ni kushauriana na wanachama wa CCM masuala mbalimbali yatakayosaidia kuendelea kuimarisha chama hicho.

"Nitaanza ziara yangu Unguja kisha kumalizia Pemba, nitakutana na wanachama mbalimbali nizungumze nao kuhusu masuala ya kuendelea kukijenga chama chetu kwani tupo kwa ajili ya kuwatumikia wananchi," alisema Dk. Bashiru.

Naye Katibu wa Kamati Maalum ya NEC Idara ya Itikadi na Uenezi CCM Zanzibar, Catherine Peter Nao, aliwasihi wanachama, viongozi na makada wa chama hicho kujitokeza kwa wingi katika maeneo mbalimbali ambayo Dk. Bashiru atafanya ziara.

# UNDP yakunwa uchumi Zanzibar

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Maendeleo (UNDP), limepongeza kasi ya ukuaji wa uchumi wa Zanzibar.

Akizungumza na Rais wa Zanzibar, Mwakilishi Mkaazi wa UNDP nchini, Christine Musisi, alieleza kuwa katika kipindi cha uongozi wa Rais Dk. Mohamed Shein shirika hilo limeona mageuzi makubwa ya kiuchumi, kimaendeleo na kuimarika kwa utawala bora.

Alisema kuwa UNDP litaendelea kuiunga mkono Zanzibar katika kuendeleza na kuimarisha miradi mbalimbali ya maendeleo ili Zanzibar izidi kupata mafanikio.

Aidha, mwakilishi huyo alieleza kuwa katika uongozi wa Rais Shein, shirika hilo limeweza kushuhudia mafanikio makubwa ya kimaendeleo ikiwamo juhudi za kupamba na umaskini na kukuza uchumi.

Alieleza kuwa huduma za kijamii zimezidi kuimarika zikiwamo huduma za afya, elimu, majisafi na salama pamoja na huduma nyingine na juhudi zilizofanyika katika kupambana na maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU).

Alisema UNDP iko tayari kuendelea kuiunga mkono Zanzibar katika kuimarisha na kuendeleza miradi ya maendeleo ikiwa ni pamoja na kusaidia vipaumbele vyote vilivyowekwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Naye Rais Shein alieleza kuwa shirika hilo ni miongoni mwa nashirika ya Umoja wa Mataifa (UN) ambalo limekuwa na ushirikiano, na kuweza kuiunga mkono Zanzibar kwa muda mrefu.

Dk. Shein alisema uchumi wa Zanzibar umezidi kuimarika kutokana na ushirikiano mkubwa kati ya uongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na wananchi wake bila ya kuwasahau washirika wa maendeleo ikiwamo UNDP.

Aidha, alieleza juhudi na mikakati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuimarisha na kukuza uchumi wake ikiwa ni pamoja na kuiimarisha sekta ya uwekezaji, viwanda sambamba na kuiendeleza na kuiimarisha sekta ya utalii ambayo inachangia kwa asilimia 27 ya Pato la Taifa la Zanzibar na asilimia 80 ya fedha za kigeni.

# SUA waomba mashamba yaliyofutiwa umiliki

Na Idda Mushi, MOROGORO

RAIS John Magufuli ameombwa kuangalia kuwapatia wahitimu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) mashambapori yanayofutiwa umiliki wake kwa kushindwa kuendelezwa na wanafunzi na wahitimu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), ili watumie taaluma yao kuyaendeleza mashamba hayo kivitendo.

Wanafunzi hao wanasema wanaweza kuyatumia kwa kuzalisha mazao mbalimbali na kuwa mfano kwenye jamii.

Ushauri huo ulitolewa na Rais wa Serikali ya Wanafunzi wa chuo hicho (SUASO), Dioniz Zakaria, kwenye kongamano la viongozi wa serikali hiyo uliokwenda sambamba na uwasilishaji wa mada mbalimbali zikiwamo za uongozi, uzalendo na utawala bora.

Akasema wanafunzi na wahitimu wa SUA wana uwezo mkubwa kwenye uzalishaji mali kupitia sekta za kilimo, mifugo na uvuvi, ingawa changamoto kubwa ni mtaji, lakini iwapo watawezeshwa kwa kupatiwa mashamba, wataweza kuonyesha taaluma hiyo kivitendo na kusaidia nchi katika uzalishaji wa chakula na mazao ya biashara sambamba na kutoa elimu kivitendo katika nyanja hizo. Akasema fursa hiyo ni muhimu sana kwao na kwa taifa hasa wakati huu ambao Taifa limejielekeza kukuza uchumi wake kupitia sekta ya viwanda, ambapo malighafi kwa ajili ya kuendesha viwanda hivyo zinahitajika kwa wingi.

"Rais anasisitiza sana dhana ya ukuaji wa uchumi kupitia sekta ya viwanda, tunataka tumuunge mkono kivitendo kwa kutumia taaluma zetu, tunakuomba sana mgeni rasmi (Katibu wa CCM Mkoa wa Morogoro, Shaka Hamdu Shaka), utufikishie salamu hizi kwa Rais," alisisitiza Rais huyo wa SUASO.

Aidha, waliomba kuongezwa zaidi ya idadi ya wanufaika wa mikopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kwani wengi wanaosoma chuoni hapo ni watoto wa wakulima na wafugaji na ni wahitaji.

Shaka, akaahidi kufikisha ombi hilo kwa Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Ally Bashiru Ally, alifikishe kwa Mwenyekiti wa CCM Taifa ambaye ni Rais Magufuli.

Naye Katibu wa Siasa na Uenezi wa CCM Mkoa wa Morogoro, Anthony Mhando, aliwahimiza wanafunzi wa vyuo vikuu kutojihusisha na migomo wala mapinduzi yasiokuwa msingi badala yake watambue kila mmoja amekwenda chuoni kwa dhamira yake binafsi ya kujiletea maendeleo na kama kuna hoja watumie mamlaka mbalimbali kuzifikisha na kuzitatua.



Mkazi wa jijini Dar es Salaam, akishusha gunia la mkaa kwenye lori, ili kujipatia ujira wa siku katika eneo la Soko la Mabibo juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Asasi kampeni 'Linda Ardhi ya Mwanamke' zatakiwa kujipanua

Beatrice Moses

ASASI na mashirika 26 yanayoshiriki kwenye kampeni ya 'Linda Ardhi ya Mwanamke' yametakiwa kujitawanya nchi nzima hasa vijijini, ili kutoa elimu itakayosaidia kuelimisha jamii kuona umuhimu wa umiliki sawa wa ardhi.

Mila na tamaduni potofu hasa zinazokandamiza wanawake, ikiwamo kuminya fursa ya kumiliki ardhi sawa kwa wanaume na wanawake, zinatajwa kupewa nafasi zaidi katika maeneo ya vijijini.

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, ndiye aliyetoa changamoto hiyo kwa kueleza kuwa serikali inabaini hilo. Hivyo kuzitaka taasisi hizo kuunganisha nguvu ya kutoa elimu vijijini, wakati zikiteleza kampeni hiyo ili kusaidia kuleta mafanikio.

Dk. Ndungulile aliyasema hayo mwishoni mwa wiki, wakati akizindua kampeni hiyo akimwakilisha Waziri wa wizara hiyo, Ummy Mwalimu. Dk. Ngungulie alibainisha kuwa wanawake wa vijiji ndiyo wamekuwa wakikumbana na vikwazo katika kumiliki ardhi, na kwamba serikali inakamilisha kuandaa sera ya jinsia na kuitengea bajeti.

Alisema wanaamini sera hiyo itasaidia kuongeza nguvu katika kuendeleza mapambano dhidi ya mila na tamaduni potofu, kwani

licha ya kuwapo kwa sheria zinazotoa uwiano sawa kwa kumiliki ardhi bado wanakutana na vikwazo kupata umiliki wa rasilimali hiyo.

"Bado kuna changamoto nyingi kwa mwanamke kumiliki rasilimali ardhi, serikali tunaendelea kuzifanyia kazi kuzimaliza, hivyo kuondoa migongano ya kisheria ikiwamo sheria ya mirathi na dini," alisema.

Mwenyekiti wa kamati inayoratibu kampeni hiyo, Tike Mwambipile alisema licha ya kuwa sheria ya Tanzania zinatoa haki sawa ya kumiliki ardhi kwa kurithi au kununua bado jamii inayomzunguka imeendelea kuwa kikwazo hasa katika umiliki ardhi ya kurithi.

Mwambipile ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA), alisema kampeni hiyo ni ya kimataifa imechaguliwa kuwa nchi ya mfano kutokana na kuwa na sheria nzuri za ardhi.

Kampeni hiyo inaratibiwa na Shirika la Kimataifa la Landesa kwa kushirikisha asasi nyingine kadhaa ikiwamo Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA).

# Madaktari 80 Korea watibu bure macho

NA Beatrice Philemon

JUMLA ya wagonjwa 80 kutoka mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Pwani na wilaya zote wamefanyiwa upasuaji wa mtoto wa jicho bure katika Hospitali ya Rufani Tumbi, mkoani Pwani kwa msaada wa Shirika la Kimataifa Korea Kusini.

Mkurugenzi mkazi wa shirika hilo, Vision Care hapa nchini, Taegyun Kim, alisema jumla ya madaktari bingwa wa huduma ya macho wakiwamo manesi wawili kutoka shirika hilo walikuwa nchini siku tano kufanya operesheni ya mtoto na kusaidia wagonjwa kuona tena.

Aliwataja madaktari bingwa wa huduma ya macho ni Dk. Jaeyoon Kim, Dk. Jihong Bae, nesi Yoona Kim na Yemin Song ambao wapo nchini kwa ajili ya kufanya upasuaji wa mtoto wa jicho pamoja na kutokomeza upofu unaozuilika.

Anasema timu hii ya wataalamu wa macho kutoka Korea Kusini ilifanya upasuaji kushirikiana na daktari bingwa wa macho wa Tanzania, Dk. Susan Kimaro.

Pia wakiwa nchi walitoa mafunzo kwa madaktari wa Tanzania kuhusu njia mbalimabli za kufanya upasuaji wa macho na jinsi ya kutumia mashine za kisasa ili wawe mahili katika utumiaji wa machine hizi na baadaye kuweza kutoa huduma bora za macho kwa wagonjwa.

"Tumeamua kutoa huduma ya upasuaji wa mtoto wa jicho bure kwa kuondoa ukungu katika jicho baada ya kugundua kuwa asilimia kubwa ya wananchi ambao wana ugonjwa huu hawawezi kumudu gharama za matibabu na wengi ni wale wenye kipato cha chini," alisema.

Aidha, alisema madaktari hao bingwa wa macho kutoka Korea Kusini watakuja nchini tena mapema mwakani kutoa huduma hiyo ikiwamo ugonjwa wa trakoma na magonjwa mengine ya macho.

Naye daktari wa macho mkoa wa Pwani, Eligreayer Mnzava, aliishukuru Vision Care kwa kuwapatia mashine za kisasa zenye teknolojia ya hali ya juu katika Hospitali ya Tumbi kwa ajili ya kufanya upasuaji wa matibabu ya huduma za macho na kusaidia wagonjwa kuona tena.

**"Tumeamua kutoa huduma ya upasuaji wa mtoto wa jicho bure kwa kuondoa ukungu katika jicho baada ya kugundua kuwa asilimia kubwa ya wananchi ambao wana ugonjwa huu hawawezi kumudu gharama za matibabu na wengi ni wale wenye kipato cha chini," alisema.**

# Mtoto wa miaka 9 kupata shahada

**BRUSSELS,** Ubelgiji

MTOTO huyo wakati akiwa na umri wa miaka minne alianza shule ya msingi, lakini hata kabla ya wanafunzi wenzake kuanza sekondari, Laurent Simons, anatarajiwa kuhitimu shahada ya chuo kikuu akiwa na umri wa miaka tisa.

Laurent Simons kutoka Ubelgiji alitumia muda wa mwaka mmoja kumaliza darasa la kwanza katika shule ya msingi, kama wanafunzi wengine.

Baada ya hapo kasi yake iliongezeka na katika mwaka uliofuatia akiwa na miaka sita alianza elimu ya sekondari na kufanya kila kitu ndani ya miezi 18 wakati kwa kawaida elimu ya msingi huchukua miaka sita kumaliza.

Baada ya hapo alipumzika kidogo. Akiwa na umri wa miaka nane, alichukua likizo ya kunoa ubongo (sabato) kwa muda wa miezi sita akichukua mapumziko hayo akiwa nyumbani. Miezi minane iliyopita, alijiandikisha katika mahafali ya chuo kikuu.

Laurent alisema anapendelea jinsi gani teknolojia inaweza saidia mwili wa binadamu na utafiti wake wa mahafali ya chuo unahusu kadi ya eletroniki iliyounganishwa kwenye ubongo.

Kadi hiyo inapima na kufuatilia maelfu ya mishipa ya fahamu 'neva' kwa wakati mmoja na baada ya miezi tisa ya kusoma, atapokea shahada ya uhandisi wa umeme mwezi ujao.

Hata hivyo alisema hana uhakika jinsi gani ameweza kufanya vitu vyote hivi. Kipindi cha BBC Newsday kilipomuuliza inakuaje anatunukiwa shahada akiwa na umri wa miaka tisa, Laurent alijibu na kusema " Hata mimi sijui.'

Mtoto huyo anayetoka katika familia ya madaktari anataka kusomea udaktari na kufanya shahada ya uzamivu. Lakini malengo yake yamepita sifa za kitaaluma.

Laurent alisema, ''Lengo kubwa ni kuongeza na kuboresha urefu wa maisha. **BBC**



Mtoto Lauent Simon akiwa anajisomea. **PICHA: BBC.**

# Walioumia maporomoko Pokot waanza kusaidiwa

**NAIROBI,** Kenya

MAOFISA wa usalama wamewasili katika jimbo la Pokot Magharibi nchini Kenya kwa ajili ya kutoa msaada kwa waathiriwa wa maporomoko ya udongo. Mmoja wa waathiriwa aliiambia BBC jana asubuhi.

Idadi ya watu waliofariki katika maafa ya maporomoko ya ardhi yaliyosababishwa na mvua kubwa inayonyesha katika eneo la Pokot Magharibi imefikia watu 56, kwa mujibu wa ofisa wa serikali katika eneo hilo.

'' Polisi na wanajeshi wamefika hapa kwa helikopta kubwa mbili'', alisema muathiriwa Thomas Ngura ambaye jirani yake alipoteza watu watano kwenye mkasa huo uliotokea mwishoni mwa wiki.

Alisema msaada ulipatikana hata hivyo haujatosha, akiwa na matumaini kuwa serikali itaendelea kuwasaidia kukabiliana na athari za maporomoko ya ardhi.

> **Tumeshauriwa twende eneo salama la Paroa. Watu wanapofika katika maeneo salama kama haya wanapewa chakula, nguo na blanketi.**

Ngura alisema kuwa waathiriwa wote na watu ambao hawana makazi kutokana na mkasa wa maporomoko ya ardhi walishauriwa kuhamia maeneo salama kama vile shule ili kuyanusuru maisha yao, kufuatia mvua kubwa inayoendelea kunyesha.

"Tumeshauriwa twende eneo salama la Paroa. Watu wanapofika katika maeneo salama kama haya wanapewa chakula, nguo na blanketi," alisema Ngura.

Hata hivyo, alisema hali ya wasiwasi bado imetanda miongoni kwa wakazi wa West Pokot kutokana na dalili za kunyesha kwa mvua zaidi inayoweza kusababisha maafa makubwa.

''Katika eneo la kijiji chetu hatujawapata watu sita waliozikwa ndani ya mapromoko ya udongo ..hatujui wako wapi, labda serikali itatusaidia kuwapata. Polisi wamekuja wamewasaidia watu kutafuta miili aliongeza Ngura.

Idadi ya miili ambayo haijapatikana ni 22, baada ya mkasa huo kuyakumba maeneo ya Parua, Nyarkulian na Muino, kwa mujibu wa Gavana wa jimbo hilo, Profesa John Lonyangapuo.

Profesa Lonyangapuo aliiambia BBC juzi kuwa shughuli ya kusaka na kuokoa miili bado inaendelea.

Juhudi za kuipata na kuivuta miili kutoka kwenye matope zimekwamishwa na miundombinu mibaya baada ya barabara zinazokwenda katika maeneo hayo kuharibika.

Alisema kuwa nyumba 22,000 zimeharibiwa na maporomoko ya ardhi na kati ya watu 80,000 na 120,000 wamesambaratika au kuathiriwa na mafuriko hayo. **BBC**



Papa akiwahutubiwa viongozi wa Japan na wanadiplomasia. **PICHA: REDIO VATICAN.**

# Papa amaliza ziara, hija nchini Japan

**TOKYO,** Japan

KIONGOZI wa Kanisa Katoliki Duniani, Papa Francisko, ametaka kuwa na uhusiano wa kidiplomasia kati ya Vatican na Japan na kuhimiza ujenzi wa utamaduni wa watu kukutana na kujadiliana ili kuwa na maono mapana ya ujenzi wa dunia inayosimikwa katika haki na udugu.

Katika kauli mbiu iliyochaguliwa na Baraza la Maaskofu Katoliki Japan kwa ajili ya hija ya 32 ya Baba Mtakatifu nchini Japan kuanzia Novemba 23 hadi 26 , 2019 ni: "Linda Maisha Yote". Alisema huo ni ujumbe mzito unaotikisa "sakafu ya nyoyo za watu" ili kusimama kidete kulinda, haki, tunu msingi, utu na heshima ya binadamu dhidi ya vitisho vinavyohatarisha misingi ya amani na utulivu na hasa zaidi mashindano na umiliki wa silaha za kinyuklia," ni kwa mujibu wa Baba Mtakatifu Francisko.

Kiongozi huyo aliyasema hayo alipomtembelea Mfalme Naruhito wa Japan na kufanya naye mazungumzo ya faragha pamoja na kumtakia heri na fanaka kwa kuanza awamu mpya ya uongozi wake.

Baba Mtakatifu alikutana na kuzungumza na Shinzo Abe, Waziri Mkuu wa Japan na baadaye akatoa hotuba kwa viongozi wa serikali na wanadiplomasia wanaoziwakilisha nchi zao huko Japan.

Katika hotuba yake alisema uhusiano wa kidiplomasia kati ya Vatican na Japan ni muhimu na kuhimiza ujenzi wa utamaduni wa watu kukutana na kujadiliana ili kuwa na maono mapana zaidi wa ujenzi wa dunia inayosimikwa katika haki na udugu wa kibinadamu.

Aidha, alikumbusha kwamba utunzaji bora wa mazingira ambayo ni nyumba ya wote ni sehemu ya mchakato wa kudumisha utu, heshima na haki msingi za binadamu duniani.

Baba Mtakatifu alisema, hija yake ya kitume nchini Japan inapania kuwaimarisha ndugu zake katika imani, matumaini na mapendo, ili waendelee kujitoa sadaka bila ya kujibakiza katika huduma kwa kutoa kipaumbele cha kwanza kwa maskini na wale wote wanaosukumizwa pembezoni mwa jamii akitumia kauli mbiu inaoongoza hija hii ni "Linda Maisha Yote" .

Alisema ni lazima kutambua na kuthamini utu wa mwanadamu kwa kuendelea kujenga na kuimarisha mshikamano wa upendo kwa ajili ya watu wenye shida mbalimbali duniani. **REDIO VATICAN**

# Ofisa anaswa kwa tuhuma ya rushwa 270,000/-

**Na Gedion Mwakanosya,** SONGEA

OFISA Kilimo wa Halmashauri ya Manispaa Songea mkoani Ruvuma, Edwin Ndunguru, anashikiliwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), mkoani humo kwa tuhuma za kuomba na kupokea rushwa ya Sh. 270,000 toka kwa mfanyabiashara wa samaki.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mjini hapa, Mkuu wa Takukuru mkoani Ruvuma, Yustina Chagaka, alisema tukio hilo lilitokea Oktoba 10, mwaka huu na ofisi yake ilipokea taarifa yenye malalamiko dhidi ya Ndunguru ambaye ni Ofisa kilimo na Kaimu Ofisa uvuvi wa Halmashauri ya Manispaa Songea kuwa anafanya vitendo vya kuwatoza wafanyabiashara wa samaki ushuru wa matenga ya samaki wabichi kwa njia ya rushwa.

Alifafanua kuwa Ndunguru pamoja na kujua kuwa wafanyabiashara hao wanalipa ushuru halali wa Sh. 4,000 kwa kila tenga, alikuwa akiwatoza fedha zaidi Sh. 50,000 kwa tenga la samaki wabichi kwa madai kuwa hiyo ni faini kwa kosa la kubeba samaki kwenye magari ambayo siyo maalumu kubebea bidhaa hiyo.

Alidai kuwa fedha hizo alikuwa akichukua kujinufaisha binafsi.

Chagaka alieleza kuwa Oktoba 11, mwaka huu, Ndunguru katika mazingira ya rushwa alimuomba mfanyabiashara mmoja ambaye jina lake limehifadhiwa Sh. 324,000 ili kulipia matenga ya samaki ambayo yalikuwa yameshafirishwa kutoka Mbambay kwenda Songea mjini na katika mtego ulioandaliwa na Takukuru, alipokea Sh. 270,000 toka kwa mfanyabiashara huyo na kukamatwa.

Alisema kuwa uchunguzi uliofanyika umethibitisha kwamba mtuhumiwa alitenda makosa ya rushwa kinyume na kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa.




Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS), Dk. Leonard Maboko (kushoto), akifanya mahojiano na Mtangazaji wa EATV/Radio, Samson Charles, jijini Dar es Salaam hivi karibuni, ambapo alielezea hatua zinazofanywa na tume hiyo katika kupambana na maambukizi ya Virusi vya Ukimwi kwa makundi mbalimbali hususani vijana, kuelekea maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani Desemba Mosi. **PICHA: EATV/RADIO**

# Wachimbaji wapewa mbinu kisasa

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya kuendeleza wachimbaji wadogo nchini (FADev), imeanza kuwaelimisha wachimbaji kufanya uchimbaji mdogo kuwa biashara badala ya kuchimba kwa mazoea.

Aidha, hatua hiyo itawawezesha kutimiza azma ya serikali ya kuwawezesha wachimbaji wadogo kukua kiuchumi kujipatia kipato na kulipa kodi.

Katibu mtendaji wa taasisi hiyo, Tina Mwasha, akizungumza na Nipashe, alisema kilio cha wachimbaji wadogo ni cha muda mrefu, na kwamba serikali haiwatambui, huku akifafanua inatokana na wachimbaji kufanya kazi kiholela bila kuweka akiba na kubaki wakilaumu serikali kuwa haiwathamini.

Akitoa elimu kwa wachimbaji wadogo zaidi ya 50 wa migodi mitatu iliyopo Msasa, Nyakagwe na Nyarugusu mkoani Geita, Mwasha alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwawezesha wachimbaji wadogo kurasimisha kazi zao na kutunza kumbukumbu ili waweze kutambulika na kupata fursa ya kupata mkopo kutoka kwenye taasisi za fedha.

"Wachimbaji wadogo awali walitegemea serikali iwafanyie kila kitu walilalamika lakini mafunzo haya yamewasaidia wanatunza fedha, wanaweka kumbukumbu na sasa wameacha kuilaumu serikali wametambua hii ni biashara kama biashara nyingine sio kusubiri kupewa vifaa bure wapo tayari hata kukopeshwa walipe kidogokidogo," alisema Mwasha.

Alisema licha ya serikali kuingia kwenye mkataba wa minamata ambao umelenga kupunguza matumizi ya zebaki, bado wachimbaji wadogo wengi hawajui madhara yaliyopo na kuzitaka taasisi binafsi kushirikiana na serikali kutoa elimu ya madhara ya zebaki na kutafuta njia mbadala ya kuwawezesha wachimbaji kuendelea na shughuli zao bila kutumia kemikali hiyo.

Mmoja wa wachimbaji waliohudhuria mafunzo hayo, Saanane Chai kutoka mgodi wa kilimo kwanza uliopo Msasa, alisema mafunzo hayo yamewasaidia kuanza kutunza kumbukumbu tofauti na awali walipokuwa wakipata fedha wanatumia wakiamini watachimba tena na kupata nyingine.

"Mafunzo ya usalama kazini yamesaidia kupunguza ajali mgodini tumejifunza mengi na sasa tumeacha kuchimba kiholela, tunaingia kwenye uchimbaji wa tija japo bado changamoto kubwa ni mtaji, na kama tutakopeshwa tutaacha kuchimba kwa kubahatisha tuchimbe kisasa," alisema Chai.

Mchimbaji mwingine, Renatus Nsangano, aliyeanza kubadili uchimbaji kwa kutunza mazingira kwa kuachana na mashimo yanayotumia miti na kutumia saruji, ali eleza mfanikio aliyoyapata.

"Kwa sasa nimeanza kuhama kutoka kwenye matumizi ya zebaki na kuanza teknolojia ya gold kisha kuchenjua dhahabu ambayo sasa ipo kwenye majaribio," alisema.

## Mbowe adaiwa kuugua dengue

INATOKA UK. 2

"Mheshimiwa hakimu tunaamini kwamba tangu Novemba 22, mshtakiwa aliporuhusiwa na kwa kuwa hakuna maelekezo mengine ya daktari atakuwa amepumzika vya kutosha na amepona," alidai Nchimbi.

Hakimu Simba alisema kuwa afya ya mshtakiwa ni jambo la msingi hivyo aliahirisha kesi hiyo kwa siku ya jana na leo na kuendelea kwa siku tano mfululizo.

Alisema kesi hiyo itaendelea kusikiliza Novemba 28, 29 na Desemba 2, 3 na 4 mwaka huu, dhamana za washtakiwa zinaendelea.

Washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Naibu Katibu Mkuu Zanzibar, Salum Mwalimu, Mbunge wa Kibamba, John Mnyika, Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche, Mbunge wa Kawe, Halima Mdee na Mbunge wa Bunda, Esther Bulaya.

Wengine ni Mbunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa, Mbunge wa Tarime Mjini, Esther Matiko na Katibu Mkuu wa chama hicho, Dk. Vincent Mashinji.

## Wataka mitaala linganifu sekta afya

**Na Beatrice Shayo**

WATAALAMU wa afya wametaka ulinganifu wa mtaala katika vyuo vya afya utakaosaidia uboreshaji huduma za utoaji afya nchini.

Mratibu wa Mradi wa Mageuzi katika utoaji mafunzo kwa wataalam wa afya Tanzania (THET), Dk. Nathanael Sirili, alisema kuwapo kwa ulinganifu wa mtaala kutasaidia kuboresha huduma za afya, kuliko ilivyo sasa kila mmoja hutoa huduma kutokana na alivyofundishwa chuo alichotoka.

"Lengo kubwa ni kutengeneza mazingira ya kimtaala ya kuwafundisha wataalamu ambayo yataboresha huduma za afya nchini, msingi wetu mkubwa ni kuboresha huduma ili Mtanzania na mtu yeyote aweze kupata huduma zenye ubora, tunafanya hivyo kwa kutengeneza mtaala linganifu," alisema.

Dk. Sirili alisema kumekuwa na ongezeko kubwa la wahitimu wa afya nchini, hivyo ni vizuri wakawa wanatoa huduma za afya kwa viwango vya kufanana kwa kuwa sekta hiyo ni muhimu katika jamii.

Ofisa Utawala wa kitengo cha Udahili kutoka Chuo cha Madakatari, Cuhas-Bugando, Mariam Nhaluke, alisema kumekuwa na ongezeko la madakatari kila mwaka ikilinganishwa na miaka ya nyuma. Alisema ubora wa elimu una changamoto baina ya chuo na chuo, hivyo mradi huo utawasaidia kutoa madaktari wenye viwango kwa kuwa italeta changamoto kwa baadhi ya vyuo vinavyozalisha madaktari wasiokuwa na viwango vinavyotakiwa.

Vile vile, alisema kuna tofauti mtu anapokwenda kupata huduma za afya madaktari wanatofautiana katika kutoa huduma hiyo kwa sababu kila mmoja amepewa elimu tofauti.


**TANGAZO**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


## *NIPASHE NI JIBU LAKO*

**NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO**
**KWA BEI NAFUU SANA**
**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**au piga simu: 0767 223311**


## KUPOTEA KWA CHETI




**.UIS BENEDICTO** anatangaza ːupotelewa na cheti cha kidato cha nne ːhenye index namba S0152-0066 ːilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa ːupitia SHULE YA SEKONDARI ;HINYANGA mwaka 2000.

Yeyote atakayekiona
atoe taarifa kituo cha polisi.

Control No. 9910810817082.

## KUPOTEA KWA CHETI CHA UALIMU



**VALENTINA HINGI** anatangaza kupotelewa na cheti cha Ualimu chenye namba E0509-0180 kilichotolewa na MATOGORO TTC mwaka 2005.

Yeyote atakayekiona atoe
taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**PWA/BAG/RB/413758/2019.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo: MIKONGENI - MVOMERO (W).

Usimamizi wa mirathi No; 07/2019
Ombi la ELIZA SHABANI SOMVI Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu SHABANI KONDO SOMVI

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 18/11/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 28/10/2019

115533802

**JAMHURi YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika Mahakama ya mwanzo DODOMA MJINI**

**<u>Usimamizi wa mirathi NA. 80/2019</u>**

Ombi la **ISSA ALLY SAID** kuteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi marehemu **YASIN ALLY SAID KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA TANZANIA BARA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnano tarehe 05-12-2019 kabla ya muombaji kuteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.

Tarehe25/11/2019

215533702

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI MOROGORO**

Usimamizi wa mirathi No; 241/2019
Ombi la **SEIF MWINYI ALLY** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **ABDALLAH MWINYI ALLY**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 10/12/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 25/11/2019

115533902

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**BUSINESS REGISTRATIONS AND LICENSING AGENCY**

**Notice of Appointment of Liquidator: Voluntary Winding-Up: for insertion in Gazette**
**ursuant to section 360 of the Companies Act 2002**

ompany Number……………….123193

ompany Name (in Full) ………U-TURN SALES AND IARKETING

ype of Liquidation: ……………...MEMBERS

ddress of Registered Office:…….

**LOT NO 1&3 BLOCK "M" NKURUMAH STREET**
**NYAMAGANA DISTRICT, MWANZA CITY**
**P.O.BOX 2162,**
**MWANZA**

quidator(s)Name (s) ………………PAUL N.BOMANI

quidator(s) Address(es):…………………

**Plot No. 30/31 Block "L" Nkuruma/Uhuru Street**
**P.O.Box1596, Mwanza, Tanzania**
**Telephone: +255 754 243 246, +255 659 793 096**
**Email: <u>bomanip@yahoo.com</u>**

**ate of appointment:** 01st November 2019


**y whom appointed:** U-turn Sales Marketing through Board Resolution

gned……………….......Date: 01st November 2019

**IAME IN BLOCK LETTERS: PAUL N. BOMANI**
(by each liquidator in more than one)

115534702

## VYETI VIMEPOTEA



**HASHIMU SUYA anatangaza** kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0119-0026** kilichotolewa na KIBAHA SEKONDARI mwaka 2004. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0110-0594** kilichotolewa na ILBORU SEKONDARI mwaka 2007. Certificate of Bachelor of Commerce kilichotolewa na UNIVERSITY OF DAR ES SALAAM mwaka 2010.

Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi.
**Control No. 9910810810292.**

**U-TURN SALES AND MARKETING**
**COMPANY NO. 123193**
**P.O.BOX 2162,**
**MWANZA**

**NOTICE OF RESOLUTION TO WIN UP VOLUNTARILY**

Pursuant to section 334(1) of the Companies Act, Cap 212 of 2002, We U-TURN SALES AND MARKETING (hereinafter called "the Company") hereby give notice to the general public that on 01st day of November 2019 the shareholders of Company resolved to wind up the Company voluntarily pursuant to section 333(1) (1) of the Companies Act.

115534102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO DODOMA MJINI**
**USIMAMIZI WA MIRATHI NA. 87/2019**

OMBI LA ATHANAS SALEHE NGOILA KUTEULIWA KUWA
MSIMAMIZI WA MIRATHI MAREHEMU DEUS ATHANAS NGOILA

KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA TANZANIA BARA

WATU WOTE WANAODAI KUWA NA MAHUSIANO WOWOTE NA MIRATHI YA MAREHEMU HUYO WANAALIKWA KUJA NA KUHUDHURIA KESI WAKITAKA MNAMO TAREHE 16-12-2019 KABLA YA MUOMBAJI KUTEULIWA KUWA MSIMAMIZI WA MIRATHI HIYO.

WOSIA WA MAREHEMU HUYO UPO MAHAKAMANI WAWEZA KUKAGULIWA. TRH 22/11/2019

115534202


***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0767 223311***

***Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# ZIDANE AANGUKIA MASHABIKI MADRID WASIMZOMEE BALE




**MADRID,** Hispania

KOCHA Mkuu wa Real Madrid, Zinedine Zidane amewataka mashabiki wa timu hiyo kuacha kumzomea, Gareth Bale.

Bale alizidi kuwatibua mashabiki wa Los Blancos baada ya Jumanne iliyopita kushangilia kufuzu kwa Wales kucheza Euro 2020 akiwa na bendera iliyokuwa imeandikwa 'WALES. GOFU. MADRID. KWA MTIRIRIKO' jambo lililoonyesha vipaumbele vyake, kwamba Madrid ni ya mwisho kwake.

Hilo liliwatibua mashabiki wa Real Madrid waliomzomea mchezaji huyo alipoingizwa kwenye mechi ya ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Real Sociedad huko Bernabeu Jumamosi iliyopita ikiwa ni mechi yake ya kwanza kwenye timu hiyo tangu Oktoba 5.

Zidane alisema: "Natumaini hili halitaendelea hadi mwisho wa msimu."

"Tunawataka mashabiki kutuunga mkono kuanzia mwanzo hadi mwisho, hatuwezi kuendelea hivi.

"Watu wana haki ya kufanya wanachotaka, lakini ninachowaomba watusapoti. Kulikuwa na kelele nyingi sana za kumzomea Bale, anataka kubaki hapa na kufanya kila analoweza, na ndio maana tunapaswa kulizungumza hili."




# *Mourinho amkataa Ibrahimovic Spurs*

**LONDON,** England

JOSE Mourinho amekataa uwezekano wa usajili wa Zlatan Ibrahimovic kwa sababu ana "mshambuliaji bora nchini England" akimtaja, Harry Kane.

Ibrahimovic amekuwa akihusishwa na mpango wa kwenda kwa miamba hao wa London Kaskazini, baada ya Mourinho kutangaza kuchukua mikoba ya Mauricio Pochettino wiki iliyopita.

Wawili hao walifanya kazi kwa muda mfupi pale Inter msimu wa 2008-09 kabla ya kukutana tena pale Manchester United mwaka 2016.

Akizungumza kabla ya mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya jana, Jumanne kati ya Spurs dhidi ya Olympiacos, Mourinho alimwagia maji baridi kwenye uvumi huo, kuhusu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 38, ambaye kwa sasa ni mchezaji huru.

"Nina mahusiano mazuri na Ibrahimovic," alisema. "Ni mchezaji anayevutia, mtu wa aina yake, lakini naweza kusema hakuna nafasi.

"Tuna mshambuliaji bora England. Tuna washambuliaji wawili au watatu bora zaidi duniani.

# Pochettino aongoza wanaowaniwa Arsenal

**LONDON,** Engaland

MAURICIO Pochettino anaongoza katika orodha ya makocha wanaotakiwa na Arsenal kwa ajili ya kuchukua nafasi ya Unai Emery, ESPN.

Emery amekalia kuti kavu Arsenal baada ya Jumamosi kutoka sare ya tatu mfululizo Ligi Kuu England katika mechi dhidi ya Southampton, na inasemekana Arsenal imeanza mchakato wa kumpata kocha ambaye atachukua nafasi yake.

Utakuwa usajili wenye utata kutokana na Pochettino kuwa kipenzi cha mashabiki wa Spurs - timu yenye upinzani wa jadi na Arsenal, lakini mabosi wa Arsenal wameanza kushawishika kuwa kocha huyo raia wa Argentina anaweza kuwa suluhisho la matatizo yao.

Kulikuwa na mpango kutoka kwa mabosi wa Arsenal kumbakiza Emery mpaka mwishoni mwa msimu, lakini kupatikana kwa Pochettino kumewashawishi kubadilisha mawazo na sasa inasemekana wameanza kumnyatia kocha huyo wa zamani wa Espanyol na Southampton.

Mkurugenzi wa Soka wa Arsenal, Raul Sanllehi pamoja na Mkurugenzi wa Ufundi, Edu Gaspar wamezidi kushangazwa na mwenendo mbovu unaoendelea kuiandama kwa kasi klabu hiyo ya Kaskazini mwa London.

Pochettino aliondolewa Jumanne iliyopita na nafasi yake kuchukuliwa na Jose Mourinho saa 12 baadaye, huku akilipwa kiasi cha pauni milioni 12.



HABARI MICHEZO

# Guardiola hataki Arteta aondoke City

**MANCHSTER,** England

PEP Guardiola hajui kama Mikel Arteta atabakia kama msaidizi wake wakati ripoti zikieleza kwamba, amekuwa anawaniwa na Arsenal.

Mchezaji huyo wa zamani wa 'Washika Bunduki' wa London, Arteta alijiunga na kikosi cha Guardiola mwaka 2016 na amekuwa na mafanikio makubwa pale Manchester City.

Arteta, ambaye alitumia miaka mitano akicheza Arsenal baada ya kusajiliwa akitoka Everton mwaka 2011, alikuwa akihusishwa na mpango wa kuchukua mikoba ya Arsene Wenger mwaka 2018, kabla ya Unai Emery kuchukua nafasi hiyo.

Licha ya kutinga fainali kwenye Ligi ya Europa msimu uliopita, kocha huyo wa zamani wa Paris Saint-Germain, Emery ameshindwa kuwa na ushawishi, huku ripoti zikieleza kwamba, mashabiki hawamtaki.

Arteta amekuwa akitajwa zaidi kama ndiye chaguo la kwanza la kwenda kuchukua kazi kama Emery akiondoka.

Na huku akitaka Arteta aendelee kubaki City, Guardiola anafahamu kwamba inaweza kuwa ngumu kumbakiza Mhispania mwenzake huyo kwenye benchi hilo la ufundi.

"Emery ni kocha wa Arsenal," alisema Guardiola akiwaambia waandishi wa habari wakati alipoulizwa kuhusu ripoti za Arteta kurudi kule London Kaskazini.

"Bila shaka (Mikel) atakuwa kocha hivi karibuni au baadaye, kama ningekuwa kwenye nafasi yake kama kocha msaidizi na umri wake, nisingetaka haraka kuwa kocha, lakini sasa tunakwenda kumaliza msimu huu. Siku za usoni sijui nini kitatokea."






# GRIEZMANN: UHUSIANO NA MESSI UNAIMARIKA

**BARCELONA,** Hispania

ANTOINE Griezmann amebainisha kwamba anakosa kujiamini kwa kufanya maamuzi, huku nyota huyo wa Barcelona akisema kwamba mahusiano yake binafsi na Lionel Messi yanaimarika.

Griezmann hajawa kwenye ubora wa juu tangu alipotua pale LaLiga akitokea Atletico Madrid kwa ada ya uhamisho ya euro milioni 120, uhamisho uliofanyika mwanzoni mwa msimu.

Mchezaji huyo wa Ufaransa amefunga mabao manne kwenye LaLiga na ametoa pasi za mwisho tatu kwa Barca, hata hivyo, kiwango chake bado hakijaimarika.

Kuelekea kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya leo, Jumatano dhidi ya Borussia Dortmund, Griezmann ameiambia UEFA.com: "Naendelea kujifunza kuelewa namna gani wachezaji wenzangu wanavyocheza kwa kuwa kila kitu kipya kwangu.

"Bado naendelea kusoma na kukimbia na mpira kama Luis Suarez, Leo Messi na Ousmane Dembele pamoja kwenye nafasi ya kiungo. Ni mpango wangu kuhakikisha kila kitu kina kwenda sawa na ninajitahidi kwa hali na mali kuwa kwenye kiwango changu cha juu.

"Kwa wakati huu ninapopata mpira huwa nakosa kujiamini wakati wa kutoa pasi au kupiga mpira golini, nina uhakika hiki ni kitu ambacho kitabadilika ndani ya muda mfupi."

Mengi yamezungumzwa kuhusu mahusiano kati ya Griezmann na nahodha wa Barca, Messi.

Mwezi uliopita, Griezmann alibainisha kwamba, ni "ngumu" kuunganika na Messi kwa sababu wote wawili si wazungumzaji.

"Mimi nina aibua na kuna wakati nina matatizo ya kuzungumza mbele ya watu wengine," alisema Griezmann.

"Ni ngumu kwangu kuanzisha majadiliano. Luis (Suarez), Leo na mimi mwenyewe tunapata chakula pamoja na mahusiano yetu yanaweza kuimarika zaidi."

# *Mbappe nenda Real - Karembeu*

**PARIS,** Ufaransa

KIUNGO wa zamani wa Real Madrid, Mfaransa Christian Karembeu, amemtaka nyota wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe kujiunga na miamba hao wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga.

Mbappe ameendelea kuhusishwa na mpango wa kujiunga na Madrid huku timu hizo jana, Jumanne zilikutana kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya katika Uwanja wa Santiago Bernabeu.

Kocha wa Madrid, Zinedine Zidane hajawahi kuficha siri yake ya kutaka kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 raia wa Ufaransa, akisema: "Tayari nina mapenzi naye."

Mfaransa Karembeu, ambaye alishinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya mara mbili wakati akiwa pale Madrid, sasa anamtaka Mbappe kwenda kujiunga na kikosi hicho cha Zidane.

"Nafikiri usajili unaofuata kwa (Kylian) Mbappe utakuwa ni kwenye Ligi ya Hispania La Liga," alisema Karembeu.

"Ndio, tunajua kwamba, (Ferland) Mendy yupo Madrid, (Ousmane) Dembele (Barcelona), (Karim) Benzema (Madrid). Na kuna uvumi kwamba, kiungo wa Manchester United, Paul Pogba atakwenda pale.

"(Antoine) Griezmann (Barcelona) tayari ameshaonyesha ujuzi wake. Kwa nini isiwe kwa Mbappe?"

Mbappe - mshindi wa Kombe la Dunia mwaka 2018 - amefunga mabao matano kwenye Ligue 1 msimu huu katika mechi tisa alizocheza kwenye mashindano yote chini ya kocha, Thomas Tuchel pale PSG.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# GUARDIOLA: NI MUUJIZA AGUERO KUIVAA UNITED

**Atakuwa nje kwa michezo michache, sijui vizuri ni kwa muda gani, wiki chache, ila...**

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola amethibitisha mshambuliaji Sergio Aguero atakuwa nje "kwa wiki chache" na akaongeza kuwa "anahitaji muujiza" kuwa fiti kucheza 'dabi' ya Manchester kutokana na majeraha ya nyama za paja aliyoyapata Jumamosi kwenye mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Chelsea.

**Straika huyo wa Argentina, Aguero, 31, alitolewa katika dakika ya 77 wakati wakishinda 2-1 kwenye mechi hiyo.**

Aguero, ambaye alikosa mechi tano msimu uliopita kutokana na matatizo ya nyonga ameshafunga mabao 13 katika mechi 16 za mashindano yote alizocheza msimu huu.

Hata hivyo, katika mkutano na waandishi wa habari jana kuelekea mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Shakhtar Donetsk, Guardiola alithibitisha kuwa Aguero atakuwa nje kwa wiki chache, ikiwa na maana straika huyo, ambaye ameshafunga mabao tisa kwenye Ligi Kuu msimu huu, atakosa mchezo wa 'dabi' dhidi ya Manchester United Desemba 7, mwaka huu.

"Ndiyo," Guardiola alikubali wakati alipoulizwa kama City itamkosa Aguero kwenye mechi hiyo ya dabi ya Manchester.

"Atakuwa nje kwa michezo michache, sijui vizuri [kwa muda gani], wiki chache, ila atakuwa nje."

Kocha huyo aliongeza Aguero "atahitaji muujiza" kuwa fiti kwenye Manchester dabi Desemba.

Gabriel Jesus, ambaye msimu huu amekuwa akipata nafasi zaidi akitokea benchi, anatarajiwa kuanzishwa zaidi kwa kipindi hiki ambacho Aguero atakosekana.

Nyota huyo wa kimataifa wa Brazil, ambaye amefunga mabao matano katika mechi 16 alizocheza, alisema: "Sina furaha Sergio kuumia.

"Sipendi hilo wakati rafiki yangu anapoumia, ila kila siku ninajituma zaidi na nipo tayari."

Aguero anakuwa mchezaji mpya wa City kuumia kwa sasa, kufuatia klabu hiyo tayari ilishawakosa beki wa kati Aymeric Laporte, winga Leroy Sane na beki wa pembeni Oleksandr Zinchenko.

## ZISIKUPITE

### HOFU MASTAA KUKIMBIA

WAKURUGENZI wa Arsenal wanahofia wachezaji wao nyota watalazimika kuamua mustakabali wao wa baadaye vinginevyo kama kocha Unai Emery ataendelea kuiongoza klabu hiyo msimu ujao. ***(Mail)***

### AMSIKILIZIA GUARDIOLA

MSHAMBULIAJI wa England, Raheem Sterling, 24, anasubiri kuona kama kocha wa Manchester City, Pep Guardiola atajifunga kuendelea kuinoa klabu hiyo kabla ya yeye kusaini mkataba mpya. ***(FourFourTwo)***

### ZIDANE AFUNGUKIA MBAPPE

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane amesema ana "mapenzi" na mshambuliaji wa Ufaransa Kylian Mbappe, 20, wakati kikosi chake jana kikiikaribisha Paris St-Germain kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(ESPN)***

### KANTE: SABABU KUIKATAA PSG

KIUNGO wa Chelsea na N'Golo Kante, 28, amesema uamuzi wake wa kutojiunga na mabingwa wa Ufaransa, PSG ilikuwa ni kwa sababu ya "uchaguzi kimchezo". ***(Canal Plus, via Mirror)***

### MOURINHO AMPA KAZI MENDES

KOCHA wa Tottenham, Jose Mourinho amemtaka wakala Jorge Mendes kuendelea kumfahamisha juu ya beki wa Benfica, Mreno Ruben Dias, 22, na kiungo raia mwenza Bruno Fernandes, 25, wa Sporting Lisbon. ***(90min)***

### SILVA KUPEWA MBILI EVERTON

KOCHA wa Everton, Marco Silva atapewa mechi mbili za kuongoza timu hiyo wakati wenye hisa wakubwa, Farhad Moshiri na mwenyekiti Bill Kenwright wakijadili mbadala. ***(Mail)***

### WEST HAM YAMTEGA WILDER

WEST Ham inamtaka kocha wa Sheffield United, Chris Wilder kuwa kocha wao ajaye, endapo itaamua kumtimua Manuel Pellegrini anayeinoa kwa sasa. ***(Mirror)***

### AONYA KWA ARTETA

PEP Guardiola amezionya klabu zinazovutiwa na msaidizi wake, Mikel Arteta, ambaye ameibuka kuwa kinara wa makocha wanaopewa nafasi ya kuinoa Arsenal na Everton, kwamba atabaki hapo City kwa angalau kipindi chote cha msimu kilichobaki. ***(Times)***

### UNITED KUWEKA REKODI JEZI

MANCHESTER United inakaribia kuweka rekodi ya dunia ya udhamini wa jezi yao utakaoiingizia pauni milioni 70 kwa mwaka kutoka Kampuni ya Haier ya China. ***(Sun)***

### LEICESTER KUMFUATA AJER

LEICESTER City inapanga kumfuata beki wa Celtic, Mnorway Kristoffer Ajer, 21, ikiwa na pauni milioni 20 katika usajili wa dirisha la Januari. ***(90min)***

### PELLEGRINI AONYWA WEST HAM

KIKAO cha Bodi ya West Ham, kimemwonya kocha wao, Manuel Pellegrini kuhakikisha anaboreshe matokeo ya timu hiyo. ***(Telegraph)***

HABARI MICHEZO

## Cecafa kuchaguana Kampala Desemba

**Na Somoe Ng'itu**

UCHAGUZI Mkuu wa Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (Cecafa), umepangwa kufanyika Desemba 18 mwaka huu jijini Kampala nchini Uganda, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Cecafa, Nicholas Musonye, amesema kuwa uchaguzi huo utafanyika kwa kutumia katiba mpya ambayo ilipitishwa kwenye mkutano mkuu uliopita wa baraza hilo.

Musonye alizitaja nafasi zitakazogombewa katika uchaguzi huo kuwa ni ya Rais, Makamu wa Kwanza wa Rais, Makamu wa Pili wa Rais na Wajumbe watatu watakaoingia kwenye Kamati ya Utendaji.

Alisema kuwa tayari nchi wanachama wa Cecafa wameshaanza maandalizi ya kuelekea katika mchakato huo, ambao anaamini utaongeza nguvu katika utendaji.

"Tulianza na jukumu la kubadilisha katiba kwa kufuata mwongozo kutoka katika Shirikisho la Soka Afrika (Caf), na sasa tunaelekea katika uchaguzi, baadaye watafuata pia wanachama wetu, hii itasaidia kuwaweka wanachama kwenye njia inayofanana, na tunashukuru Fifa pia wanatufuatilia, hizi ni habari njema," alisema Musonye.

Alizitaja nchi wanachama zitakazotoa wagombea na kushiriki katika uchaguzi huo ni pamoja na Tanzania Bara, Zanzibar, Uganda, Kenya, Rwanda, Burundi, Ethiopia, Eritrea, Djibouti, Somalia, Sudan na Sudan Kusini.

## Muuaji Kili Queens achekelea kisasi

**Na Shufaa Lyimo**

MFUNGAJI Bora wa Mashindano ya Afrika Mashariki na Kati (Cecafa Challenge Cup) kwa Wanawake, kutoka timu ya Taifa ya Kenya, Jentrix Shikangwa, mbali na kutwaa Kiatu cha Dhahabu katika michuano hiyo, amesema kilichomfurahisha zaidi ni wao kulipiza kisasi kwa Kilimanjaro Queens.

Timu hizo juzi zilikutana katika mchezo wa fainali uliopigwa Uwanja wa Azam FC, na Kenya kuibuka na ubingwa baada ya kushinda kwa mabao 2-0, yote yakizamishwa nyavuni na Jentrix, moja kwa penalti na lingine mkwaju wa mbali.

Akizungumza jijini Dar es Salaam baada ya mechi hiyo, Jentrix alisema kilichowafanya kuibuka na ushindi, ni kutokana na Kilimanjaro Queens kupoteza umakini uwanjani.

"Tanzania wangetulia wangefunga kwa sababu walipata nafasi nyingi za wazi, lakini walishindwa kuzitumia," alisema Mkenya huyo aliyemaliza michuano hiyo akiwa na mabao 10 kileleni mwa orodha ya wafungaji bora.

Alisema, hajawahi kuwafuatilia Tanzania Bara isipokuwa walikuwa wanafuatiliwa na walimu wao.

Alisema idadi ya mabao aliyoyapata ni juhudi binafsi alizozitumia pamoja na kumsikiliza mwalimu wake kwa makini.

# YANGA 20 WAIFUATA ALLIANCE FC KIRUMBA

**Na Shufaa Lyimo**

YANGA imeanza ratiba ngumu ya kula viporo vyake vya Ligi Kuu Bara, ambapo keshokutwa Ijumaa itashuka Uwanja wa CCM Kirumba kuivaa Alliance FC kabla ya kurejea jijini Dar es Salaam kuvaana na KMC FC katika Uwanja wa Uhuru Jumatatu ijayo.

Miamba hiyo ya mtaa wa Twiga na Jangwani jijini Dar es Salaam, ambayo ilitarajiwa kuondoka leo asubuhi kuelekea Mwanza, hadi sasa imeshuka dimbani mara sita na kujikusanyia alama 13 zilizoiweka katika nafasi ya 13 kwenye msimamo wa Ligi Kuu, wakati huu ikiivaa Alliance iliyopo nafasi ya tano baada ya kucheza mechi 11 na kuvuna pointi 17.

**Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli alisema baada ya mchezo huo, moja kwa moja watarejea Dar es Salaam kujiandaa tena kukutana na timu ya KMC FC hapo Jumatatu.**

"Kikosi chetu kitaondoka kesho asubuhi (leo) kuelelea Mwanza kikiwa na wachezaji kama 20 hivi, tayari kwa ajili ya kujiandaa kukutana na timu ya Alliance FC, maandalizi yetu yapo vizuri," alisema Bumbuli.

Alisema wameamua kuondoka na wachezaji wachache ili wengine wabaki jijini Dar es Salaam wakiendelea kujinoa kwa lengo la kukutana na timu ya KMC FC.

Bumbuli alisema jana timu imeendelea na mazoezi kwenye Uwanja wa Uhuru ili kuwapa wachezaji utimamu wa mwili, kuelekea katika mchezo huo.

Kuhusu usajili wa dirisha dogo, alisema kuna baadhi ya wachezaji ambao wataachana nao, na kuongeza wengine ili kuboresha kikosi hicho.

"Tutaongeza na kuacha baadhi ya wachezaji katika usajili wa dirisha dogo ili kuziba mapengo ambayo tumeyaona yana mapungufu," alisema msemaji huyo.

Alisema jukumu zima la usajili lipo chini ya kamati ya ufundi na kuongeza kuwa, baada ya kumaliza mchezo wao dhidi ya KMC, kamati hiyo itakutana na kuanza kupanga mikakati ya usajili.



Mshambuliaji wa Kilimanjaro Queens, Mwanahamisi Omary 'Gaucho' (Jezi Na. 7), akipata upinzani mkali kutoka kwa beki wa Kenya, Ruth Ingosi katika mechi ya fainali ya Kombe la Cecafa kwa Wanawake iliyopigwa Uwanja wa Chamazi jijini Dar es Salaam juzi. Kenya ilishinda kwa mabao 2-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## *Kili Queens sasa yawazia Afcon*

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya timu ya Taifa ya Wanawake Tanzania Bara, Kilimanjaro Queens kuvuliwa ubingwa wa Kombe la Cecafa, uongozi wa timu hiyo umesema lengo lao sasa ni kutafuta nafasi ya kushiriki mashindano makubwa zaidi wakianza na fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) kwa Wanawake.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Mwenyekiti wa Soka la Wanawake Tanzania, Amina Karuma, alisema kwa sasa mikakati yao ni kuhakikisha timu hiyo inashiriki mashindano makubwa kutokana na uwezo mkubwa wanaoonyesha.

Alisema hiyo itasaidia wachezaji kupata nafasi ya kununuliwa kwenda kucheza nje ya nchi na kuzidi kusonga mbele, lakini kuwa msaada mkubwa pindi watakapoitwa timu ya taifa.

Akizungumzia mchezo uliopita, alisema wamejifunza mengi kupitia mashindano ya Afrika Mashariki na Kati (Cecafa Challenge Cup) kwa Wanawake, yaliyokuwa yakifanyika kwenye Uwanja wa Azam Complex Chamazi nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam.

"Tumejifunza mambo mengi katika mashindano ya Wanawake ya Cecafa, vile vile wachezaji wetu wamejitahidi mpaka kushika nafasi ya pili ingawa lengo letu lilikuwa ni kutwaa ubingwa huo kwa mara ya tatu mfululizo," alisema mwenyekiti huyo.

Amina alisema mpira wa soka la Wanawake Tanzania umekua na kudai wachezaji wadogo ndio wana uwezo mkubwa wa kucheza mpira.

"Mimi nitakaa na mwalimu wangu [Bakari Shime] tutajua jinsi ya kujipanga kurekebisha makosa yaliyojitokeza katika mchezo wetu wa fainali," alisema.

Kwa upande wa mchezaji wa timu hiyo, Mwanahamisi Omary 'Gaucho', ambaye alipata tuzo ya Mchezaji Bora wa mashindano hayo, alisema tunzo hiyo kwake ni historia kubwa pamoja na wachezaji wenzake.

"Hii tunzo ni historia kubwa kwangu kwani kulikuwa na wachezaji wengi katika mashindano, lakini mimi nikaonekana kuwa bora zaidi," alisema Mwanahamisi.

Michezo
Jumatano Novemba 27, 2019
Nipashe



Guardiola: Ni muujiza Aguero kuivaa Utd

HABARI UK.30

WALETENI HAO...



Wachezaji wa Liverpool, beki Virgil van Dijk (mbele) na Mohamed Salah (katikati) wakijifua. Mabingwa watetezi hao wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, leo wataikaribisha Napoli katika Uwanja wa Anfield kwenye mechi ya hatua ya makundi ya michuano hiyo. **PICHA: MTANDAO**

## Dante aliamsha sakata Yanga SC

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kukaa kimya kwa muda mrefu, hatimaye beki wa Yanga, Andrew Vincent 'Dante' ameamua kuliamsha kwa 'moto' sakata lake la kudai kulipwa fedha zake za usajili katika klabu hiyo.

Pamoja na kutakiwa kurejea kazini Yanga ili aendelee kulipwa kwa mafungu fedha hizo ambazo zinaelezwa ni takriban Sh. milioni 40, na Dante kugoma akitaka chake kwanza, beki huyo sasa ameelezwa kutinga Shirikisho la Soka nchini (TFF) kuishtaki klabu hiyo.

Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, akizungumzia sakata hilo, amesema kwa namna hali ya kiuchumi ilivyo ndani ya klabu yao ni vigumu kumlipa Dante kiasi chote hicho cha pesa kwa wakati mmoja.

Bumbuli alisema awali walikubaliana naye kuwa watakuwa wanamlipa kidogo kidogo, lakini walishangazwa na namna alivyoamua kwenda TFF kushtaki jambo ambalo hata kama shirikisho hilo likitoa uamuzi bado utaangukia katika kumlipa kwa mafungu.

"Ukweli ni kwamba anaidai klabu na tulikubaliana tuwe tunamlipa kidogo kidogo, kwa sababu hali kwa sasa ilivyo, ni ngumu kumlipa kwa mkupuo, kwa sababu hata TFF kama ikiamua kutukata sehemu ya mapato ya mechi zetu za nyumbani bado anaweza akalipwa kama Sh. milioni tatu.

"Hivyo ni bora angerejea kikosini na sisi tungeweza kumlipa kwa awamu na haraka zaidi kuliko sisi kukatwa sehemu ya mapato," alisema.

# Simba, Yanga zaamshwa Caf

**Na Somoe Ng'itu**

●●● Siasa yatajwa chanzo kushindwa kufurukuta michuano hiyo ya Afrika, Azam yatakiwa kukaza msuli ili...

BAADA ya kuliongoza Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (Cecafa), kwa muda wa miaka 20, Katibu Mkuu Mkenya Nicholas Musonye amezitaka klabu za Simba na Yanga kuacha kuchanganya "siasa" na utawala wa mpira ili kufikia mafanikio kama klabu nyingine kongwe barani Afrika.

**Musonye, ambaye kwa taaluma ni mwandishi wa habari, alianza kuongoza katika nafasi hiyo tangu mwaka 1999 na mwaka jana akiwa jijini Kigali, Rwanda, alitangaza rasmi kuwa ataachia ngazi ifikapo Juni mwakani.**

Akizungumza na Nipashe katika mahojiano maalumu jana, Musonye, alisema Simba na Yanga zimekuwa ni klabu kubwa kwenye ukanda wa Cecafa, lakini zinachelewa kupata mafanikio kutokana na viongozi wake kutokuwa na msimamo kwenye maamuzi mbalimbali ndani ya timu hizo.

Musonye alisema umefika wakati kwa klabu hizo kujiendesha vizuri na anaamini zikifuata taratibu na weledi, timu hizo zitafika mbali kwenye michuano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho, kutokana na hazina walizonazo.

Kiongozi huyo amekiri kuwa klabu hizo zinapokosekana katika mashindano ya Klabu Bingwa Afrika Mashariki na Kati maarufu Kombe la Kagame, msisimko huondoka na hali hiyo humfanya kuwa mkali kwa kuhakikisha timu hizo zinashiriki michuano hiyo inayodhaminiwa na Rais wa Rwanda, Paul Kagame.

"Zinapokosekana Simba na Yanga katika mashindano ya Kombe la Kagame, huondoa msisimko na raha ya mashindano, hasa inapofanyika hapa nyumbani Tanzania, huwa nawajibika kuwa mkali kwao, lakini simwonei mtu, kila siku huwa nasimama kwenye kanuni na sheria, nawakumbusha kuacha maneno maneno, wajiandae ili wafanye vizuri wanapokwenda katika mashindano ya Caf," alisema Musonye.

Huku akiwa anatarajia kuacha kijiti kwa kiongozi mwingine atakayepitishwa na mabosi wa Cecafa, Musonye ameitaka Azam FC kuendelea kupambana kuhakikisha inatoa ushindani kwa vigogo hao wawili wa soka hapa nchini.

"Ninaitaka Azam isilale, ijiimarishe na kupambana na Simba na Yanga, isikubali hao wawili watawale soka la Tanzania, presha yao inasaidia kuwaongezea presha ya kujijenga, isipofanya hivi, watawafanya wasiongeze bidii, pia kupambana kwao kutaongeza msisimko kwenye soka na ligi kwa ujumla," Musonye alisema.

### AJIVUNIA AFCON 2019

Musonye pia amejivunia chini ya uongozi wake, mwaka huu Ukanda wa Cecafa umefanikiwa kupeleka timu nne katika fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon 2019), ambazo zilifanyika nchini Misri.

Alisema timu hizo nne ambazo ni Tanzania, Kenya, Burundi na Uganda, zimepata nafasi ya kufuzu kucheza fainali hizo kutokana na maandalizi waliyoyapata kupitia mashindano ya Kombe la Chalenji.

"Mashindano yetu ya Kombe la Chalenji yamekuwa ni moja ya fursa ya kuwajenga wachezaji na kuwa tayari pale wanapokutana kuwania nafasi za kucheza Afcon, ni daraja ambalo pia limechangia kuwatoa nyota mbalimbali ambao walipata klabu za Ulaya," aliongeza kiongozi huyo.

Musonye aliwataja baadhi ya wachezaji ambao waling'ara na wengine wanaendelea kufanya vema Ulaya na walianzia Cecafa ni pamoja na Mark Donald Mariga, Victor Wanyama, Dennis Onyango na nahodha wa Taifa Stars ya Tanzania, Mbwana Samatta.

Aliongeza kwa kuwataka viongozi wajao wa Cecafa kuhakikisha wanaendeleza mazuri ili wafanye vizuri zaidi katika mashindano mbalimbali wanayoshiriki.

### AJIPANGA KUWANIA UBUNGE

Baada ya kuondoka Cecafa, Musonye, amesema ataelekeza nguvu zake katika siasa na anatarajia kuwania kiti cha Gavana wa Western Kenya (Kakamega).

"Nimeshaanza maandalizi ya kuwania kiti huko nyumbani, mimi ni mwanachama wa ANC, lakini ninasubiri muungano wa vyama vyetu na nitajua nitasimama kupitia chama kipi, lakini nimejipanga kuingia kwa kishindo, uzinduzi wa kampeni yangu utakuwa na nguvu kama ya Tsunami," alisema.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >